**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Pili - Tarehe 8 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of Mzumbe University for the Year ended 30th June, 2004).*

Taarifa ya mwaka ya Utendaji na Hesabu za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mwaka 2003/2004 *(The Annual Report on the Activities of the Open University of Tanzania for the year 2003/2004).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 11

**Majimbo Yaliyo na Wabunge wa Upinzani**

**MHE. PHILEMON NDEMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa wako viongozi wa juu Serikalini ambao wametoa matamko kwamba Majimbo yaliyo na Wabunge wa Upinzani hayataletewa maendeleo na Serikali:-

(a) Je, hiyo ndiyo Sera ya Serikali?

(b) Je, Serikali inakusudia kuwachukulia hatua gani viongozi hao wanaoitia dosari Serikali yetu isiyo na ubaguzi?

(c) Je, sasa sio wakati muafaka kwa Serikali kutoa tamko rasmi la kufuta hisia walizo nazo wananchi kuwa Serikali ina ubaguzi wakati sio kweli?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mipango ya maendeleo katika Wilaya au Halmashauri nchini hutokana na mchakato unaofanywa wa kubainisha mahitaji mbalimbali ya maendeleo ambayo hufanyiwa uchambuzi na hatimaye kupata mpango mzima wa maendeleo wa eneo husika. Mchakato wa mipango ya aina hii huanzia ngazi ya chini kwa maana ya kijiji na kupanda ngazi ya Kata, Wilaya hadi Taifa.

Katika hatua hizo mbalimbali, mchakato huhusisha wadau wote wakiwemo wananchi, wataalam, wanasiasa na jamii kwa ujumla wake. Inapofikia ngazi ya Wilaya, mipango hiyo, hupata fursa ya kutengewa raslimali kwa utekelezaji wake lakini kwa kuzingatia uwezo wa Serikali uliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa maana ya Ofisi ya Rais, Mipango, Ubinafsishaji na Uwezeshaji, Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) wao ni wadau muhimu katika hatua za awali kabla hata mchakato huo kufikishwa katika vikao vya Bajeti ya Serikali na hatimaye katika Bunge lako Tukufu, ambalo ni chombo cha kusimamia ugawaji wa raslimali na usimamizi wa maendeleo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi ya ushirikishwaji katika mchakato mzima wa utayarishaji wa mipango yetu, uidhinishwaji wake, utekelezaji na usimamizi wake ulivyo wa uwazi, haiwezekani kwa kiongozi kuzuia utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika Majimbo au Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa au Jiji lolote nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sikubaliani na kauli ya kwamba Majimbo yaliyo na Wabunge wa Upinzani hayataletewa maendeleo na Serikali. Hiyo siyo sera ya Serikali. Sera ya Serikali ni kuleta maendeleo kwa wananchi wote nchini bila kuangalia wanawakilishwa na kiongozi kutoka chama kipi cha siasa.*(Makofi)*

(b) Ikithibitika kwamba wapo viongozi wanaozuia utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika maeneo wanayosimamia, Serikali itawachukulia hatua kali za kinidhamu viongozi hao na ikibidi kuwaondoa katika nafasi hizo.*(Makofi)*

(c) Dhana kuwa Serikali ya nchi yetu ina ubaguzi nadhani ni hisia tu za watu wachache. Wananchi hao wengi wana imani kubwa na Serikali yao na ndiyo maana wamekuwa wanashiriki kikamilifu kwa hali na mali katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo wanayoyahudumia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwakilisha.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu sahihi na mazuri yaliyotolewa na Waziri. Lakini wako viongozi wametamka matamshi hayo na tumewakamata mpaka kwenye *video* na je, Waziri yuko tayari kuwachukulia hatua hao viongozi waliofanya hivyo kama tukiwaletea majina hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea katika majibu sahihi na fasaha ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri, ameyasema. Msimamo wa Serikali ni huu uliosemwa hapa. Lakini kuna maeneo yamejitokeza baadhi ya vyama vinahamasisha wananchi wao wasishirikiane na Serikali katika kuleta maendeleo. Sasa katika misingi hii inakuwa taabu sana wale wanaohusika kushirikiana katika kuleta maendeleo inakuwa taabu kama wanashindwa kupata ushirikiano.

Kwa hiyo, katika maeneo hayo ambayo wanachama wa vyama hivyo wanakataa kushirikiana na Serikali kwa maagizo pengine ya viongozi wao hao inabidi kuchukuliwa hatua na pengine ndiyo sababu katika maeneo hayo ambayo wameshika wao maendeleo yanarudi nyuma kwa sababu ya hamasa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ikiwa pande zote mbili upo ushahidi yaani wale waliosema na hao ambao wamekataa maendeleo Serikali itakubali pande zote mbili kuchukuliwa hatua? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali hili kama ifuatavyo:-

Ushahidi ni kweli lakini lazima uwe ushahidi wa kutosha, siyo ushahidi wa barabarani tu, kwa kusema ushahidi ni ushahidi. Ushahidi unaotolewa uwe ushahidi wa kweli kweli. Haya niliyoyasema mimi ni ushahidi ambapo maeneo yale yanarudi nyuma kimaendeleo kwa hiyo, ushahidi huo upo. Sasa oh, viongozi wengine wamesema! Si kweli. Kwa hiyo, hakuna ushahidi na ushahidi uwe wa kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 12

**Ukarabati wa Barabara za Vijijini**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania inapongezwa sana kwa kasi yake ya kujiletea maendeleo kama vile kuunganisha barabara zote za Mikoa kwa lami na baadhi ya barabara hizo zikiwa zimechukuliwa na ushirikiano wa Afrika Mashariki na kwa kuwa ni dhahiri kuwa maendeleo hayatawafikia wananchi endapo barabara za vijijini hazitatengenezwa ili kuwawezesha wananchi kusafirisha mazao yao kwa urahisi kwenye masoko na kwa kuwa kuna barabara nyingi ambazo Halmashauri zetu za Wilaya

zinashindwa kuzihudumia kutokana na uwezo mdogo kifedha na hivyo Wilaya nyingi zimeomba barabara hizo zichukuliwe na Serikali Kuu:-

(a) Je, ni lini Serikali Kuu itaanza kuzifanyia matengenezo barabara za Iguguno hadi Singa na Ilunda kupitia Kiboriri, Lukomo, Kikonda na Kinampanda, barabara ya Iguguno kwenda msingi na barabara za Kiomboi Kidaru, Ibaga, Mkalama, Matongo hadi Kidarafa?

(b) Je, kama Serikali Kuu itasema haina fedha za kutengeneza barabara hizo kwa sasa, haioni kwamba umefika wakati wa kuziweka barabara hizo kwenye mpango kabambe wa utengezaji wa mawasiliano vijijini na *BADEA* pamoja na Serikali mbalimbali kuja kusaidia kufanya kazi hizo kwa manufaa ya wananchi wetu hasa ikizingatiwa kwamba wafadhili wengi wako tayari kuleta fedha zao kwetu kutokana na matumizi mazuri yanayofanywa na Serikali yetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara zote zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, isipokuwa kisehemu kidogo cha Iguguno - Kiboriri ambayo ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iguguno - Kiboriri - Lukomo - Kihonda - Kinampanda - Singa ina urefu wa kilometa 16 na kilometa 10 kati ya hizo ndizo zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Sehemu hii ya barabara ni kweli kwa muda mrefu haijfanyiwa matengenezo na iko katika hali mbaya. Aidha, iko barabara nyingine ya Iguguno - Lyelembo - Yulansoni - Msingi yenye urefu wa kilometa 32. Barabara hii imepita katika eneo lenye Mito mingi na mabonde hivyo inahitaji madaraja na makalvati mengi. Gharama ya kutengeneza barabara hii imekisiwa kufika shilingi milioni 963. Barabara ya tatu ni ile ya kutoka Kiomboi - Ibanga - Mkalama - Matongo - Kidarafu yenye urefu wa kilometa 108.8. Hii ni mojawapo ya barabara ambazo mwaka 2005 ziliombewa zichukuliwe na Mkoa kwa sababu matengenezo yake yanahitaji fedha nyingi kiasi cha shilingi bilioni 2.5. maamuzi bado kutolewa kwa Serikali na Serikali inaamini kuwa bado Halmashauri inaweza kufanya matengenezo katika barabara hizo hizo kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005 Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilipata kiasi cha shilingi 156.6 milioni kwa ajili ya matengenezo ya mtandao wa barabara zote za Halmashauri zenye urefu wa kilometa 753.5. Mahitaji ya kuhudumia barabara zetu ni makubwa lakini uwezo wetu wa kifedha ni mdogo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa mwaka 2005/2006 imetengewa jumla ya shilingi milioni

158.63, Hivyo zinashauriwa kupanga mipango yake ya matengenezo ya barabara kwa hela hizo zinazopatikana kiasi kidogo kwa kuzingatia vipaombele.

(b) Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika maendeleo kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mipango kabambe ya uendeshaji wa huduma kwa wananchi wake kama vile barabara, afya, elimu na kadhalika. Kwa upande wa barabara hivi sasa Ofisi yangu imechukua hatua zifuatazo ili kujua mahitaji halisi ya kuimarisha mtandao wa barabara za vijijini.

Mpango wa kwanza, imeanzisha mradi wa kutathmini hali na urefu wa barabara za Halmashauri *(Local Government Road Inventory and Conditional Survey)* nchi nzima. Mradi umeanza Septemba, 2005 na utakamilika Mei, 2006. Mradi huo kwa pamoja unagharamiwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania. Madhumuni ya mradi huo ni kufahamu urefu wa barabara za Halmashauri, hali yake, aina ya matengenezo yanayohitajika katika nchi nzima na timu ya wataalam wa kutathmini hali na urefu wa barabara watakuwa mkoani Singida kuanzia katikati ya mwezi Machi, 2006. Hivyo nategemea kuwa barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, zitatembelewa na kutathminiwa kwa ajili ya kuingizwa katika mpango kabambe wa matengenezo ya barabara za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imeanzisha mradi wa Kitaifa wa Usafiri Vijijini *(National Rural Transport Programme).* Mradi huu umepangwa kutekelezwa katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni matayarisho ambayo itachukua miaka miwili kuanzia Januari, 2006 mpaka Desemba, 2007.

Awamu hii ya matayarisho kwa pamoja inagharamiwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Norway. Madhumuni ya mradi ni kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini kwa kuzifanyia ukarabati, kujenga madaraja, kuweka lami rahisi, kutengeneza sehemu korofi ili kurahisisha usafirishaji vijijini. Kupitia mradi huu Halmashauri zitaimarishwa na kupewa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi wanaohusika na kazi hizo. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu marefu ya Waziri na amekiri dhahiri kwamba Halmashauri hazina uwezo wa kutengeneza barabara hizi muhimu na tukizingatia kwamba watu wa Iramba Mashariki wanashindwa kwenda Makao Makuu ya Wilaya kutokana na ukosefu wa barabara na inawabidi lazima wazunguke Singida ndiyo waende Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

(a) Je, katika hawa wafadhili wanaokuja hizi barabara zitapewa umuhimu wa kwanza?

(b) Kwa kuwa Waziri wa Miundombinu yuko hapa na najua yeye ni mtafutaji mzuri wa fedha za utengenezaji wa barabara na miundombinu mingine, je, atalichukulia hili swali kwa umuhimu wake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea majibu marefu na ya kina ya Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Lengo la Serikali kwa miaka mitano ijayo ni kuhakikisha kwamba kila Wilaya, kila Mkoa, unaunganishwa vizuri na barabara kuu za Kitaifa na za Kimataifa ambazo zimeainishwa katika mpango wetu wa barabara nchini. Kwa kweli hiyo ndiyo hasa ilikuwa sababu ya kuanzisha Wizara ya Miundombinu.

Kwa hiyo, Wizara yangu inaangalia upya barabara zote za Wilayani na Mkoani na vile vile inaangalia upya mpango kabambe ambao ulikuwa umeandaliwa wa kugharamia barabara hizi kupitia wafadhili Bajeti yetu na kwa njia nyingine za kibiashara. Tumaini langu ni kwamba muda si muda tutazungumza na wafadhili tutaelewa wao wana uwezo gani wa kusaidia mpango mkubwa wa barabara, tutaangalia vipaumbele upya.

Mheshimiwa Spika, tutaangalia ni barabara zipi mpya zinaweza zikawa za Mkoa na za *TANROADS* badala ya kuhudumiwa na Wilaya na kipaumbele kitawekwa kwenye Wilaya na Mikoa ile ambaye kwa muda mrefu imekuwa haina mawasiliano ya kuridhisha kwa njia ya barabara au reli au vinginevyo. Kwa hiyo, ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba wakinipa muda mambo haya nitayaweka sawa na tutaendelea kuzungumza na Mheshimiwa Mgana Msindai ili nielewe vizuri mambo yake na baadaye tunaweza tukafikia muafaka. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti niliofanya nimeona kwamba Serikali inaangalia zaidi barabara za tambarare.

Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza akatuambia wana mikakati gani ya kuangalia barabara za vijijini milimani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi yetu kwa kweli haina ubaguzi wa kuangalia kwamba hii ni barabara ya tambarare au hii ni barabara ya mlimani. Nafikiri kuna sehemu nyingine za milima katika nchi hii barabara zimefika huko. Kwa hiyo, sisi tunaangalia *areas* zote, hatutabagua na huo mradi utaingia vijijini kila sehemu, haitatenga milimani wala tambarare. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha kwamba hata huko milimani tutafika bila matatizo yoyote. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 13

**Mpango wa Kuigawa Wilaya ya Kilosa**

**MHE. AHMED M. SHABIBY** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kilosa ni kubwa kuliko Mkoa wa Kilimanjaro na kwa kuwa Wilaya hiyo ina wakazi wapatao 489,513 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 na kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kuigawa Wilaya hiyo:-

(a) Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kutotekeleza mpango huo hadi sasa?

(b) Kama mpango wa kuigawa Wilaya hiyo ili kufanya Wilaya mbili za Kilosa na Gairo, je, ni lini mpango huo utatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uundaji au ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 kwa Mamlaka za Miji na zote hizi ni sheria za mwaka 1982 pia zinatawaliwa na sheria na taratibu za uanzishaji wa Mikoa sheria Na. 12 ya mwaka 1994. Aidha, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Kilosa ni kubwa na ina wakazi wengi na kwamba inakidhi vigezo vya kugawanywa katika Wilaya mbili. Vigezo hivyo ni pamoja na:-

(i) Ukubwa wa eneo la kilometa za mraba zisizopungua 5,000;

(ii) Idadi ya kata zisizopungua 15;

(iii) Idadi ya Tarafa zisizopungua 5;

(iv) Idadi ya Vijiji visivyopungua 50;

(v) Idadi ya watu wasiopungua 100,000; na

(vi) Eneo lenye jiografia ambayo inazuia huduma kuwafikia wananchi kwa urahisi kama vile Milima, Mito, Misitu mikubwa, Visiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kutekeleza kwa uanzishwaji wa Wilaya mpya ya Gairo kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokamilika kwa taratibu za kuanzisha Wilaya hiyo. Taratibu hizo ni pamoja na Mheshimiwa Rais kuridhia pendekezo la kuanzishwa kwa Wilaya mpya na kutoa tangazo la Serikali gazetini.

Aidha, ukosefu wa raslimali, fedha, watu na miundombinu ni muhimu na ni sababu mojawapo ya ucheleweshwaji huo. Uanzishwaji wa Mkoa mpya au Wilaya unakadiriwa kuigharimu Serikali kiasi cha fedha takribani shilingi bilioni moja kwa

kuanzisha Wilaya na shilingi bilioni nne hadi sita kwa kuanzisha Mkoa. Hizi ni gharama kubwa kwa Serikali ikilinganishwa na uwezo uliopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu hapo juu Wilaya ya Kilosa imekidhi vigezo vyote muhimu vinavyohitajika. Kwa kuzingatia hili Wilaya hii itawekwa katika mpango wa kuigawa hapo Mheshimiwa Rais atakaporidhia na uwezo wa kifedha utakaporuhusu.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri Kilosa imekidhi sifa zote, je, Serikali iko tayari kuahidi hapa Bungeni katika awamu nyingine Kilosa itagawanywa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, kama ifuatavyo:-

Mwishoni mwa mwaka 2005 Waheshimiwa Wabunge, waliokuwepo watakumbuka kwamba Serikali ilitoa maelezo kuonyesha mwelekeo wa uanzishwaji wa maeneo yalivyo na Wilaya ya Kilosa kwa maana ya Wilaya mpya ya Gairo ilikuwa ni moja kati ya Wilaya 18 ambazo tulikuwa tumefikiria ziombwe ziweze kuanzishwa. Lakini kutokana na sababu mbalimbali za kiuchumi, ilishindikana na Mheshimiwa Rais akaanzisha Wilaya mpya saba. Kwa hiyo, bado tuna eneo hilo limebaki. Lakini kama alivyosema Naibu itategemea kwa kweli mambo ambayo ameyaainisha ikiwa ni pamoja na uwezo wa Serikali. Lakini mambo yakikamilika haya tuna hakika Wilaya chache zitaundwa.

Na 14

**Vituo vya Kazi kwa Wakuu wa Mikoa**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni utaratibu wa kawaida kwa Serikali kuwapangia Wakuu wa Mikoa vituo vyao vya kazi na kwa kuwa kiutaratibu Wakuu wa Mikoa wanapaswa kuishi katika Mikoa waliyopangiwa:-

(a) Je, kuna Wakuu wa Mikoa wangapi wanaoishi nje ya Mikoa waliyopangiwa?

(b) Kama wapo wanaoishi nje ya Mikoa waliyopangiwa, je, ni sababu zipi zinazowafanya Wakuu hao kuishi Mikoa ambayo siyo vituo vyao vya kazi na wanaishi kwa muda gani?

(c) Je, Serikali ipo tayari kumaliza kwa haraka sababu hizo zinazowasababisha Wakuu hao waishi nje ya vituo vyao vya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ni utaratibu wa kawaida wa Serikali kuwapangia Wakuu wa Mikoa vituo vyao vya kazi na Wakuu hao wanapaswa kuishi katika Mikoa waliyopangiwa.

Hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ni Mkuu wa Mkoa mmoja tu ambaye ni Mkuu wa Mkoa wake alikuwa anaishi nje ya kituo chake cha kwa sababu maalum. Huyu ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani ambaye amekuwa akiishi Mkoani wa Dar es Salaam tangu ahamie Mkoa wa Pwani tarehe 20 Februari, 2003.

(b) Sababu zilizomfanya Mkuu wa Mkoa wa Pwani kuishi mkoani Dar es Salaam ilikuwa ni kutoa nafasi ya kukamilisha nyumba ya Mkuu wa Mkoa ambao ukarabati huo ulikuwa unaendelea. Ukarabati wa nyumba hiyo umekuwa ukifanyika kwa awamu kulingana na kiasi cha fedha na kuendana na Bajeti za Mikoa. Awamu ya kwanza ya ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, ulihusisha uwekaji wa paa jipya na ujenzi wa mnara wa matanki ya maji. Kazi hizo ilikamilika tarehe 22 Aprili, 2003 kwa gharama za kiasi cha shilingi 24,766,646/=

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya matengenezo hayo yalihusu jengo la nyumba ya Mkuu wa Mkoa yenyewe, nyumba ya mtumishi, kibanda cha mlinzi na sehemu ya uzio ambapo gharama yake ilikisiwa kwamba ni shillingi 38,499.005/=

Mheshimiwa Spika, gharama za matengenezo haya ziliingizwa
Utawala ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitembelea nyumba hiyo tarehe 4 Juni, 2004 kwa madhumuni ya kujiridhisha na sababu za nyumba hiyo kuendelea kuombewa fedha za matengenezo kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Kamati iliridhika na matengenezo yaliyokuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kiasi cha shilingi 14,899,800/= zilitengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa uzio pamoja na *land scaping* na pia shilingi 2,400,000/= kwa ajili ya ununuzi wa samani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ukarabati wa nyumba umekwishakamilika na shughuli zinazoendelea ni ununuzi wa samani pamoja na *land scaping.* Shughuli hizi zinategemewa kukamilika hivi karibuni na kumwezesha Mkuu wa Mkoa Mteule kuhamia katika nyumba hiyo kwa mwaka huu wa fedha 2005/2006.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu swali hili.

(a) Je, Serikali kwa miaka mitatu Mkuu wa Mkoa kukaa nje ya Mkoa ni kitendo cha kumfanya Mkuu wa Mkoa asifanye kazi vizuri?

(b) Gharama za mafuta na gari alilokuwa anazunguka nalo kila siku kwenda na kurudi na watu kukosa kumwona wakati walipowajibika huoni Serikali haikumtendea haki?

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali juu ya suala hili naamini yako wazi, jambo hili halikucheleweshwa kwa makusudi hata kidogo na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama mjumbe wa *RCC* anajua kabisa kwamba jambo hili halikuwa siri, limekuwa likizungumzwa kwa maana kujaribu kutoa maelezo kwa nini Mkuu wa Mkoa hajaweza kuhamia katika ile nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile yeye ni mkazi wa Kibaha vile vile na amekuwa akiona juhudi hizo zinaendelea, kama kulikwama, anajua kwa nini kulikwama kwa hiyo, tunataka kumhakikishia tu kwamba hakuna aliyekuwa na nia mbaya hata kidogo na hayo mengine yote ya mafuta ni matokeo ya kutokuweza kumalizika kwa jumba hilo mapema. *(Makofi)*

Na. 15

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba; na kwa kuwa taswira ya majukumu ya Tume hiyo yameainishwa kwenye Ibara ya 130(1) (a -h), (2) mpaka (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa Ibara ya 103(2) imeeleza bayana kuwa Tume itakuwa na Idara inayojitegemea na haitalazimika kufuata maagizo au amri ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama cha siasa au taasisi nyingine yoyote ya umma au sekta binafsi:-

(a) Je, ni matukio mangapi yameripotiwa Serikalini wakati wa kampeni kuelekea Uchaguzi Mkuu kuanzia Septemba hadi Desemba 14?

(b) Je, ni matukio mangapi kati ya hayo yamewahusu Polisi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Usalama wa Taifa, Magereza na ni wahusika wangapi wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria na kuadhibiwa na ni kutoka maeneo gani ya nchi?

(c) Je, matukio mangapi kati ya hayo yanayowahusu raia nchini kote na ni watu wangapi wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria bila ukiukwaji wa taratibu za Tume husika?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salum, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) (b) (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba taswira ya majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yameanishwa kwenye Ibara ya 130(1) (a-h), 2 hadi 6 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ni kweli pia kwamba Tume ni Idara huru inayojitegemea kwa mujibu wa Ibara 130(2).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tume kuwa na mamlaka hayo, taarifa zilizopo kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Tume haikupokea lalamiko au tukio lililohusiana na Kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 14 Desemba, 2005 Tanzania nzima. Aidha, hakuna tukio ambalo limeripotiwa na Tume linalohusu Jeshi Polisi au Jeshi la Wananchi. Vile vile Tume haikupokea taarifa kuhusu raia ambao wamehusika katika matuko wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi na kwa mujibu wa sheria, masuala yanayohusu kampeni za uchaguzi hushughulikiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na iwapo kutatokea uvunjifu au kuvunjika kwa amani, vyombo vya dola huingilia kati na sheria huchukuwa mkondo wake.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, swali moja la nyongeza, kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haiwezi kufanya kazi Zanzibar na kwa kuwa suala la usalama wa raia na mali zao na suala la haki za binadamu sio jambo la Muungano.

Je, Serikali itakubali kuunda Tume kuchunguza matokeo ambayo kama Tume hii ingekuwa ina haki ya kufanya kazi Zanzibar ingeweza kuwasilisha, lakini kwa sababu haiwezi kufanya Zanzibar haiwezi kusawazisha?

Je, Serikali iko tayari kuunda Tume kwenda kuchunguza matukio yaliyotokea Zanzibar ya uvunjaji wa haki za binadamu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, baada ya Mheshimiwa Naibu Waziri kujibu swali hili vizuri sana kwamba Ofisi ya Tume vile vile iko Zanzibar na napenda kurudia kwamba Tume ya Uchaguzi ndiyo ina mamlaka ya mambo ambayo yanahusu uchaguzi lakini kama kutakuwa na uvunjifu wa haki za binadamu, Ofisi iko vilevile Zanzibar.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Serikali itachukua hatua gani dhidi wa askari wa KMKM ambaye alimuua kijana, alimpiga risasi na kumuua kinyama kijana Saleh Seif Haji, akiwa nyumbani kwao siku ya terehe 1Novemba, 2005.

**WABUNGE FULANI:** Ni swali jipya.

**SPIKA:** Waheshimiwa naona ningependekeza kwamba kwa sababu hili linaleta hoja mpya ambayo haimo katika maudhui ya swali la awali, namshauri kwa sababu tuna nafasi ya maswali katika Mkutano huu basi atupatie swali likiwa pekee kwa maandishi litapokelewa. Ahsante.

Na. 16

**Sheria ya Makampuni Na. 12 ya Mwaka 2002**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa dhamira ya Tanzania kwa miaka mitano iliyopita na miaka mitano ijayo ni kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea; na kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua kadhaa kufanikisha azma hiyo ikiwa ni pamoja na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria mpya ya Makampuni ambao ulipitishwa na Bunge na sasa ni Sheria Na. 12 ya mwaka 2002

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazozuia kutumika kwa sheria hiyo mpya na kuruhusu tuendelee kutumia Sheria ya Makampuni iliyopitwa na wakati ambayo ilitarajiwa na Baraza la kutunga Sheria la Kikoloni *(LEGCO)* mwaka 1932;

(b) Je, ni kwa kiwango gani kuendelea kutumia Sheria hiyo iliyonakiliwa kutoka kwenye Sheria ya Uingereza ya Makampuni ya mwaka 1929 ambayo Waingereza wenyewe walishaifuta miaka mingi iliyopita, sheria ambayo inasaidia na kukwamisha juhudi za Tanzania kujenga msingi wa uchumi wa kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, napenda nitoe ufafanuzi mfupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza dhamira ya Tanzania ya kujenga msingi wa uchumi imara na wenye mwelekeo wa kujenga Taifa linalojitegemea imejikita katika mikakati kadhaa chini ya dhana ya maboresho ya kisekta yanayoendelea hivi sasa hapa nchini. Katika sekta ya sheria, maboresho yanalenga pamoja na mambo mengine katika kuzirekebisha au kuzifuta kabisa na kutunga sheria mpya mbadala zinazokwenda na wakati na zinazokidhi mahitaji ya jamii ya sasa ya Kitanzania. Katika miaka mitano iliyopita hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2005, sheria kadhaa zilishughulikiwa ambapo baadhi zilifanyiwa marekebisho na zingine zilifutwa na kuandikwa sheria zingine mpya. Moja ya sheria hizo ni Sheria ya Makampuni yaani *The Companies Ordinance (Cap. 212)* ambayo sasa imefutwa na kuandikwa upya na Sheria Na. 12 ya mwaka 2002 *(The Companies Act, (No. 12 of 2002).*

Mheshimiwa Spika, pili, kazi ya maandalizi ya Sheria Mpya ya makampuni imechukua muda mrefu. Katika muda huo ulifanyika mchakato wa mashauriano na wadau mbalimbali wa biashara, wataalamu na watumiaji wa Sheria, ili hatimaye kuiwezesha Sheria hii kuzingatia mahitaji halisi ya kibiashara ya Makampuni, ambayo ni kulinda haki za wenye hisa wakubwa na wadogo na wadai wa Makampuni, kuanisha wajibu wa Wakurugenzi na Watendaji wa Makampuni na vile vile kulinda maslahi ya umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tatu, Sheria ya Makampuni haiwezi kutekelezeka bila kuwa na Kanuni zake. Maandalizi ya Kanuni hii yalipaswa kufanywa kabla ya sheria kuanza kufanya kazi. Kazi ya kuandaa kanuni hizo sasa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, nne, kwa kuwa Sheria hii imeleta mabadiliko makubwa katika shughuli za Makampuni, ilikuwa ni lazima kuwajengea uwezo watendaji watakaokuwa wanaisimamia Sheria hii ili waweze kuisismamia vizuri na kwa ufanisi zaidi. Hivi sasa zoezi la kuwaandaa watendaji linahitimishwa na mafunzo yao yalianza toka mwezi Januari 2006, chini ya uhifadhili wa Mradi wa *Business Environment Strengthening for Tanzania* yaani *BEST,* ulioko chini ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kulijibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Sheria ya Makampuni ya zamani sasa imepitwa na wakati na Sheria mpya imechukua muda mrefu kuanza kufanya kazi. Baada ya kukamilisha maandalizi ya Kanuni na kuzichapisha, sasa Sheria Mpya ya makampuni Na. 12 ya 2002 itaanza kutumika tarehe 1 Machi, 2006.

(b) Ingawa hakuna utafiti uliofanyika kubaini hasara iliyopatikana kutokana na kuendelea kutumika kwa Sheria ya makampuni ya zamani. Hata hivyo Serikali inajua kwamba Sheria hiyo ilikuwa na mapungufu ambayo yameondolewa na Sheria mpya.

Na. 17

**Njia za Kupunguza Deni la Taifa**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa katika juhudi za Serikali za kupunguza deni la Taifa imekuwa ikibuni njia mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo:-

(a) Je, ni njia gani hizo zilizotumika kupunguza deni hilo?

(b) Je, deni hilo la Taifa katika kipindi cha miaka kumi limeongezeka au kupungua kwa kiasi gani?

(c) Je, ni makampuni mangapi ya Tanzania yalifaidika na ununuaji wa madeni na ni ya nchi gani kati ya hayo ni magapi yamelipwa na yamewezeshwa kwenye miradi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a) (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo kupunguza deni la Taifa:-

(i) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa Taifa wa kusimamia deni la Taifa wa mwaka 1999;

(ii) Kurekebisha na kusimamia kwa makini utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 pamoja na kanuni zake;

(iii) Kuzishawishi nchi zinazotudai pamoja na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kutoa unafuu wa madeni;

(iv) Kubadili baadhi ya madeni yake ya nje kuwa mitaji kwa ajili ya uwekezaji hapa chini ya mpango wa *Debt Coversion* uliofanyika hadi mwaka 1993/1994, *Debt Buy Back Scheme (CBBS)* uliotekelezwa kati ya mwaka 1994 na 2004 pamoja na mpango wa *Debt Swap* unaoendelea kutekelezwa hivi sasa.

(v) Kuwashawishi wafadhili kuchangia mfuko wa kulipia madeni-*Multilateral Debt Fund (MDF)* uliotumika kati ya miaka ya 1999 na 2001

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha hadi Desemba, 2005 deni la nje lilifikia Dola za Marekani bilioni 7.93 likiwa limeongezeka kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 7.54 katika kipindi kinachoishia Desemba, 1995. Ongezeko hili ni ambalo ni dogo sana linatokana na mafanikio ya kufutiwa madeni na udhibiti wetu wa ukopaji. Deni letu kwa sasa linahimarika *(sustainable)* tofauti na ilivyokuwa mwaka 1995.

(c) Mheshimiwa Spika, makampuni 7 ya Tanzania yalifaidika na ununuaji wa madeni na hadi mwishoni mwa mwaka 2005, nchi za Ubelgiji, Urusi, Bulgaria, Czechoslovakia, China, Libya na Hungary ziliuza sehemu ya madeni yake kwa utaratibu huo. Miradi iliyonufaika ni katika sekta za kilimo, viwanda, utalii na makazi ambapo fedha za miradi husika zimelipwa taslimu au kwa hatifungani *(Treasury Bonds)* kwa kuzingatia mkakati wa kusimamia deni la Taifa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, katika swali langu la tatu, nilitaka kufuta hayo majina ya makampuni ambayo yamepewa fursa hii badala yake Serikali imetaja kwa jumla kama kilimo na kadhalika na mimi nilitaka *specific* yatajwe makampuni ambayo yamo katika swali.

(a) Je, Waziri atakubali kuniletea majina ya kampuni ili kama ni swali lingine la kuongeza niongeze?

(b) Kwa kuwa pamoja na kufutiwa deni bado Serikali inaelekea inaendelea kukopa na deni letu bado liko juu kwa asilimia tano kama alivyosema Waziri, je, huku kufutiwa kuna msaada gani kama bado deni ni kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kampuni zilizofaidika na mpango huu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ubelgiji, kampuni zilizonufaika ni *GS Motors* katika mradi wa kilimo, *Afri Tena Tanzania Limited* katika mradi wa kilimo na *Mahafudhi and Family* katika ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, Urusi, kampuni iliyonufaika ni *Kobelimo* ya Ubelgiji ambayo kwa kushirikiana na *NBC* ya hapa nchini imewekeza katika miradi ya viwanda na madini, Burgalia, kampuni iliyonufaika ni *Debt Advisory International* ya Marekani ambayo kupitia *Gombay State* hapa nchini imewekeza katika mradi wa kilimo cha mboga mboga, Hungary, kampuni iliyonufaika ni *Debt Advisory International* ya Marekani ambayo kupitia *Gombay State* tena ya hapa nchi imewekeza katika miradi ya kilimo cha mboga mboga, Czechoslovakia, kampuni iliyonufaika ni *Techno Farm Limited* katika mradi wa kilimo, China imetumia baadhi ya madeni yake kuendeleza miradi waliyofadhili hapa nchini kama Urafiki, *UFI* na mengineyo na Libya inaandaa taratibu za kuwekeza hapa nchini kwa kutumia sehemu ya deni lake hasa katika sekta ya kilimo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la pili lilikuwa je, tunaendelea kukopa. Labda niseme kwamba hii asilimia tano *point* aliyoitaja ni katika miaka kumi ni sawa kati ya mwaka 1995 mpaka 2005 na hivi sasa kama tulivyosema kwamba tuko *credit worthy* yaani tunaweza kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kweli kukopa sio jambo baya, ukope kwa ajili ya maendeleo na ukopaji wetu utakuwa kwa kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), kwa hiyo, hilo sio jambo, isipokuwa tu tujue ni jinsi gani tunakopa na jinsi tutakavyotumia fedha hizi kwa ajili ya kuondoa umaskini.

Na. 18

**Kushuka kwa Thamani ya Sarafu ya Tanzania.**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya sababu ya kushuka kwa thamani ya sarafu yetu ya Tanzania ni kupungua kwa uuzaji wa mazao yetu ya biashara nje ya nchi, mbali na sababu hiyo, pia

nchi yetu sasa ina migodi ya dhahabu na almasi ambayo ingesaidia kupanda kwa thamani ya sarafu yetu:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu falsafa hiyo ya kushuka kwa sarafu hiyo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za uhakika za kuzuia hali hiyo?

(c) Je, Serikali inawaambia nini wananchi inaposema uchumi wetu unakua na wakati huo huo thamani ya shilingi yetu inazidi kushuka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zinazosababisha thamani ya shilingi kupungua, mojawapo ikiwa ile iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge yaani kutokuongezeka haraka vya kutosha mauzo yetu nchi za nje. Thamani ya ununuzi wetu kutoka nchi za nje ni kubwa zaidi na inaongezeka kwa kasi kuliko thamani ya mauzo yetu nchi za nje. Hivyo, kuna nakisi au pengo kubwa katika urari wa malipo. Pengo hili hufanya thamani ya shilingi kushuka. Kwa mfano, katika mwaka 2004, mauzo yetu ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa ni dola za Kimarekani milioni 2,220.7, wakati ununuzi wetu wa bidhaa na huduma toka nje ulikuwa ni dola za Kimarekani milioni 3,283.2. Kwa hivyo, kulikuwa na pengo la dola milioni 1,062.5, ambalo ni sawa na asilimia 47.8

Mheshimiwa Spika, pengo hili lilijazwa kutokana na misaada ya wafadhili. Kwa hiyo, kukiwa na ucheleweshaji au upungufu wa fedha kutoka kwa wafadhili kujaza pengo hili, thamani ya shilingi hushuka.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya kushuka kwa thamani ya shilingi ambayo imetokea katika miezi ya hivi karibuni, ni nguvu ya dola ya Kimarekani ambayo imesababisha kushuka kwa thamani ya fedha ya nchi kubwa nyingi kama vile Japan, Uingereza na nchi za Ulaya. Hivyo katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2005 thamani ya Yen ya Japan na thamani ya *Euro* ya nchi za Ulaya na Paundi ya Uingereza zimeporomoka zaidi kuliko hata shilingi ya Tanzania. Kwa sababu nchi hizi ndizo zilizo muhimu katika biashara ya Tanzania na nchi za nje, shilingi nayo imelazimika thamani yake ishuke kwa kiasi kikubwa kutokana na nguvu ya dola ya Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia kuzingatia kuwa kupungua kwa thamani ya fedha siyo kila wakati ni jambo baya. Kwani kushuka kwa thamani kunasaidia kuongezeka kipato kwa thamani ya fedha yetu, wauzaji mazao na huduma nje ya nchi na hivyo kusaidia kukuza uchumi wetu haraka zaidi, ingawa kwa wakati huo huo huongezeka gharama za ununuzi wetu nchi za nje.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuzuia kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania Serikali imechukua hatua zifuatazo kuongeza mauzo nje ya nchi:-

(i) Kuanzisha kwa *Export Processing Zones;*

(ii) Kuwa na Mfuko wa Udhamini wa Biashara nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme);* na

(iii) Kuanzisha Mifuko ya Mikopo inayolenga katika kukuza uzalishaji na hivyo kuhamasisha mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Benki Kuu huingilia soko la fedha za nje kila inapobidi.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli uchumi wetu unakua, lakini kigezo cha ukuaji wa uchumi siyo kuongezeka kwa thamani ya shilingi. Vigezo vya hali ya uchumi ni kasi ya ukuaji wa uchumi kwa jumla yaani *GDP, growth rate,* mfumuko wa bei *(the inflation rate),* nakisi katika Bajeti ya Serikali na akiba ya nchi ya fedha za kigeni, pamoja na hali ya urari wa malipo ya biashara ya nje kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kupunguza umaskini na kuleta hali nzuri katika maisha ya Mtanzania hutokana na kasi ya kukuza uchumi. Hivi sasa uchumi wetu unakua kwa asilimia 7. Kupunguza umaskini mpaka Mtanzania ajione kuwa hali yake inabadilika haraka inatakiwa uchumi wetu ukue kwa asilimia 8 mpaka 10 na tutaweza kufikia lengo hilo ikiwa kwa upande mmoja thamani ya shilingi inaambatana na kusaidia kuongeza mauzo yetu nchi za nje.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hali tuliyokuwa nayo sasa ya njaa na suala la *inflation* imekuwa ni tatizo na hasa kwa kushuka sarafu yetu ya Tanzania, Serikali imeweka utaratibu wa kuagiza chakula kutoka nje na hatimaye kuwauzia wananchi wetu. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba hivi sasa Benki Kuu ya Tanzania yaani *BOT* inawajibu wa kuhakikisha inadhibiti sarafu ya Tanzania isishuke zaidi ili kuweza kuwapa nafasi wananchi wasinunue chakula hiki kwa bei ya juu zaidi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Naibu Waziri ni kwamba mara nyingine Benki Kuu inabidi kuingilia kati kitu ambacho kinaitwa mara nyingine *moping* ambapo inaondoa fedha zaidi, ili kwa kweli suala la *inflation* lisizidi. Kwa hivyo, Benki Kuu hivi sasa iko makini na inaangalia kwamba hali ya uchumi isiweze kushuka.

Na. 19

**Gharama za Kupeleka Maji Kata za Itezi na Nsagala**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kata za Itezi na Nsalaga waliamua kuchanga fedha na kufanikiwa kuvuta maji toka chanzo cha maji cha Mwatezi.

(a) Je, Mamlaka ya majisafi na majitaka ipo tayari kurejesha gharama walizotumia wananchi hao ambao ndio wanaomiliki chanzo hicho cha maji?

(b) Kwa kuwa kuna malalamiko na manung'uniko toka kwa wananchi wa Kata hizo juu ya mkataba walioweka viongozi wao, je, Serikali itakuwa tayari kukaa nao ili kumaliza tofauti zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli katika Kata za Itezi na Nsagala zilizopo katika Bonde la Uyole utoaji huduma ya maji ulikuwa kwa mfumo wa uchangiaji. Uendelezaji wa vyanzo vya Itezi na Nsagala katika bonde hilo uligharamiwa na wananchi pamoja na msaada wa Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo *DANIDA* wa shilingi milioni 152.41.

Mradi ulipokamilika walikabidhiwa watumiaji wa maji ili wauendeshe. Kwa vile eneo lote la Bonde la Uyole liko ndani ya jiji, jukumu la kutoa huduma za majisafi na majitaka ni jukumu la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka, Mbeya. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya maji Na. 8 ya mwaka 1997. Makabidhiano ya mali kati ya jumuiya ya watumiaji maji wa Bonde la Uyole na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka yalifanyika tarehe 20 Julai, 2004 baada ya kuonekana kuwa huduma inayopatikana haitoshelezi. Japokuwa mkataba wa makabidhiano ya mali haukuhusisha fidia yoyote, Mamlaka ililipa deni kwa kampuni ya *Idege Hardware* la shilingi 2. 917 milioni kwa ajili ya bomba na vifaa vya ujenzi vilivyotumiwa na jumuiya ya watumiaji maji kwa ajili ya uendeshaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mamlaka ndiyo inayotoa huduma ya maji kwa wateja 2,825 katika maeneo hayo. Ili kuendeleza huduma ya maji katika eneo hili Mamlaka imekwisha wekeza shilingi milioni 130. Fedha hizi zimetumika katika kuendeleza chanzo cha maji Mwatezi, kujenga chanzo cha Nsagala na kulaza mabomba ya kusambaza maji.

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ya maji inaipa uwezo Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Jijini Mbeya kumiliki, kusimamia, kuvitunza na kuviendeleza vyanzo vya maji vilivyopo katika eneo la Jiji la Mbeya kwa manufaa ya wakazi wote wa Jiji. Mamlaka inaongozwa na Bodi yenye wawakilishi wa aina mbali mbali ya watumiaji maji. Hivyo,

endapo bado kuna malalamiko Bodi ya Wakurugenzi na uongozi wa Mkoa wa Mbeya wanaweza kuyasuluhisha bila kuathiri huduma inayotolewa. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nishukuru kwa majibu mazuri na ya kina yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ilikuwepa migongano, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuzitembelea Kata hizi za Nsalaga na Itezi pamoja na Itagano, ili akajiridhishe mwenyewe hali halisi ya usambazaji wa maji katika eneo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu na mimi mwenyewe niko tayari kwenda kutembelea na kubadilishana mawazo ili kwa maendeleo ya maji ya Jiji la Mbeya.

Na. 20

**Kuundwa kwa Bodi ya Mtaro wa Ntomoko**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilielekeza umuhimu wa kuunda Bodi ya kushughulikia Mtaro wa Ntomoko, na kwa kuwa Wilaya ya Kondoa imekwishatuma mapendekezo hayo Wizara ya Maji kwa hatua zake:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kukamilisha uundwaji wa Bodi iliyopendekezwa?

(b) Kwa kuwa hatua inayofuata ya baada ya kuundwa kwa Bodi hiyo ni ukarabati wa Mtaro huo, je, hatua hiyo itaanza lini?

(c) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakiri kupokea maombi ya uundaji wa chombo huru cha kisheria cha watumiaji maji eneo la Mtaro wa Ntomoko. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa maombi yaliyotumwa Wizarani yalikuwa ya usajili wa Jumuiya ya Watumiaji Maji kwa eneo la Mtaro wa Ntomoko.

Taratibu za usajili wa Jumuiya hiyo zilikamilika tarehe 30 Mei, 2005 baada ya kupata idhini ya Wizara ya Maji na kufuatiwa na kutangazwa kwake kwenye Gazeti la Serikali Na.167 la tarehe 17 Juni, 2005. Cheti cha kuidhinisha Jumuiya ya watumiaji maji

kilitolewa tarehe 15 Julai, 2005 na wahusika walipewa cheti hicho. Kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kumeipa Jumuiya uwezo wa kisheria wa kuendesha mambo yao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Maji tarehe 01 Februari, 2006 katika Mradi wa Ntomoko, aliagiza uongozi wa Wilaya ukabidhi mradi huu kwenye Jumuiya ya Watumiaji Maji ili wananchi waweze kushiriki vizuri katika usimamizi wa mradi huu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Ntomoko umekuwa ukitengewa fedha za ukarabati na Wizara yangu hata kabla ya kuundwa kwa Jumuiya. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya shilingi 20,000,000/= zilitengwa na kutumika. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya shilingi 30,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya ukarabati. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kipengele (b) hapo juu, shilingi 20,000,000/= zilitengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005 ambazo zilitumika kukarabati chanzo cha maji *(intake)* na vituo 42 vya kuchotea maji katika vijiji vya Makirinya, Kinkima, Kirere cha Ng’ombe, Mtakuja, Hamai, Churuku, Goima, Jenjeluse na Songolo. Fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2005/2006 zitatumika katika ukarabati wa vituo vya maji katika viijiji vya Jinjo, Jangalo, Mapango, Chandama, Mlongia na Itolwa.

Aidha, Wizara yangu inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kuingiza mradi huu kwenye Programu ya Taifa ya Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira itakayoanza Julai, 2006. Programu hii itaweza kushughulikia ukarabati wa mradi huu na pia itawezesha kufanyika kwa upembuzi yakinifu ambapo lengo ni kutafuta vyanzo vya kuongeza maji katika mtaro huu. Uchunguzi utafanywa pia kuona uwezekano wa kutumika Bwawa la Mwisanga ili liweze kutumika kuhudumia vijiji vinavyohusika na mradi huu.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri wa Maji kwa majibu yake mazuri, naomba niulize maswali mawili.

(a) Mheshimiwa Spika, katika majibu yake ya msingi alisema kwamba Wizara ilitenga shilingi milioni 20 katika Bajeti ya mwaka 2004/2005, napenda nimhakikishie kwamba mpaka sasa tumepokea shilingi milioni 10 tu. Je, Wizara iko tayari kuleta milioni 10 zilizobaki ili ziweze kusaidia kukarabati mtaro huo?

(b) Katika jibu lake la msingi amekiri kwamba katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 Wizara imetenga shilingi milioni 30 lakini hizo pesa bado hazijapokelewa.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kwanza amekwenda kutembelea mradi huo na ameshuhudia kwamba chanzo pekee cha maji katika eneo la vijiji 19 ni mtaro huu, je, atachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hiyo shilingi milioni 30 inatolewa mapema ili ukarabati ufanyike kwa sababu hivi sasa hatuna vyanzo vingine vya maji katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Paschal Degera, yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakiri mimi nimetembelea mradi huu na nilikutana na Halmashauri ya Kijiji pamoja na Bodi ya Maji ya Ntomoko. Katika kikao hicho wote kwa pamoja walikiri kupokea milioni 20 na walielezea kazi zilizofanyika na baada ya hapo napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu na yeye ni Mbunge na pia ni Diwani na yeye naomba akatusaidie zaidi kuangalia hiyo hali na kwa kuwa kule walikiri kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, swali lake la (b) alikuwa anauliza kuhusu milioni 30, ni kweli milioni 30 hazijapelekwa lakini ziko katika Bajeti sasa hivi ambapo kwa kufuatana na mkutano tuliofanya kule ni kwamba zitatolewa wakati wowote katika kipindi hiki cha sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Bodi imepewa uwezo wa kuendesha mambo yake, nina uhakika kwamba Bodi itasimamia milioni 30 na pia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu na yeye pia ni Diwani katika Halmashauri ya Kondoa namwomba tusaidiane wote kusimamia milioni 30 zitumikaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya maji ni kweli chanzo kiko kimoja na pia pesa hizi zitafanya kazi hiyo lakini pia ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Bwawa la Mwisanga ambalo wakishaingiza mradi huu katika programu ya majisafi na usafi wa mazingira na lenyewe litapatiwa fedha ili liwe chanzo kingine cha kusaidia mtaro wa Ntomoko. *(Makofi)*

Na. 21

**Mikopo kwa Akina Mama**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wengi wa Kisiwa cha Pemba ni wafanyabiashara wazuri na hufanya biashara zao kwa kutegemea mikopo; na kwa kuwa kuna mikopo inayotolewa na benki tofauti na ile ya *PRIDE Tanzania* lakini ina masharti magumu na riba kubwa jambo ambalo linawarudisha nyuma akina mama hao kimaendeleo.

(a) Je, Serikali inawasaidiaje kina mama hao ili kujikwamua na hali ngumu ya maisha?

(b) Je, isingekuwa vema suala la ukubwa wa riba nalo likaangaliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kwa kuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya wanawake. Pia ninawapongeza akina mama wa Kisiwa cha Pemba kwa kuwa wafanyabiashara na wajasiriamali wazuri. Hii inaonyesha ni jinsi gani wanathubutu kuomba mikopo na kujiingiza katika biashara, kujiletea maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kuwa mikopo inayotolewa na Mabenki na Taasisi mbalimbali za fedha zina masharti magumu. Mfano kuhitajika kuwa na dhamana ya mali zisizohamishika kama hati ya nyumba, gari na ardhi, kuwa na biashara zilizo rasmi na akaunti ambayo huwafanya wanawake wa kipato cha chini washindwe kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya Benki na Taasisi zisizo za Kiserikali hutoza riba kubwa kwa viwango tofauti kulingana na gharama za uendeshaji kwa mfano Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)* 21%, Benki ya Maendeleo Vijijini *(CRDB)* 21%, Benki ya Posta 19.2%, *National Micro Finance Bank (NMB)* 24% na Taasisi kama *Credit Scheme for Productive of Women in Tanzania (CREW-T)* 22%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi napenda kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake Tanzania Bara na Mfuko wa Kujitegemea Zanzibar ambayo ina masharti nafuu. Mfuko wa Kujitegea uliopo Zanzibar ambao pia una ofisi zake Pemba umeweza kukopesha mwanamke mmoja, mmoja na katika vikundi. Mfano kikundi cha *Jambonia Cooperative Society* kilichopo Wawi kimepata mkopo na kinajishughulisha na shughuli za ushonaji ili kujikwamua na hali ngumu ya maisha. Mifuko hii ni mifuko pekee ambayo inawafikia wanawake katika ngazi zote za chini, nchi nzima waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kuhimiza na kusaidia wanawake wengi kuunda Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na *(SACAS)* ambavyo vinatoa riba nafuu na kumwezesha mwanamke kujenga tabia ya kujiwekea akiba. Mfano Rombo, Kilimanjaro riba ni asilimia 10 - 13 kutegemea na makubaliano ya wanachama wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada za kuhamasisha na kuwaelimisha Maafisa Maendeleo ya Jamii juu ya mbinu za kuwahamasisha wanawake ili kuweza kujiunga na *SACCOS* na *SACAS* na kuanzisha vikundi vya kuwawezesha kukopa kwa kujidhamini wenyewe.

Aidha, jitihada zingine zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine katika kuhakikisha kwamba akina mama wanaondokana na hali ngumu za kiuchumi, ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya ujasirimali ili kuwawezesha akina mama hao kubuni biashara, kupanga na kuendesha biashara zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo ni muhimu, kwani yanawaongezea uwezo ambao wengi wao umewawezesha kupata mikopo kwenye Benki na Taasisi mbalimbali za fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuwaondolea wanawake baadhi ya vikwazo vya kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za fedha, Serikali imeweka Sheria ya Ardhi ambayo inawawezesha wanawake kumiliki raslimali ya ardhi. Sheria hiyo kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 inawezesha ardhi kutumika kama dhamana ya kupata mikopo. Vile vile Serikali imeanzisha mpango wa kurasimisha mali (MKURABITA), mpango ambao utawezesha wanawake kutumia biashara ndogo ndogo wanazofanya kama dhamana ya kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Tunatarajia kuwa Benki hii itakapoanzishwa wanawake wanachama wa Vyama vya Ushirika na vya kuweka na kukopa wataweza kufaidika na mikopo kupitia Benki hii.

(b) Mheshimiwa Spika, hata hivyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa ukubwa wa riba ni jambo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa makini. Sera ya *National Micro Finance* ya mwaka 2000 imeelekeza kuwa Taasisi za kifedha ndizo zitakazojipangia riba za mikopo wanayotoa.

Aidha, suala la riba kibiashara ni suala ambalo hutawaliwa na vigezo mbalimbali vikiwemo vya mfumuko wa bei, gharama za usimamizi na uendeshaji na kutokana na hali hiyo suala la ukubwa wa riba ni changamoto. Kulingana na vigezo hivyo inakuwa vigumu kwa Serikali kudhibiti viwango vya riba hasa katika mabenki ya biashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inaangalia suala hili la riba kama changamoto kwetu. Hivyo basi kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Ibara ya 120, ninanukuu, "Tutaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuziwezesha benki na asasi nyingine zinazotoa huduma ya mikopo kutoa mikopo kwa masharti nafuu kwa wanawake miongoni mwa wananchi wote," mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa changamoto kwa wanawake wajiunge na kuanzisha vikundi au vyama vyao vya kuweka na kukopa ili waweze kusimamia na kupanga riba iliyo nafuu kulingana na mazingira yao.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasirimali ili wanawake wengi zaidi wajue umuhimu wa kukopa, umuhimu wa kurejesha mikopo na umuhimu kuanzisha biashara ambazo zitawapatia faida na hatimaye kujiwekea akiba kwa maendeleo yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, akisimama Spika huwezi tena na wewe kuendelea kusimama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jibu hili limekuwa ni refu sana na naendelea tu kuwa na huruma kwa sababu kwa mfano Mheshimiwa aliyejibu sasa hivi ndio mara yake ya kwanza. Lakini nadhani tuseme tu wiki hii itakuwa ni ya mwisho, kuanzia wiki ijayo sitakubali majibu marefu ambayo yanazunguka sana. *(Makofi)*

Taarifa tu ya ziada ni kwamba saa 4.30 itanibidi nitoke kwenda kwenye shughuli nyingine na Naibu Spika atachukua kiti, huwa nafurahia sana akija hapa kwa sababu ndio namna ya kugawana madaraka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kuna swali la nyongeza.

**SPIKA:** Kuna nyongeza? Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, samahani swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu ambayo nakiri ni ya kufahamika zaidi.

Naomba kumuuliza kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba tatizo hili la benki kwa wanawake lipo na vile vile amesema kwamba kutaanzishwa Benki ya Wanawake hapa Tanzania ili kuwapatia mikopo nafuu wanawake. Je, Benki hiyo itaanza lini ili kuwakomboa wanawake hao wa Tanzania, maana yake kila siku itakuwa kesho, kesho, lini itaanza benki hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba kwa kuwa kuna baadhi ya taasisi za mikopo kuwadhalilisha sana wanawake pale wanapochelewa au wanaposhindwa kulipa mikopo yao kwa sababu tofauti na kufikia hadi kuwatolewa vifaa vyao ndani ya nyumba na kuvipiga mnada na kuviuza, huko ni kuwadhalilisha wanawake.

Je, Serikali haioni kwamba tatizo hilo linadhalilisha wanawake na siyo kuwaendeleza? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ni lini Benki yetu ya Akina mama itakapoazna rasmi, napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zinafanyika sasa hivi tayari tuna *load map* na tunao tayari mchakato mzima wa utekelezaji. Tuko katika hatua ya kumpata *consultant* na matarajio yetu benki hii itaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu unaotumika na baadhi ya asasi mbalimbali zinazotoa mkopo wa kutoa vyombo vya watu si mzuri. Lakini pia tuweze tukakumbuka kwamba mkopo ni mkopo siyo msaada, siyo hisani kwa hivyo tushirikiane sisi wote viongozi wa dini, taasisi

mbalimbali tukajenga tamaduni za kuweza kuhakikisha kwamba watu wanafahamu mkopo ni lazima urejeshwe. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 22

**Uvamizi wa Viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa vyombo vya habari vimekuwa vikiandika taarifa ya uvamizi na ujenzi kwenye viwanja vya Marehemu Mwalimu J.K Nyerere kwa jeuri:-

Je, Serikali inasema nini juu ya taarifa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo Wizarani kwangu kiwanja kilichopo eneo la *Msasani Beach* karibu na nyumba ya Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu J.K Nyerere kimetengwa kwa ajili ya burudani na michezo.

Kwa hiyo, kiwanja hicho hakijamilikishwa kwa mtu au taasisi yoyote. Katika vipindi tofauti, Serikali iliwahi kupokea maombi kutoka kwa wananchi mbalimbali wakitaka wamilikishwe eneo hilo bila ya mafanikio. Wananchi hao walishauriwa kuomba maeneo mengine na walioafiki waliomba na kumilikishwa kwenye maeneo mengine.

Miongoni mwa waombaji ni mwananchi mmoja aliyetaka kumilikishwa mwaka 1998. Pamoja na kushauriwa kuwa aombe eneo lingine, hakufanya hivyo na mwaka 1999 aliweka makontena katika eneo hilo kwa lengo la kuendesha shughuli za biashara ya kutengeneza matofali kinyume cha sheria. Iliyokuwa Tume ya Jiji ililishughulikia suala hili kwa kufungua kesi mahakamani. Hivyo, mwakanchi huyo na ambaye hadi sasa anafanyia biashara zake katika eneo hilo hajawahi kumilikishwa, bali ni mvamizi.

Pia, hakuna kesi yoyote ambayo hukumu yake ilimtangaza kuwa ni mmiliki wa eneo hilo, kwa kuwa kesi aliyowahi kushtakiwa na iliyokuwa Tume ya Jiji mwaka 1999 na kuachiwa huru mwaka 2004, haikuwa na uhusiano wowote na miliki, bali ilihusiana na yeye kuweka makontena katika eneo hilo na kuendesha biashara bila ya kibali kutoka Tume ya Jiji. Manispaa ya Kinondoni haikuridhika na uamuzi huo wa Mahakama na kwa kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali walikata rufaa Mahakama Kuu. Shauri hilo liko Mahakamani mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuyalinda maeneo ya wazi na maeneo ya huduma za jamii ili yasivamiwe. Natoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na vyombo vinavyohusika katika kuyalinda maeneo hayo kwa manufaa ya wananchi wote.

**SPIKA:** Kwa kuwa liko Mahakamani nadhani tuliache kwa sasa.

Na. 23

**Mgogoro wa Ardhi Kibamba, Kiswopa na Mloganzila**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na mgogoro wa ardhi kati ya Chuo Kikuu kishiriki cha Afya Muhimbili na wananchi wa Kata ya Kibamba, Mloganzila na Kiswopa; na kwa kuwa, kumekuwepo na juhudi za Serikali katika kutatua mgogoro huo:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutatua mgogoro huo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo lenye mgogoro liko mpakani mwa Wilaya ya Kinondoni, Wilaya ya Kisarawe na Wilaya ya Kibaha na lina ukubwa wa ekari 3,800. Awali eneo hili lilitolewa na Serikali kwa Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania *(KABIMITA)* iliyokuwa chini ya Wizara yenye dhamana ya Mifugo. Eneo hili lilitumika kwa ajili ya kunenepesha mifugo *(holding ground)* kwa ajili ya kukuza mifugo kwenye Kampuni ya *Tanganyika Parkers* iliyokuwa inazalisha nyama nchini. Kampuni ya *KABIMITA* ililitelekeza eneo hili kutokana na kiwanda cha *Tanganyika Parkers* kusimamisha uzalishaji wa nyama. Sehemu ya eneo hilo inatumika kwa Mnada wa Mifugo Pugu na eneo lingine lilivamiwa na wananchi kwa ajili ya kilimo na makazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili kiliomba kumilikishwa eneo hilo kwa ajili ya kujenga Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya na Hospitali ya Rufaa. Kutokana na mchakato wa kulitoa eneo hilo kwa waombaji, wananchi walipinga hatua hiyo kwa hofu ya kunyang'anywa maeneo waliyovamia. Tangu kipindi hicho, eneo hilo limekuwa na mgogoro ambao unaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa shughuli zitakazofanywa na Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili kwenye eneo waliloomba, inafanya uchambuzi wa kubaini wakazi, idadi na thamani ya majengo na mazao yaliyomo ndani ya eneo linaloombwa kwa lengo la kulipa fidia. Aidha, Serikali ilikwisha kuzuia

maendeleo ya aina yoyote kwenye eneo lenye mgogoro. Mara taratibu zitakapokamilika, Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili watamilikishwa eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi nina swali moja la nyongeza. Swali langu ni kwamba wanakijiji wamesema kwamba wamemwandikia Waziri barua kwa madhumuni ya kulizungumzia hili suala bila majibu? Je, Waziri ana mpango wowote wa kwenda kukutana na wanakijiji hao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba wametuita na hatukwenda kwanza. Naomba kusema kwamba tumefanya mikutano kadhaa kwa kupitia Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wa Mtaa wa eneo hilo, Afisa Mtendaji wa Kata pamoja na wananchi wa pale na tukakubaliana na tumeweka kabisa ilani kwamba wasiendelee kujenga na sasa hivi tunachokifanya kwa wale ambao wako katika eneo kwa huruma kabisa Chuo cha Afya cha Muhimbili kimekubali kufidia, lakini watakaojenga upya hawatafidia. Kwa hiyo, tuko tayari na sasa hivi tunaendelea kuongea nao ili kuhakikisha kwamba tumeweza kuwaondoa na kupata eneo kwa ajili ya chuo. *(Makofi)*

Na. 24

**Wanafunzi kukosa nafasi shule za sekondari za Serikali**

**MHE. SUSANA A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* unahimiza kila Kata kuwa na shule moja ya sekondari; na kwa kuwa wanafunzi wengi waliomaliza shule za msingi mwaka 2005 wamefaulu lakini wamekosa nafasi katika shule za Serikali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wanafunzi hao kujiunga na Elimu ya Sekondari?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inawavunja moyo wanafunzi hao hivyo kutafanya juhudi za makusudi kwa kuona kwamba hata wakifaulu hawapati nafasi katika shule za sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Susana Lyimo, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge kupitia Viti Maalum.

Aidha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya mafanikio ya *MMEM,* ni kuwawezesha wahitimu wa darasa la saba kufanya vizuri katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Ufaulu katika mitihani ya darasa la saba umepanda kutoka asilimia 25 ambayo ilikuwa wanafunzi 110,633 mwaka 2001 kabla ya *MMEM* na kufikia asilimia 62 mwaka 2005 ambayo ni wanafunzi 305,062, karibu mara tatu ya idadi ya waliofaulu kabla ya *MMEM.* Hali hii imesababisha vijana wengi waliofaulu kukosa nafasi katika shule za sekondari zilizopo. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004 - 2009 ulianzishwa ili kuboresha Elimu ya Sekondari na pia kuongeza nafasi katika ngazi hiyo ya Elimu ili iweze kupokea vijana wengi wanaohitimu Elimu ya Msingi. Katika Mpango huo inatarajiwa 40% tu ya wahitimu wa Darasa la Saba mwaka huu wapate nafasi katika shule za sekondari. Lengo ni kufikia 50% ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susana Lyimo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imepanga kufungua shule mpya na kuongeza mikondo hadi kufikia minne katika shule zote za sekondari. Pia shule zote za sekondari zilizoko mijini zimeruhusiwa kuendesha masomo katika awamu mbili *(Double Session).* Aidha, Serikali inahimiza wadau mbalimbali kufungua shule binafsi za sekondari katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata elimu katika ngazi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haitarajii kuona wanafunzi wanavunjika moyo wa kutofanya juhudi za makusudi katika masomo kwa mawazo kuwa hata kama wakifaulu hawatapata nafasi katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nafasi za sekondari kuwa chache tunatarajia kuona wanafunzi kuongeza juhudi zaidi katika masomo ili kushindania nafasi hizo, kwa kuwa wale wanaopata alama za juu zaidi ndiyo wanaokuwa katika nafasi nzuri ya kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama nilivyosema katika sehemu (a) ya jibu, Serikali katika kutekeleza *MMES* inaendelea kushirikiana na wananchi kufungua shule nyingi zaidi. Naamini wanafunzi wetu na wahusika wengine watatiwa moyo kwa kuona juhudi hizi za Serikali za kuendelea kupunguza tatizo la ukosefu wa nafasi za sekondari hatua kwa hatua. *(Makofi)*

**MHE. SUSANA A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza. Je, katika kuongeza hizo *double session,* tunaelewa kwamba shule nyingi za Serikali zina upungufu mkubwa wa walimu, Wizara yako imejiandaa vipi katika kuhakikisha kwamba shule hizi zitakuwa na walimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la walimu ni la nchi nzima. Hivyo tunatarajia katika mpango huu wa *double session* kuwatumia walimu wale wale walioko katika shule zetu lakini pia kujaribu kutumia wale walimu ambao wamestaafu hivi karibuni na wanaweza kuendelea kufanya kazi hii kwa kushirikiana na walimu waliopo ili kuweza kuondoa tatizo hili la ufundishaji katika miji yetu hasa kwa huu mpango wa *double session.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha. Katibu!

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kunishangilia. Katibu! *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni Tarehe 30 Desemba, 2005

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana tulikuwa tunaendelea na majadiliano kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Sasa nitawaita wafuatao. Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuata Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Mheshimiwa John Paul Lwanji, ajiandae.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mambo mazuri iliyofanya kuhusu njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua jukumu la kutembelea maeneo mengi yenye njaa na imeshachukua hatua pamoja na kwamba tuna chakula hapa nchini lakini bado imeendelea kuagiza chakula kingine na vile vile wafanyabiashara kupata kibali cha kuagiza chakula bila kodi na pia kuzishirikisha Balozi mbalimbali ili zitusaidie kutuletea chakula cha msaada. Kwa niaba ya wananchi wa Iramba Mashariki, naipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula kimeshaanza kupatikana lakini kuna maeneo bado ugawaji sio sahihi. Naomba Serikali kwa sababu imeshajua nchi nzima ina njaa iendelee kupeleka chakula na kama Mheshimiwa Rais alivyosema jana sasa hivi wananchi wengi hawana uwezo wa kulipia chakula kile kwa hiyo, tunaomba Serikali itafute njia ya kusaidia. Hili ni janga kubwa na kwa vile Serikali imesema hakuna mwananchi wake atakayekufa njaa, sasa hivi wahakikishe chakula kinakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alitaja mambo kumi ambayo Serikali ya Awamu ya Nne itayazingatia. Mimi nisome namba tano inayosema, "Serikali ya Awamu ya Nne, itaimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia wake, tutapambana na uhalifu wa kila aina na majambazi hayataachwa yatambe yanavyoona."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kipengele hiki kinavunjwa tena kinavunjwa kwa makusudi na kiwango cha hali ya juu sana. Ujambazi umekithiri sana hapa nchini na hali hiyo inachafua sifa nzuri iliyonayo Serikali ya Awamu ya Nne. Sasa ni juu ya Serikali kuhakikisha jambo hili linakomeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majambazi wanaofanya uhalifu wana ujuzi sana wa kutumia silaha kubwa na silaha za aina mbalimbali. Inasemekana wengine wametoka katika Majeshi ya nchi jirani, wengine ni wanajeshi wetu humu humu ambao walifukuzwa kazi kutokana na uhalifu. Kama tunavyojua Jeshi letu la Polisi, kazi yake ni kulinda usalama wa ndani na mafunzo wanayopata ya kutumia silaha sio mafunzo ya hali ya juu sana, sasa umefika wakati ni lazima Serikali ibadilishe utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Jeshi la Wananchi ni kulinda mipaka yetu na kuhakikisha hatuvamiwi lakini mafunzo wanayoyapata ni ya hali ya juu sana. Mimi naishauri Serikali, sasa hivi wenzetu wa Polisi wapate mafunzo kama ya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa makusudi kabisa, hatua hii ichukuliwe haraka la sivyo wananchi wetu watazidi kufa, mabenki yetu yatazidi kubomolewa na hata sisi wenyewe tutaingiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kabisa Jeshi la Polisi, Magereza, wapate mafunzo ya Kijeshi hata kwa miezi kadhaa kutoka kwa Jeshi la Wananchi, baadaye ndio waende kusomea utaalamu mwingine walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawapongeza sana *FFU* ingawa nao mafunzo haya ya hali ya juu hawajapata, ningeomba sana wapate mafunzo kamili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba mu-*observe* utaratibu, hamuwezi kupita kati ya Spika na Mzungumzaji. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kusema kwamba ni lazima Serikali itafute mikakati mipya. Sasa hivi amani na utulivu, usalama wa raia hapa nchini haupo, wananchi wetu wanakwenda kwa mashaka. Juzi mtu amevamiwa na majambazi kwenye gari ndogo, sasa hiyo kwa kweli inatupeleka mahali pabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa sababu imeamua na ilitamka yenyewe, sasa wakati ndio huu. Polisi wetu wengine wanakimbia wanaposikia majambazi wapo au wanasita kwenda mpaka majambazi waondoke. Hiyo inaharibu sifa ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kuzungumzia kidogo juu ya miundombinu. Mheshimiwa Rais amesema kabisa kwamba atahakikisha miundombinu mbalimbali kama barabara, mawasiliano ya simu na kadhalika yanatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu za vijijini ni mbovu kabisa. Wananchi wetu wanashindwa kusafirisha mazao yao kwa sababu magari hayaendi huko. Mimi naipongeza Serikali kwa sababu imeshakamilisha barabara za Kitaifa. Sasa zile fedha zihamie kwenye barabara za vijijini, zihamie kwenye barabara zinazounganisha Mikoa na Mikoa ambazo sio za Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mikoa ya Kati, Mikoa ya Kaskazini, tuna barabara ambayo ni muhimu sana na magari karibu yote makubwa na madogo yanapita wakati wa kiangazi. Hiyo ni barabara inayounganisha Mkoa wa Shinyanga, Singida na Mikoa mingine kupitia Mto Sibiti. Serikali ilishasema itatengeneza daraja hilo na kutengeneza kilometa 18 ambazo ziko Iramba Mashariki ambazo ndio huwa zinasababisha vurugu wakati wa masika. Naomba kusema hivi ahadi zimetosha sasa Serikali ianze kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile barabara ni muhimu sana. Sasa hivi mvua zimenyesha, magari hayapiti, lakini ni barabara ya mkato na wafanyabiashara wakubwa wa Mikoa hii yote ya Kaskazini, Kati na Mikoa ya Ziwa na hata nchi jirani wanatumia barabara hiyo. Naomba Serikali na nashukuru asubuhi Waziri wa Miundombinu amesema atapitia barabara hizo na mimi nitamwona, nitamshauri na tunaomba Serikali ifanye hivyo. Sisi Wabunge wa Meatu, Iramba Mashariki, Mbulu na Karatu kwa miaka mingi iliyopita tumekuwa tunaishauri Serikali sasa ni wakati wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya kilimo. Kweli kilimo chetu bado ni duni, tunatumia jembe la mkono, wachache wanatumia wanyama kazi na wachache zaidi wanatumia matrekta. Lakini kilimo cha kusubiri mvua hakitatufikisha kule tunakokwenda. Tuna makorongo mengi ambayo wakati wa masika yanajaa maji, sasa umefika wakati kwa makusudi kabisa kuzuia hayo makorongo yasipeleke maji kwenye Maziwa ambayo hayana faida. Tuzuie maji hayo kwa ajili ya kilimo na vile vile tuchimbe mabwawa, nenda Zimbabwe, *South Africa* wanatumia mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Sisi tungekuwa tumefanya hivi leo tusingekuwa na njaa, lakini tunahangaika kwa sababu hatujaweka dhamira yetu ya makusudi kukabiliana na tatizo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wanajituma sana kulima. Sasa hivi karibu Mikoa mingi ya Tanzania, wananchi walilima lakini mazao yamenyauka lakini hakuna mvua, lakini tungekuwa tumekinga mito na kuchimba mabwawa na visima virefu kwa ajili ya umwagiliaji tusingekuwa na tatizo hilo. Mimi nashauri kabisa kama Mheshimiwa Rais wetu alivyosema hatua za makusudi zichukuliwe ili sisi Watanzania tujikomboe. Ni bahati nzuri tu uchumi wetu sio mbaya sasa hivi, tuna fedha za kutosha kidogo, je, ingekuwa wakati ule hatuna fedha? Wananchi wengi sana wangekufa na njaa. Naomba suala la kilimo liwekewe mkazo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi niongelee juu ya maslahi ya watumishi wote hapa nchini. Watumishi wetu kwa kweli wanapata kipato ambacho hakiwezi kumwezesha kuishi kwa mwezi mzima. Mishahara ya watumishi wetu wote haikidhi mahitaji ya watumishi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umefika wakati kwa makusudi Serikali ipitie upya na ile watumishi kutopata mshahara wa kutosha ndio unahamasisha rushwa, unahamasisha wizi na mambo mengine yanayokwenda kinyume na taratibu za Serikali. Mimi naomba, maslahi ni kitu cha kwanza.

**WABUNGE FULANI:** Ndio! *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSIDAI:** Watumishi wetu wote waangaliwe, walimu, madaktari, mabwana kilimo na wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi walimu wana madai mengi sana, madaktari wana madai mengi sana, sasa ni juu ya Serikali, Serikali inataka ipate huduma nzuri kutoka kwa hawa watu lakini Serikali haiwajali. Huu mtindo kwa kweli ndio unaofanya sisi tusiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nikirudi tena kwenye miundombinu, wananchi wetu wameamka, wanataka wapate simu za mikononi na kwa wingi wanataka wanunue simu hizo. Kwa makusudi kabisa Serikali ibane haya makampuni ya simu yapeleke mitambo kule vijijini. Sasa hivi tuko kwenye dunia ya kileo, wananchi wetu wanataka kuwasiliana na watoto wao, Serikali badala ya kufunga safari atoke kwenda kudai pensheni Dar es Salaam anaongea na Katibu Mkuu Hazina anaambiwa mambo yake yamefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu *Celtel* waliahidi kujenga mtambo haraka iwezekanavyo na waliahidi wangemaliza mwishoni mwa mwaka uliopita mpaka sasa wamekaa kimya. Wananchi zaidi ya 10,000 wamenunua simu, wanapiga kelele. Sasa naomba kwa makusudi kabisa Serikali iliangalie hilo na sio Iramba Mashariki tu ni kote Tanzania. Kwa hiyo, nawaomba sana sasa hivi tuende kwenye dunia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo juu ya kuondoa umasikini. Kuna MKUKUTA, MKURABITA na mengine yote. Naiomba Serikali iwahishe haya mambo. Wananchi wetu kwa kweli wako tayari kujiletea maendeleo lakini bado tunaambiwa kwa makongamano, kwa semina na kadhalika. Tunaomba utekelezaji uanze haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipitisha sheria ya masoko lakini mpaka sasa imenyamaza, Rais alishasaini sijui imeishia wapi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ili kuhimiza kasi mpya, ari mpya ni lazima mambo haya yaende kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishie hapo ili niwapishe na wenzangu watoe michango yao, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo muhimu. Kamati ya *PAC,* watakuwa na mgeni mchana huu saa sita na nusu kwa hiyo, wakutane katika chumba cha *Chief Kasusura,* tangazo limetoka kwa Mwenyekiti wao, Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, ambaye ni Katibu wa *Amani Forum Region,* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa *The Great Lakes Parliamentarian Forum on Conflict Resolution and Peace Management, Amani Forum Tanzania,* inakaribisha maombi ya usajili wa wanachama wapya ambao watapenda kujiunga na chama hicho cha kihiari Bungeni. Naomba uwajulishe Waheshimiwa Wabunge kuwa kuna dokezo lenye fomu za usajili linapitishwa ili kufanikisha zoezi hilo.

Sasa mimi nashauri kwamba Katibu huyu awakaribishe kwenye ukumbi fulani halafu awaeleze *Amani Forum* ni nini halafu wajaze fomu vinginevyo kujaza fomu bila kuelewa wanajaza nini pengine sio vizuri. *(Makofi)*

Tangazo la tatu, orodha ya wasemaji imebandikwa kwenye *notice board* pale, kwa hiyo, kila mtu anayechangia atajiona yuko pale na ukikuta namba yako ni ya mbali maana yake huwezi kuchangia karibuni. Maana ziko barua nyingi za salaam niko wa ngapi, mimi wa ngapi, kwa hiyo, orodha iko pale. *(Makofi)*

Tunaendelea!

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ambayo imetoa msisimko mkubwa na imeonyesha dira ya kwamba sasa tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupa pongezi kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na nakuhakikishia nitakuunga mkono kwa siku zote utakazokuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pongezi kwa Spika tuliyemchagua juzi na kura yangu nilimpa. Pia nampa pongezi Waziri Mkuu na Rais wetu wa Tanzania Mheshimiwa sana Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Moshi Mjini ambao walinichagua kwa kishindo, wanachama wa CCM pamoja na wa CHADEMA na wa vyama vingine ambao wote waliungana na kunichagua kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake anatutaka sisi Wabunge tuchangie kwa kuonyesha ni namna gani ile hotuba yake inaweze kuleta maendeleo katika nchi yetu. Katika hotuba yake anataka tuangalie uchumi endelevu ambao utawasaidia Watanzania katika awamu iliyopita tuliona na tumeona uchumi wa nchi Serikali inasema umekua na ni kweli

uchumi wa nchi umekua lakini uchumi wa nchi umekua kwenye makaratasi na kwa wageni sio kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wa kawaida na Mheshimiwa Rais ametamka juzi ya kuwa uchumi wa nchi ukikua ni kwenye mifuko ya wananchi apate angalau milo miwili kwa siku. Lakini Tanzania kwa muda mrefu tumekuwa tunajenga uchumi ambao umewafaidisha wageni kuliko wakazi wa nchi hii kitu ambacho ni cha hatari lakini kwa sasa tumeona mwelekeo ambao unabadilisha ile *trend* na sasa tunataka kubadilisha uchumi kwenye wakazi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka uchumi endelevu katika utalii, nitatoa mfano wa wenzetu wa Italia nchi ambayo imeendelea na Mozambique ambayo hajaiendelea ni kama sisi wenzetu. Hawa wenzetu katika utalii, tuseme katika ufukwe wa Tanzania badala ya kuleta wageni wakajenga mahoteli kwenye ufukwe wananchi wenyeji wanaokaa katika sehemu zile Serikali inawawezesha, inawafundisha namna ya kupika chakula, namna ya kufua nguo za wageni, namna ya kuwapokea na namna ya kuwatunza wakati wakiwa pale, pesa wageni watakazolipa zitabaki hapa nchini zote. Lakini mtindo wa Watanzania walioujenga na ambao ndio ulioko sasa tunasema tunajenga utalii Tanzania sio kweli tunajenga utalii tunawajengea wenzetu, wanatoka kule wanakuja hapa na zile pesa wanarudisha kule kule na unamkuta Mtanzania anabaki maskini pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalojaribu kulisema ni kwamba Serikali kwa makusudi kabisa ingebadilisha mwelekeo kwa sasa, ingewekeza kwa wenyeji wanaokaa katika sehemu zile na sio wageni. Ingewakopesha au ingewajengea wakaendesha zile hoteli ndogo ndogo na tuna uhakika zile pesa zingerudi kwa sababu hazitakwenda tena nje zitabaki hapa nchini lakini tumekuwa na mtazamo mbaya wa kuwajenga wageni badala ya kujenga wananchi wa hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie suala hili vizuri kwa sababu tunaposema ya kuwa nchi imepata mapato makubwa kutoka kwenye utalii, hawatuambii ni ngapi zimesafirishwa kupelekwa nje, unaweza kukuta hatubakiwi na chochote hapa! Wale wale wanaoleta wale wageni ni wale wale wanaokuja kuwalisha hapa, ni wale wale waliojenga majumba, ni wale wale wanaotoa zile pesa kuzipeleka nje, tunasema utalii umekua, sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema tunataka uchumi endelevu sio lazima tuwe na viwanda kila mahali. Siku hizi tubadilishe mwelekeo *raw material* ifuate viwanda kule viliko sio viwanda vifuate *raw material.* Tumekuwa tunangojea, tunasema Muheza kuna machungwa mengi, tunataka mtu akawekeze kule Muheza ili tuweze kuanzisha kiwanda cha machungwa, *it's a wrong concept.* Tunataka kiwanda kikubwa labda kikae Dar es Salaam wale watu wa kule Muheza wakamue juisi ya machungwa wai-*preserve* wawake kwenye matanki iletwe Dar es Salaam na kila mahali nchi nzima inaweza kufanya hivyo hivyo na sasa kila tunda Tanzania linaweza kuwa-*preserved* na kuwa *packed* na kuweza kutumika bila tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tujaribu kubadilisha maono yetu tunapoangalia uchumi endelevu, tutaufanyaje uchumi endelevu uweze kwenda mpaka kwa mtu wa kawaida? Tunataka mtu anayelima nyanya sio lazima pawe na kiwanda cha kutengeneza nyanya pale, lakini afanyiwe mpango, si lazima asafirishe lakini anaweza kui-*preserve* isioze halafu aipeleke kwenye kiwanda. Tubadilishe mtazamo *raw material* sasa itafute kiwanda badala ya kiwanda kwenda kutafuta *raw material. It is very expensive* kujenga viwanda Tanzania nzima lakini ukiwa na kimoja mahali pamoja watu wataleta zile *raw materials* na huo ndio uchumi endelevu ambao una-*spread* Tanzania nzima na watu wote wataweza kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makamu wa Rais.....

**WABUNGE FULANI:** Eeh! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio mwanzo wa kukupandisha cheo na huenda ukawa Makamu wa Rais katika kipindi kijacho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Rais amezungumzia juu ya mikataba. Tumekuwa tunapiga kelele juu ya mikataba mibovu ambayo imeiletea nchi matatizo mengi. Sisi tunasema, kama alivyosema ataipitia ile mikataba, tungependa ipitiwe na ikishapitiwa na iletwe hapa Bungeni sisi Wabunge tuiangalie na tuifanyie kazi na wale wote waliohusika kuiingiza nchi hii katika matatizo ya madeni makubwa wachukuliwe hatua za kutosha. Tusianze kuoneana aibu ya kuwa huyu ni nani lakini wakati tunataka kufanya kazi ya kuikomboa nchi hii katika matatizo ambayo imekwishayafikia, kwa kweli tusioneane aibu, tufanye kazi kwa kujua tunafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, tumezungumzia matatizo ya Muungano. Kwa miaka mingi tangu tuwe na Muungano pana manung'uniko ya Muungano hayajawahi kuisha, kila siku yapo. Tumekuwa na Tume ya Jaji Francis Nyalali ikatoa mapendekezo ya kuwa ili tuondoe matatizo ya Muungano tuwe na Serikali tatu. Serikali ikapokea ripoti ile ikakataa ku-*implement.* Jaji Kisanga kaja baada ya miaka chungu mzima akatoa mapendekezo yake ya kuwa ili tuondoe matatizo ya Muungano ni lazima tuwe na Serikali tatu, bado Serikali ikakataa. Sasa tumefika mahali huu mmomonyoko unaendelea na waanzilishi wa Muungano ni wachache walio hai ambao wanajua huu Muungano ulianzaje. Mimi ningeona ni jambo la busara tulishughulikie jambo la Muungano ili liishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo moja kule Moshi labda nisiache kulizungumzia maana yake naona umeshapiga kengele. Kuna *National Housing.* Tulipopitisha sheria hapa ya kuwapa ruhusa ya kufukuza wapangaji sugu ambao hawajalipa kodi, kule Moshi wanafanya vioja. Wanakuja wewe ni mpangaji kama unadaiwa, wanafika kwenye nyumba hata mwenye nyumba hayupo ndani wanavunja nyumba na wanahamisha vitu ndani. Sidhani kama sheria tuliyopitisha hapa ni ya kwenda kuvunja nyumba za watu na kuchukua vitu vyao ndani. Sidhani hiyo ndiyo sheria inayompa nguvu mtu mwenye nyumba kumfanyia unyama mpangaji namna hiyo lazima

kuna kanuni, hata kama tumewapa nguvu ile, kuna kanuni za kufanya kazi hiyo. Wanakwenda wanamtafuta dalali anapewa nguvu hizo wanakwenda kuvunja nyumba za watu na wanachukua vitu vya watu hata mwenyewe hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Ardhi na Makazi, namkaribisha aje Moshi, aje akaone na kutatua tatizo lile. Ni matatizo makubwa *National Housing* wanatufanyia kule Moshi. Wengine wanakaa katika nyumba za kupanga za *National Housing* wanaambiwa wanauziwa wanapewa mwezi mmoja kulipa, kibanda cha vyumba viwili wanauziwa kwa shilingi milioni 20 na zaidi lakini tuna uhakika kuna viongozi wa Serikali wanakaa Oysterbay wameuziwa majumba ya ajabu kwa shhilingi milioni 10 na wanapewa miaka 10 kulipa, hawa watu wanapewa mwaka mmoja tu, haki iko wapi? Ni vizuri jambo hili likaangaliwa kwa sababu sijui kama kuna mji mwingine unatendewa mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilizungumza hapa juu ya viwanda japokuwa Waziri kweli alinijibu lakini inasikitisha hata Kiwanda cha Bia ambacho kilikuwa kina-*employ* zaidi ya watu 10,000 kilinunuliwa na kikafungwa, kuua Moshi kabisa. Unanunua kiwanda watu 10,000 wanategemea pale maisha yao halafu unakifunga, sasa tusemeje? Ule mji hauko Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unakwisha lakini kidogo ningezungumzia juu ya chakula. Mimi naomba kusema nyama ni chakula lakini wengine wanasema ni kitoweo, tunajua jua linazidi kuendelea na ng'ombe watazidi kufa basi tutafute mkakati wa kufanya zile nyama zikaushwe wananchi wale. Ipi bora mwanafunzi aende na *cotton cake* au nyama iliyokaushwa akaenda nayo mfukoni? Tukubaliane na wale wafugaji na Serikali isaidie.

Mifugo ambayo tunayo Tanzania ambayo inakufa badala ya kufa ni chakula kile jamani, ndugu zangu ni chakula. Tuna njia zetu za kiasili za kukausha nyama zikakaa miaka na miaka tukala, zile nyama zikaushwe wananchi wale tutawakomboa wananchi katika janga la njaa, tunajua mvua isiponyesha watazidi kufa hawa ng'ombe. Tungekuwa na *mobile canning* ambazo zingeweza kufanya hizi nyama zikawa *caned* badala ya hawa ng'ombe kufa kwani wanakufa halafu tunazika maana yake nini na watu wanakufa njaa, tusindike hizi nyama na ziweze kupelekewa watu wale na tutaokoa badala hata ya kuagiza vyakula nje hizi nyama zingekuwa chakula wenzetu sisi nyama tunakula ni chakula siyo kitoweo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unakwisha lakini kidogo ningezungumzia juu ya muafaka wa Kitaifa kama Rais alivyosema kwamba anataka tuwe na muafaka wa Kitaifa katika nchi hii. Kama tunataka kujenga muafaka wa Kitaifa katika nchi hii Serikali haingewatenga wapinzani na wao wangeshirikishwa katika Serikali, wangeshirikishwa katika Ubalozi, wangeshirikishwa katika kuwekwa katika makampuni kama kwenye bodi, kama kweli tunataka muafaka wa Kitaifa ili tuweze kuwatumia Watanzania wote tuwe na mwanzo na pia tuwe na mwelekeo mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kalizungumza Mheshimiwa Rais na nina imani alilolisema ni la msingi na ninajua labda niliyoyazungumza atayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa John Paul Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Suleiman Saddiq, ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii ambayo ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai tokea wakati wa mchakato wa uchaguzi mpaka hivi sasa. Wengine madiwani na watu wengine hawakuweza kuona na kufikia siku kama hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu mwenyewe hajaridhia ni wapi waendelee kuwa hai na wapi awachukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kwa kunipa ushindi mkubwa na kuweza kuja hapa. Pia nikishukuru Chama changu kwa kuridhia utashi wa wananchi kwa kura nyingi tu na Singida ilikua mkoa wa pili kutoka mkoa wa Singida kwa *percent* ya kumpa kura Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuunda Baraza la Mawaziri linalokidhi falsafa nzima ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, pamoja na kwamba Baraza hilo ni pana haina msingi. Baraza hilo limeundwa kushambulia kero zilizoainishwa kwenye hotuba kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni kubwa na ni Muungano wa nchi mbili na hivyo matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ni mapana vile vile kama unavyoona Baraza hilo kuna mseto wa vijana na wazee bila kujali jinsia dini wala rangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mawaziri wanawake walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali. Rais amewaamini, nasi tutakuwa pamoja katika kutekeleza majukumu yao lakini wakumbuke kwamba wamekuwepo akinamama wengine duniani ambao wameshika nyadhifa nyingine mbalimbali siku za nyuma na hata sasa hivi wapo na mifano ipo mingi, mfano Ulaya yupo Mama Angella Michael, Glory Aroyo na Liza Aloyce na hivi majuzi tu Afrika imeshuhudia kuibuka kwa mwanamke wa kwanza Rais Bibi Ellen Johnson Sirleaf wa Liberia huyu ni mfano wa kuigwa katika mapambano ya kijasiri ya kuinusuru kwenye makucha ya mabwana wa vita na ni juzi tumeshuhudia hatua kali alizochukua za kuwafurumusha maafisa wote wa Wizara ya Fedha katika hatua zake za awali za kupambana na rushwa. *(Makofi)*

Kana kwamba haitoshi huko Amerika ya Kusini nchini Chile mwanamama Bibi Michelle Batileti amekuwa Rais wiki iliyopita na kuwateua Baraza la Mawaziri la aina

yake ndani ya usawa wa jinsia yaani wanaume 10 na wananwake 10, wawili kati yao amewapa Wizara nyeti za Ulinzi na Fedha. Kwa hiyo, haya mambo siyo mapya tunayoyashuhudia hapa kwetu

Katika ndoto za Marehemu Dr. Martin Luther King, kuhusu habari za usawa kwa watu wote nadhani ndoto hii imetimia kwa wanawake, enzi za wanawake kuwaweka jikoni sasa hivi zimekwisha, ikumbukwe kuwa alikuwa ni mwanamke aliyewasha moto wa kupinga ubaguzi wa rangi huko Marekani pale alipogoma kumpisha kiti cha mbele mzungu kwenye basi kama sheria za wakati huo zilivyoagiza. Nchi ya Marekani ilitikisika na hatimaye sheria hizo za kibaguzi zikafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri wanawake wengine walioshika nyadhifa mbalimbali nchini waige utendaji wa viongozi wetu wanawake hawa walioteuliwa. Nasema hivyo kwa sababu sehemu nyingine wanawake wamepewa madaraka lakini badala ya kuwasaidia wenzao wamekuwa ndiyo vizingiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 8 ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Rais anazungumzia maadili ya viongozi wa kisiasa wakati umefika wa kurudisha maadili ya uongozi siyo tu kwa viongozi wa kisiasa, bali kwa yeyote ambaye ni kiongozi wa umma na hapa ikibidi likaziwe zaidi kwa kuwepo sheria ambayo itawabana wale wote watakao kiuka maadili tuliyojiwekea ili kulinda amani, utulivu na umoja wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua nchi hii ni ya utawala wa sheria lakini sheria ya kuwaweka kizuizini wale wote wanaochochea vurugu zihuishwe na kufanya kazi ili kuwadhibiti viongozi hao ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo maalum ya uraia wakati wanapokuwa huko.

Katika ukurasa wa 9 Mheshimiwa Rais anazungumzia kuhusu fedha kununua viongozi, ni kweli usiopingika kuwa kwa sasa gulio la ununuzi wa uongozi na hasa wa kisiasa unazidi kupanuka. Sasa hivi ni rahisi kwa wajanja kukupa bei ya udiwani, ubunge na pengine huko mbeleni hata bei ya kuupata urais inaweza kufahamika, hii ni hatari sana kwa Taifa letu, chimbuko kubwa la tatizo hili ni rushwa iliyotuzunguka, kama tutaweza kupunguza rushwa hii tatizo hili litaanza kupungua gharama za Msingi katika uchaguzi zingefanyiwa utafiti ili zijulikane baada ya hapo wagombea wabanwe kwa kuweka sheria ya kuwataja hadharani wadhamini ili umma uweze kumwelewa kiongozi mtarajiwa na washiriki wake, vilevile wadhamini hao lazima wataje kiasi watakachokuwa tayari kumchangia mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majukumu ya msingi ya Serikali ya awamu ya nne Mheshimiwa Rais ameainisha mambo kadhaa ambayo mengi tumekuwa nayo tangu tupate Uhuru. Amezungumzia kuhusu Utaifa ambao hata mimi naungana naye kuwa ili tusisambaratike msukumo mpya unahitajika ili kuendeleza Utaifa tuliorithishwa na Marehemu Baba wa Taifa na Mzee Karume. Vita dhidi ya maadui wakuu watatu ujinga,

umaskini na maradhi inabidi iongezewe ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ikiambatana na mikakati mipya ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nzi, mbu na wadudu walioingia baada ya madirisha kufunguliwa ni jukumu letu sote kuona wanadhibitiwa, hii ikiwa ni mwendelezo wa kazi nzuri aliyoanzisha Rais Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 majukumu mawili ya msingi ni kwanza kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa kiuchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea.

Pili, ni kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umaskini katika kutekeleza ilani hii Mheshimiwa Rais amejiwekea mambo takriban 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo hayo 10 mimi nitachangia machache ili niwaachie na wenzangu wachangie vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia Umoja wa Kitaifa. Akizingumza kuhusu Umoja wa Kitaifa Mheshimiwa Rais amezungumzia umoja kati yetu sisi yaani makabila 120 pamoja na wenzetu kutoka upande wa pili wa Muungano. Muungano wetu umekuwa na matatizo siyo kwa sababu ni mbaya, la hasha! Tatizo tulilonalo ni kwa sisi tuliopewa dhamana ya kuulinda badala ya kufuata dhamira nzuri ya waasisi wake tumetumbukiza maslahi binafsi na kuyahalalisha kuwa ndiyo matatizo ya Muungano hivyo kama anavyosononeka Mheshimiwa Rais kuhusu mpasuko kati ya Pemba na Unguja hata mimi nasononeshwa na hali hiyo pamoja na Wapemba kutapakaa nchi nzima inashangaza kuona yaliyotokea huko visiwani.

Mheshimiwa Spika, kisiasa nchi imegawanyika vipande viwili, nadhani mpasuko wa kisiasa Zanzibar usichukuliwe tu kwamba ni siasa, viongozi warudi kwa wananchi kwenye Kata na Vijiji kujua kwa kina tatizo liko wapi na ni kwa nini hawa ndugu zetu Wapemba wawe hivyo.

Ningependa pia kutoa wito kwa wenzetu wa Zanzibar kuwa Muungano huu tunawajibika kuulinda kwa gharama yoyote ile kwa sababu ndiyo uliotufikisha hapa tulipo hata tukaweza kukutana hapa kujadili haya tunayoyajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo niliyoyazungumzia tatizo la ukabila, ukanda, udini na rangi linashabikiwa zaidi na baadhi ya viongozi ambao kimsingi wameshindwa kabisa kutekeleza majukumu waliyopewa na badala yake hujishughulisha zaidi na ubunifu wa mikakati ya kuhakikisha wanabaki hapo walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inachangiwa zaidi na mfumo wetu wa jinsi ya kupata viongozi tangu ngazi ya chini kabisa hata ngazi ya juu, mambo ya uongozi yamerahisishwa sana kiasi cha kuwapa ujasiri hata wale wasio na uwezo kuanza mikakati ya kuusaka uongozi kwa gharama yoyote ile, hapa ndipo tatizo la udini, ukabila, ukanda,

rangi na rushwa linapoanza pengine ipo haja ya kuangalia upya utaratibu tulionao ili kuhakikisha kwamba wababaishaji hawa hawatakuwa na ujasiri wa kuusaka uongozi kwa udi na uvumba kama wafanyavyo hivi sasa tukiwaachia watatuvuruga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikakati ya kujenga Utaifa Mheshimiwa Rais anakusudia kutumia mfumo wa elimu kujenga na kuimarisha Umoja Kitaifa ikiwemo kutenga shule za sekondari za Kitaifa zitakazochangia kwa makusudi zitakazochanganya wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kutoka pembe zote za Tanzania. Pamoja na shule hizi za wenye vipaji mimi ningeshauri twende mbele zaidi kwa kuhakikisha kuwa angalau kila mkoa uwe na shule tatu za bweni ambazo nazo zipewe jukumu la kukusanya wanafunzi kutoka kila pembe ya nchi.

Kuhusu amani na utulivu tulio nayo naona hapa nchini bado ni kitendawili kwa wajanja wengi wa dunia hii ambao kwao vurugu ndiyo kigezo cha biashara zao kukua na kupata faida kubwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais moja ya sababu zilizojenga amani hii ni sera ambazo kwa makusudi zilijenga hisia za umoja na hazikubagua Watanzania kwa sababu za dini, rangi kabila, jinsia au maeneo wanakotoka, matarajio yake ni kuwa Serikali aliyoiunda itatakiwa isiwabague wananchi kwa sababu yoyote ile na wawe watetezi thabiti wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Vile vile amependekeza tuwe na maadili ya miiko ambapo kiongozi wa Chama chochote kiwe Chama Tawala au cha Upinzani, Chama cha Hiari au Chama cha Wafanyakazi, Chama cha kitaaluma au Chama kingine chochote kile atajiuzulu mara moja huyo kiongozi ikidhibitika kuwa atajihusisha na sera za ubinafsi, ubaguzi, uchochezi, chuki na zote zinazobomoa umoja wa Kitaifa na kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu. Mimi ningependa kuongeza hata watakaojihusisha na unyanyasaji wa jinsia hawa nao walazimishwe kujiuzulu mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la rushwa ni tatizo sugu katika jamii yetu, kwa bahati mbaya sana vita hii inazungumzwa zaidi katika upande wa majukwaa lakini kwa kweli ni kwamba tunao watu ambao wametajirika kwa kasi ya kutisha katika kipindi kifupi sana kiasi cha kutia shaka utajiri wao. Leo hii ndiyo watu hao hao wanaoalikwa katika hafla mbalimbali na ndiyo wanaoonekana ndiyo raia bora, wananchi wa kawaida wanapolalamika kuhusu hali hii majibu kutoka kwa wahusika yamekuwa ni kejeli za kuwaita wavivu na wana wivu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Rais kuahidi kuimarisha Taasisi zinazohusika na vita, ipo pia haja ya kuzitimiza upya na kuzitazama upya sheria zetu ili kuona kama zinakidhi hali iliyopo sasa, kama mtoa rushwa na mpokea rushwa wote ni wahalifu, je, ni nani atakayemsema mwenzake? ni wakati muafaka sasa wa kuangalia uwezekano wa kumpa kinga mtoa rushwa ili tuweze kuwashika wala rushwa wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mapato na Matumizi ya Serikali, Rais anasisitiza kusimamia vizuri mapato na matumizi ya Serikali na kwamba ni sehemu ya utawala bora, anasisitiza kuwa ataendeleza kazi nzuri iliyoanzishwa na awamu iliyopita na kuahidi kutowavumilia wakwepa kodi na wabadhilifu. Pamoja na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais, Taifa letu linakabiliwa na tatizo kubwa na tabia iliyojengeka

miongoni mwa waliopewa uongozi kuwa fedha za Serikali ni zao na mpango wa kuzitumia ni *agenda* zao binafsi bila kujali maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inawabana sana walipa kodi lakini sheria hii hufikia ukomo mara kodi zetu zinapoingia mikononi mwa warasimu Serikalini. Matumizi ya hovyo hovyo ya fedha za Serikali yamekuwa ni kitu cha kawaida kabisa na wa kuhoji hayupo kwa sababu wote ni washiriki katika ubadhilifu huu. Mkwepa kodi anapokamatwa inakuwa ni *criminal case* lakini mbadhilifu anapokamatwa inakuwa ni suala la kuchukuliwa hatua za kinidhamu, pamoja na kuwepo kwa kanuni za fedha na kanuni za matumizi lakini bado warasimu hawa wanafanya manunuzi mengi na ya ajabu kwa kuzitumia sheria hizihizi ambazo tulifikiri zingeweza kuwadhibiti. Hainiingii akilini kuona mkuu wa Taasisi ya Umma yenye majukumu mengi ya kijamii kununuliwa gari aina ya *Mercedes Benz 500SEL* ilhali wengi walio chini yake hawana hata baiskeli ya kufuatilia majukumu yao katika jamii. Je, wakuu hao watapungukiwa nini wakinunuliwa magari bora na ya bei nafuu ili fedha zinazobakia zitumike kuboresha majukumu waliyopewa kwa jamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhilifu kama huu kwa hakika hauna haja ya kuangukia kwenye hatua za kinidhamu bali warasimu hao wangeshughulikiwa kama wahujumu uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matatizo ambayo nimeishi nayo katika maisha yangu yote ni hili tatizo la maji, kama alivyosema Rais, Serikali yake itaweka msukumo mpya katika kuwawezesha wananchi kupata maji ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae, kwanza saa imefika, Kanuni ya 49 inakataza kwamba Mbunge haruhusiwi kusoma hotuba yake ndani ya Bunge na mchangiaji wa sasa alikuwa anasoma hotuba yake.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli na bahati nzuri wengine wameandika vibarua wananiambia huyu anasoma hasemi ni kifungu gani, ni kweli kifungu 49 (3) inasema hivi hizi ni kanuni za majadiliano inasema hivi; " Isipokuwa kama ameruhusiwa na Spika, Mbunge hatasoma hotuba yake lakini kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake anaweza kusoma madondoo kutoka katika kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia katika kumbukumbu alizoandika na siyo kusoma."

Mheshimiwa sasa amesoma hotuba yote na siyo utaratibu hata yeye mwenyewe akijisikiliza kwenye redio atakuta hakusema vizuri kama angesema bila kusoma. Sasa maana tunajifunza kwa hiyo, nilimuacha aendelee.

Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Saddiq na Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, ajiandae.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mheshimiwa Anne Makinda, napenda kwanza nitoe pongezi zangu kwako. Nimekuona, tumefanya kazi wote tukiwa Mawaziri Ofisi ya Waziri Mkuu na tumekuwa katika mikakati mingi pamoja leo najisikia vizuri kukuona hapo mbele, najisikia vizuri, uko hapo siyo kwa sababu ya kubahatisha ni kwa sababu ya uwezo ulio nao. *(Makofi)*

Kwa sasa hapa duniani tunaanza kuona uwezo wa wanawake wanachukua nafasi mbalimbali siyo kwa sababu wanabahatisha au wanahurumiwa au wanapewa kama fadhila, mojawapo akiwa Elen Johnson Sirleaf, ambaye tumefanya naye kazi *UN* yeye akiwa *UNDP* ni kitu cha kufurahisha kuona akinamama, vijana mnaoibukia ninawaombea wote Mungu awasaidie mfike katika ngazi za juu zaidi na zaidi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amina!

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka nipongeze wote ambao tulishinda katika Uchaguzi Mkuu, Rais wetu ambaye Khartoum aling'ara kama nyota walimkaribisha kabisa unajisikia Marais wenzao wanaona wamepata mwenzao mwenye uwezo na hasa alipotoa hotuba yake mahiri kwa lugha ya kiswahili kilicho sanifu. *(Makofi)*

Ninawapongeza Mawaziri na kuahidi kwamba tutashirikiana nao kwa karibu katika kazi zao kwa sababu kazi zao ni kazi zetu, tumejipanga tu wengine kukaa mbele na wengine kukaa mstari wa nyuma na mnapokuwa vitani wa mstari wa nyuma wakizembea mnashindwa vita. Kwa hiyo, sisi tulio mstari wa nyuma tuna wajibu mkubwa wakati mwingine zaidi kuliko hata walio mstari wa mbele. *(Makofi)*

Ndugu zangu wakati wa kampeni umekwisha na mazungumzo ya kikampeni yakiingia hapa tunaharibu kwa sababu tulipewa siku maalum za kampeni, aliyetukana mwenzake katukana tani yake, aliyemkashfi mwenzake kamkashfu vya kutosha, aliyemshabikia mgombea kashabikia vya kutosha kwa hiyo, mimi matumaini yangu ni kwamba wananchi walitupa nafasi hiyo wakatuchagua kwa makini ili tuje katika nyumba hii tuwafanyie kazi wanayotegemea tuifanye na ndiyo maana leo tunavyojadili hotuba ya Rais ni mwanzo wa kazi, tunachokitafuta ni kuona ni jinsi gani sasa tutakavyotekeleza matumaini waliyonayo wale waliotuchagua.

Mimi wananchi wa visiwa 38 katika Ziwa Victoria wa Wilaya ya Ukerewe wananitegemea sana na wana matumaini makubwa sana na mimi na ninajua na wenzangu ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, katika kujadili nitajiweka zaidi katika utekelezaji wa hotuba hii sina la kuongeza wala kupunguza, Rais alipoiandaa hii hotuba nadhani alikaa kwa makini hakuna eneo ambao hakuligusia kwa hiyo, kazi iliyoko mbele yetu ni kuhakikisha tunatekeleza. Wa mstari wa mbele waondoke kwa mwendo wa kasi na mstari wa nyuma tutaendelea kuwapa nyenzo kwa michango tunayoitoa hapa Bungeni ili mradi tu mtusikilize. *(Makofi)*

Kwanza, la siasa. Suala la siasa ni lazima tulielewe kama Wabunge, sisi wenzenu tumeanza katika Chama kimoja nilikuwa najihisi nilikuwa na uhuru zaidi katika Chama

kimoja kwa sababu niliweza kumpinga mwenzangu wa Chama kile kile kwa nguvu yangu yote na bado tukaendesha nchi mpaka tukaifikisha hapa tulipofika. Vyama vingi vya siasa vina maana moja tu ya kwamba binadamu wote hamuwezi kuwa na fikra sawa, hauwezi kuwa na mawazo sawa katika kuliangalia jambo moja kwa hiyo ndiyo maana vyama vimepewa nafasi ili viwe vinatoa kwa kiingereza wanasema *alternative thinking* siyo *alternative bad image* nadhani tulielewe hilo.

Kwa hiyo, tunaposimama hapa mtu asimame kama ni Chama cha Mapinduzi tunatoa *alternative* ya kwamba katika maendeleo tunachokitaka tumekieleza wazi bayana katika Ilani ya Uchaguzi. Kwa hiyo, sisi kazi yetu tumemaliza kwa hiyo, si suala tena la kutafuta na kubabaika na wote tuliomo humu ili mradi tulikwenda kwa wananchi, wananchi wakasema mmetueleza sera zenu tunazitaka sera za Chama cha Mapinduzi kwa hiyo sasa tunachotekeleza ni sera za Chama cha Mapinduzi ukiwa CHADEMA, *CUF* na wengine hiyo ilikwisha tarehe 14 Desemba, 2005 wananchi wa Tanzania walipoamua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuna kazi moja na tutakapokwenda mwaka 2010 tutatoa tena Ilani ya Uchaguzi na Chama kitakachokubalika ndiyo sera yake itakavyotekelezwa ndiyo siku zote walioelewa na waliobobóea katika siasa wanavyofanya mambo yao. Tuchukua Uingereza kama *Labour Party* ikishinda wataendesha unajua *Labour Party* kama vitu vilikuwa vimekuwa *liberalized Labour Party* itavi-*nationalize,* unajua tu ya kwamba *Labour* sasa imeingia mwelekeo ni huu ni kama sisi ukijua Chama cha Mapinduzi kimeingia kikatetea haki za binadamu, italinda amani katika nchi hii unajua hii ni Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndugu zangu kampeni imekwisha tuelewe siasa kazi ni kutoa hoja na hoja sisi wana Chama cha Mapinduzi tumemaliza na wananchi wamezikubali hoja na Rais wetu ametoa hotuba ya kutuelekeza wapi twende. Nina mchango mdogo tu, mimi naona katika hotuba ya Rais jambo linalonipa matatizo ni moja nalo ni utendaji, utendaji unanifadhaisha.

Nilipoanza kazi ukiiba senti tano zilifunga watu na hakuna mjadala tunaouona kesi iko mahakamani, kesi inakwenda wapi na ninataka nim-*quote* Mheshimiwa Galinoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Galinoma alikuwa ni Katibu wangu Mkuu wakati mimi niko Ofisi ya Waziri Mkuu, alifuata zile sheria walizofundishwa, anakuandikia *memo* kama Waziri, anakupa *alternative* zaidi ya tatu anakuambia nawasilisha kwako na wewe unakuwa unaamua kufuatana na hizo *alternative* ambazo ni *scientific.*

Kwa hiyo, sasa utendaji wa siku hizi mtu anaiba milioni, tunaanza tena kutafuta yule moja kwa moja kama *External Auditor* amekuja akikuta milioni, pingu mkononi atajibu huko mahakamani ndiyo tunavyopaswa kwenda katika kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Lakini huko Wilayani tumekaa na watu pesa hizi tunazozitoa hapa Bungeni wanakwenda wanakula tunakuwa na malumbano wanabadilishwa vituo huko nako wanakwenda kula tunakwenda hivyo hivyo, kwa hiyo, utendaji mimi unanisumbua.

Lakini unanisumbua zaidi inapokuwa watu hawawajibiki, ipo mifano mingi ya watu kutowajibika jambo linatendeka inapaswa kufika mahali Rais Ali Hassan Mwinyi, alishawajibika wakati watu walipokufa Shinyanga leo nani anawajibika?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Kila mtu kakalia kiti chake, tunarudi katika nafasi ya uwajibikaji, kama uko kwenye eneo lako na jambo limetokea la aibu siyo kwa sababu wewe umelifanya ni kwa sababu wewe ni mzalendo unasema kwa aibu hiyo mimi naondoka. Turudi kwenye uwajibikaji. *(Makofi)*

Katika utendaji pia ni lazima tufanye vitu kwa usahihi ukikosea huwezi kuwa na kisingizio kwamba aah! Ilikuwa ni bahati mbaya nilifikiria, katika utendaji nilioufahamu na akina Mheshimiwa Galinoma hubabaishi ni lazima upime na ukiamua umeamua sahihi. Hivi Rais kama angekuwa mbabaishaji ana uwezo wa kuweka sahihi mtu ahukumiwe kunyongwa, hivi akibabaisha wakisha mnyonga huyo mtu ndiyo atamfufua?

Kwa hiyo, katika kazi ni kama madaktari, madaktari wangebabaisha *operation* wangapi wangekufa? Hawababaishi, mwendesha ndege akababaisha akaondoa ndege bila mlango kufunga halafu akasema ilikuwa bahati mbaya nilipitiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, una *professionalism* lazima tuirudishe kama tunataka kuyatekeleza haya Rais anayoyataka, *professionalism* mwalimu awe mwalimu, Jaji awe Jaji, Polisi awe Polisi, mkulima awe mkulima lakini sasa tunavichanganya na hiyo ndiyo *point* yangu ya pili katika utendaji, tujipange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi huwezi kutambua Mkuu wa Wilaya ni yupi, kwa sababu kila mtu anahutubia, tulioomba kuhutubia ni sisi Wabunge na tumeomba kwa jasho. Kwa hiyo, wengine kama *DED,* huna ruhusa ya kuhutubia UKIMWI, una kazi ya kutekeleza. Kama wewe ni *DO* unasimamia shule mpango wa *MMEM,* usihutubie ubora wa *MMEM,* kazi yako ni kuhakikisha madarasa yamejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uchanganyaji wa mambo na majukumu ndio unatupa matatizo, mwanasiasa anakuwa mtaalam, mtaalam anakuwa mwanasiasa, inakuwa mchanganyiko. Kwa hiyo, katika kufanya hivi Mheshimiwa Rais labda atusaidie pamoja na Mawaziri kuhakikisha watu wote wamejipanga katika sehemu zao, wanasiasa ni wanasiasa, wanataaluma ni wanataaluma na utawala ni utawala. Kuna kitu kinaitwa *Administration,* una *administer,* sio tena wewe unaanza kuomba tafadhali, *you are administering.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka hapo, mimi ningeomba pia tutofautishe katika maagizo na maombi. Siku hizi maombi nayo ni maagizo, agizo likishaagizwa ni la kutekelezwa.Tunababaishwa huko Wilayani, unakuta mtu kaagizwa kuleta taarifa Makao Makuu haleti na bado ni *DED.* Kwa hiyo, ndugu zangu ubabaishaji huo tuuache na tuondokane wahamasishaji tutakuwepo sisi, lakini pia msitutwishe mzigo wa utekelezaji kwa sababu naanza kuona hatari ya wale ambao wamepewa dhamana ya utekelezaji

wanamrudishia Mbunge. Wewe umepewa dhamana mpaka unapewa na *OC,* mambo yakiharibika na Mbunge naye yupo katika kikao cha *Council.* Mimi kwani nimepewa *OC* ya kusimamia kilimo? Wewe ndio unapaswa kusimamia, kwanza umesoma na pili wewe umepata *OC* inayokuwezesha kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu ningependa kusema kwamba, ninayo mifano ya utekelezaji mbaya. Nchi hii imekwenda kwenye Mkataba wa *East Africa* unaolinda Ziwa Victoria, watu wanatekeleza vibaya sana, kazi yao ni kufukuzana na wavuvi ili wapate hongo, badala ya kukaa na wavuvi wakawasaidia kupata nyenzo na vifaa vinavyofaa, kazi yao ni kuwafukuza na mabunduki kwa kushirikiana na Polisi na Maliasili na ipo mifano mingi katika Wilaya nyingi ambazo agizo linapotoka badala ya kulitafsiri katika njia iliyo sahihi, wanakaa kufukuzana na wananchi na kuwabugudhi wananchi. Bunge hili la 2005-2010 hivyo vitu lazima tuviache kwa sababu vinavunja haki za binadamu. Lazima maagizo yakitoka iwe uwezo wa mtu yule kubaki kwenye madaraka ni uwezo wa kutafsiri maagizo hayo katika vitendo vilivyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Rais aendelee hivyo hivyo. Tusiposema hivyo sisi Wabunge watasema ni moto wa kifuu. Rais Jakaya Kikwete aendelee na kazi hiyo hiyo. Yule ambaye hawezi kwenda kwa mwendo wa kiongozi wake akibaki nyuma mwingine ana-*take over,* tangu kwa watendaji wa Vijijini, Wilayani, Mikoani na Taifani. Tunaomba Rais Jakaya Kikwete aendelee kwa moto ule ule na tusiuzime haraka maana tuna tabia ya kusema Rais naye kazidi, hapa mbona kafanya hivi, ahaa, tuache kwanza moto ubabue watu halafu ndio tutajua baadaye na humo humo ndio tutakuwa na sisi tunaongeza mioto tunapokuwa huko Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na naunga mkono hoja na haya yakitekelezwa nitashukuru sana hasa kwa kuanzia Wilayani kwangu. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kurudi tena kwenye Bunge hili, lakini naomba nianze kuwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Mvomero walionipa ridhaa yao ya kuja kuwawakilisha humu Bungeni na mimi naahidi kutekeleza yale yote niliyowaahidi wakati wa kampeni. Naomba Mwenyezi Mungu anipe uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukupongeza wewe na Spika kwa kuchaguliwa katika nafasi hii. Lakini pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba yake nzuri, makini, hotuba ambayo imetupa dira sisi Wabunge na hotuba ambayo tayari tuna maeneo ya kuyafanyia kazi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa uwezo Rais wetu, aendelee kutekeleza ahadi zake na aendelee kutekeleza ahadi zake zote kama alivyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa kuwa ndani ya Bunge hili na naomba tushirikiane kwa faida ya wananchi wetu. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa

Waziri Mkuu na niwapongeze sana Mawaziri na Manaibu wote pamoja na Wenyeviti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango mdogo na naomba nianze na kilimo. Kabla sijaanza naomba niseme naunga mkono hoja iliyo mbele yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro ni Mkoa uliojaaliwa, ni Mkoa wenye Mito mingi, una rutuba, wenye ardhi nzuri. Serikali bado haijawa makini katika kuendeleza kilimo katika Mkoa wa Morogoro. Kutokana na maji mengi na Mito mingi iliyopo katika Mkoa wa Morogoro, nina hakika kama Serikali itawekeza katika Mkoa wa Morogoro basi Mkoa wa Morogoro una uwezo wa kulisha Mikoa mingine zaidi ya mitano. Kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Morogoro bado hakijapewa kipaumbele. Yapo maeneo kilimo cha umwagiliaji kinasuasua na yapo maeneo kilimo cha umwagiliaji kinahitaji kazi ya ziada. Mimi niiombe Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika baada ya tatizo hili la njaa na ukame sasa Wizara ije Morogoro, sisi kama Wabunge wa Mkoa wa Morogoro tukae, tuwaeleze wataalam wa Wizara maeneo yapi wanaweza kuwekeza na Wizara itaona matunda mazuri ya Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mvomero tuna mabonde matatu ya umwagiliaji, Bonde la Mkindo, Bonde la Dakawa na Bonde la Mlali. Haya mabonde yote matatu yanaendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kusuasua. Naomba Wizara ya Kilimo kutokana na kauli ya jana ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwamba atatembelea Mikoa yote mimi ningeshauri aanze na Morogoro na aanze na Wilaya ya Mvomero kwa kuwa tupo jirani na Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam. Ningeshauri Serikali iwe makini sana na katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia na hili ni eneo ambalo lina sura ya kiuchumi ya Kitaifa katika kilimo. Sasa hivi tunazungumzia sana suala la kilimo ambacho kitatuletea mapato ya nje. Lipo zao ambalo Serikali ikiwekeza tutaona faida yake kwa zaidi ya miaka thelathini. Zao hili ni raba, raba ambayo inazalishwa kwa ajili ya kutengeneza matairi ya magari, ambayo inaingiza fedha za kigeni, raba ambayo miti yake ni sehemu ya utunzaji wa mazingira na raba ambayo itatoa ajira. Hili zao la raba katika nchi yetu linastawi katika Mikoa ifuatayo:-

Mikoa ya Arusha, Morogoro, Tanga na Zanzibar. Nashauri Serikali ya Awamu ya Nne iwekeze katika zao la raba. Raba inastawi na inaanza kuzaa baada ya miaka mitatu na mitano, lakini mazao yake huvunwa kwa zaidi ya miaka thelathini. Raba ile inatumika sana kutokana na dunia ya sasa kubadilika na mahitaji ya matairi yamekuwa mengi, raba inaletwa Tanzania pale *General Tyre* kutoka nje ya nchi, kutoka Malaysia, *Latin America* na nchi nyingine. Kwa kuwa mahitaji ya raba yamekuwa ni makubwa na kila siku tunazungumzia fedha za kigeni au kuinua uchumi, naomba sasa tubadilike, tuingie katika uchumi utakaotuingizia fedha za kigeni na uchumi ambao utahifadhi mazingira katika eneo hili la kilimo na ajira kama nilivyosema awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa yote niliyotaja sasa hivi raba inazalishwa Zanzibar tu na Tanga kidogo, lakini Morogoro yapo maeneo ambayo wataalam waliyaainisha wakasema raba inaweza kuzalishwa. Ningeomba wataalam wa Wizara ya

Kilimo, Chakula na Ushirika waliangalie hili kwa makini na itakuwa ni faida ya baadaye. Naiomba Serikali ilifanyie kazi hilo kama ni sehemu ya kilimo katika uchumi wa Taifa utakaoingiza fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la Chuo Kikuu cha Mzumbe kilichopo katika Wilaya ya Mvomero, wanafunzi zaidi ya 2,500 waliomba mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kati ya hao waliopata mikopo ni 1,800 na wanafunzi walioomba mikopo waliomba kati ya fedha za Tanzania shilingi 750,000/= na shilingi 1,000,000/= lakini fedha iliyotolewa pale na Bodi hiyo ni shilingi 500,000/= na wanafunzi walioomba mikopo hiyo walikuwa wale wa *private* na wale wa *under government sponsorship.* Tatizo ambalo limejitokeza na mgogoro uliopo Chuo Kikuu cha Mzumbe ni kwamba wanafunzi wamepata mikopo kwa kiwango cha chini na hakuna ufafanuzi uliotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge hili kuiomba Wizara husika ituletee wajumbe wa Bodi ya Mikopo pale Mzumbe waje wafanye kikao, watoe ufafanuzi juu ya tatizo lililopo sasa hivi ili tuepushe migogoro katika vyuo vikuu. Suala hili limezungumzwa jana katika kipindi cha Maswali na Majibu, majibu yametolewa lakini bado naiomba Serikali, jana nilijaribu kusimama kuuliza swali la nyongeza, kutokana na muda sikupata nafasi, kwa hiyo, nimeona ni vema nilitoe hapa leo kwamba naiomba Serikali iagize Bodi ya Mikopo ifike Chuo Kikuu cha Mzumbe, tukae, tuwaeleze ya kwetu na Bodi itoe ufafanuzi ili migogoro isiwepo katika vyuo Vikuu vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie katika eneo la barabara. Barabara ya kutoka Korogwe-Handeni-Turiani-Mvomero hadi Magole ni barabara iliyokuwa ikipitika miaka ya nyuma. Katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005, barabara hiyo imeainishwa kwamba itawekwa lami. Mgombea Urais kwa tiketi ya CCM alifika Turiani tarehe 6 Septemba, 2005 wakati wa kampeni, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi iwapo ataingia Ikulu barabara ile itawekwa katika mipango ya kuwekwa lami. Nimeona ni vema nilikumbushe hili katika Bunge hili la kwanza ili mipango ya awali ianze na utekelezaji wake uanze mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la barabara za Mikoa. *TANROADS* wanasimamia barabara za Mikoa. Katika Jimbo langu la Mvomero barabara za Mikoa zipo nne, lakini barabara moja imesahauliwa kwa miaka zaidi ya saba. Hili nimelizungumza ndani ya Bunge hili, ahadi zimetolewa mara kwa mara. Barabara hii ni barabara ya kutoka Mvomero kwenda Maskati - Kibati yenye urefu wa kilometa 80, ni barabara ya Mkoa chini ya *TANROADS.* Naiomba Wizara kupitia kwa Mheshimiwa Basil Mramba, barabara hii ipewe kipaumbele, ni barabara ya Mkoa iko chini ya *TANROADS,* inapita kwenye Vijiji zaidi ya ishirini na inaunganisha Kata nne. Kwa hiyo, naiomba Serikali iipe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ni kipindi cha ukame, jana tumezungumza mambo mengi kuhusu chakula, njaa na kadhalika. Lipo suala nataka kuitahadharisha Serikali ambalo halihusiani na chakula lakini ni sehemu ya chakula, suala hilo ni sukari. Viwanda vya Sukari nchini vimemaliza msimu wa uzalishaji, hakuna sukari

inayozalishwa kuanzia mwezi Februari hadi mwezi Mei au Juni, upungufu au uhaba wa sukari nchini umeanza kuonekana. Desemba kilo moja ya sukari ilikuwa shilingi 600/=, sasa hivi imeshafika shilingi 900/= na wakati wowote itafika zaidi ya shilingi 1,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ianze mkakati mapema wa kuliangalia suala hili. Kuna upungufu wa tani zaidi ya 50,000 za sukari katika nchi yetu. Mimi kama mdau, kama mkulima wa miwa na kama Mbunge ninayetoka kwenye eneo tunakozalisha sukari nimeona ni vema niliseme hili, tuna upungufu wa sukari katika nchi yetu wa zaidi ya tani 50,000. Serikali iliangalie hilo kama inavyoangalia mazao mengine. Upungufu huu utasababisha bei ya sukari kupanda sana na hili limeanza kuonekana. Naiomba Serikali ilifanyie kazi suala la sukari na mimi kama mdau nina maoni yangu mawili, matatu katika hilo, kwa sababu muda hautoshi siwezi kuyasema yote hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu la mwisho, tunajenga sekondari za Kata tena kwa kasi mpya. Tunaomba fedha za *MMES* ziwahi kufika katika Majimbo yetu. Naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iharakishe kupeleka fedha za *MMES* katika Halmashauri zetu, fedha zile zianze kutumika mapema, tumeshakamilisha vigezo mbalimbali, tumeshafikia hatua ya kupeleka maombi. Wizara imesema fedha zile zitatoka mapema. Januari imekwisha, Februari ndiyo hiyo, naomba Wizara iharakishe kupeleka fedha za *MMES* ili lengo letu la kufungua sekondari mpya likamilike katika Majimbo yetu. Wilaya ya Mvomero, kwa Jimbo la Mvomero mwaka 2005 tumefungua sekondari mpya tano za Kata na mwaka 2006 tuna mpango wa kufungua sekondari sita mpya za Kata, tunaomba Wizara kwa maombi yetu ya *MMES* watuwahishie ili fedha zile zifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona muda umekwenda, kwa hiyo, nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ambayo imetokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kabla sijachangia hoja, kwanza ningependa nimpongeze Rais wetu kwa kuchaguliwa na wananchi wa Tanzania kwa kura nyingi.

Lakini pia pamoja na kuchaguliwa kwa kura nyingi Rais huyu kwa jinsi wananchi wa Tanzania walivyokuwa na imani naye angeweza kupita bila kufanya kampeni. Kupendwa kwake huko pia kumesaidia hata sisi Wabunge wa Bunge hili kuweza kupita kwa kura za vishindo na hiyo ilitokana na juhudi zake ambazo mahali alipoona palikuwa na ugumu alikuwa anakwenda hata mara mbili au tatu angalau kuweka hali nzuri. Kwa hiyo naomba tumshukuru kwa hilo kiasi cha kufanya Chama cha Mapinduzi kipate ushindi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi lakini pia napenda nimpongeze Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu na kura

nyingi na jambo ambalo kwa kipindi ambacho nimekaa hapa Bungeni kwa huu muda mfupi nimeona ni kwamba Spika na Naibu Spika kwa utendaji wenu naona kama vile mnatulea ingawaje sisi wote ni watu wazima. Kwa hiyo naomba nitoe shukrani za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa niwapongeze Wabunge waliochaguliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri, lakini pia ningependa niwapongeze Wabunge wenzangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini hasa hasa ningependa pia niwapongeze wale wananchi wa Jimbo la Morogoro Mjini ambao wamenipa kura nyingi za kuniwezesha kuja hapa Bungeni na leo hii nikapata nguvu ya kusimama hapa ili kuweza kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja ningependa kusema kwamba mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na hotuba hii ya Rais haina kasoro yoyote. Sisi tuliosimama kuchangia tunachangia tu ili kuweza kuweka msisitizo kwa wale watendaji ambao watatekeleza haya maagizo ya Mheshimiwa Rais lakini hotuba ni nzuri haina kasoro yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningeomba sasa niende katika jambo la msingi ambalo limenifanya nisimame hapa. Katika hotuba ya Rais ukurasa wa 14, Mheshimiwa Rais alizungumzia suala linalohusiana na masuala ya afya kwa maana ya maadui wetu wakuu watatu ambao ni maradhi, ujinga na umaskini.

Sasa mimi nilikuwa naomba nizame kidogo katika suala la maradhi. Watendaji wakuu au askari ambao wanapambana na suala la maradhi ni watendaji wa Wizara ya Afya ambao ni waganga, wauguzi pamoja na mabwana afya. Sasa watu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa maana kwamba kipato chao kwanza ni kidogo, lakini pia vitendea kazi ni duni na havitoshi. Pia na nyenzo nyingine za kufanyia kazi katika hospitali kwa mfano umeme ambao sio stable pamoja na wakati mwingine ukosefu wa maji kunachangia kutotoa huduma nzuri katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hawa wafanyakazi wa hospitalini kwa maana ya waganga, wauguzi na mabwana afya kwanza mishahara yao haitoshi. Lakini pamoja na mishahara kuwa haitoshi ni kwamba wao wameondolewa marupurupu yote ambayo zamani kabisa walikuwa wanayapata kwa mfano, *risk allowance, extra duty allowance* na *allowance* nyingine ambazo zingeweza kukidhi haja ukiondoa suala la mshahara kuwa mdogo. Hali hii ilikuja kubadilishwa miaka michache iliyopita kwa kusema kwamba hizi pesa zinaingizwa kwenye mishahara yao, lakini utakuta kwamba hakuna chochote kilichofanyika, ni kama vile mishahara yao imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapunguzia hizo *allowance,* utakuta mtu alikuwa anapata pengine mshahara shilingi 100,000/= pamoja na marupurupu, baada ya kuyaondoa marupurupu hayo unakuta sasa anapata chini ya laki moja, kitu ambacho katika mapato yake ya kila mwezi kimempunguzia hela ya kumwezesha kuendesha

maisha yake pamoja na familia. Kwa hiyo, wafanyakazi hawa wamekuwa hawana uhakika wa maisha yao kutokana na kipato chao kuwa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nataka kuzungumzia ni kwamba bahati nzuri katika hotuba ya Rais ametwambia kwamba amepokea Awamu ya Tatu ikiwa nchi yetu haina madeni na uchumi umeongezeka. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba wafanyakazi hawa wa afya warudishiwe marupurupu yao kama *risk allowance* na *extra duty allowance* kwa sababu zifuatazo:-

Mtumishi wa afya anafanya kazi katika hatari ya maisha yake hasa kwa magonjwa ya kuambukiza kwa mfano *hepatitis,* UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa ya ngozi kama fangasi na magonjwa mengine ya kuambukiza. Sasa utakuta kipindi wakati *risk allowance* ilipokuwa imeondolewa ugonjwa, kama wa UKIMWI wakati huo ndio ulikuwa haujajitokeza, lakini kwa sasa hivi ugonjwa kama wa UKIMWI kwa daktari au muuguzi kuupata kwake ni jambo la kawaida kwa sababu shughuli zake za kila siku anagusana na damu za wagonjwa na mambo mengine ambayo yanaweza kumsababisha akapata UKIMWI ingawa watu wanafikiri mtu kupata UKIMWI ni lazima afanye tendo la ngono, kumbe si kweli, kwa mfanyakazi wa Wizara ya Afya anaweza
kupata matatizo haya kutokana na *professional* yake ya kazi. Sasa nilikuwa nafikiri kwamba jambo hili liangaliwe kwa makini ili wafanyakazi hawa waweze kupata moyo waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa hatari ya magonjwa wafanyakazi hawa wanazo hatari nyingi. Hatari mojawapo ni pamoja na kuumizwa na wagonjwa ambao kwa bahati mbaya huenda wakarukwa na akili kama wagonjwa wa akili au wagonjwa wanaopata *cerebral malaria* na kadhalika, tunao wafanyakazi wengi ambao wamepigwa na wagonjwa na baadaye hawakupata hata mafao ya kuwasaidia katika muda wao uliobaki wa kazi. Lakini pia kama nilivyosema ni kwamba nikizungumzia suala la *extra duty allowance* katika utaratibu wa Serikali unasema kwamba atalipwa mtumishi pale ambapo mwajiri wake atakapokuwa amemtuma kazi ya ziada baada ya masaa ya kazi lakini kwa daktari hilo ni gumu kwa sababu daktari *let say,* yeye anatakiwa atoke saa tisa na nusu lakini akipata wagonjwa wa dharura labda watatu au wanne wa kufanyiwa *operation* hawezi kusema kwamba naondoka nyumbani kwa sababu muda wangu umekwisha ni lazima aendelee na *operation.*

Kwa hiyo, suala la *extra duty allowance* kwa daktari ni suala ambalo ni jukumu lake la kila siku kutokana na maadili ya kazi yake vinginevyo asipotelekeza atakuwa amevunja maadili ya kazi yake na ana haki ya kufukuzwa kazi.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili litiliwe uzito unaostahili ili waweze kupata mafao yao. Lakini pia kuna kero katika Wizara ya Afya, kero hii ipo katika masuala ya Bajeti, wakati wa Bajeti wakuu wa Hospitali za Mikoa au Wilaya wanapotengeneza Bajeti zao kuzipeleka kwa Makatibu Tawala aidha wa Wilaya au Mkoa mara nyingi Bajeti hizo zilikuwa zikipunguzwa kwa kuonekana kwamba labda pesa hazitoshi na hii ndio inachangia kufanya kwamba Wizara ya Afya au watendaji wa Wizara ya Afya

wakashindwa kufanya kazi zao vizuri kwa sababu mahitaji au vitendea kazi ambavyo vingeweza kuwasaidia haviwezi kupatikana kutokana na uhaba wa pesa.

Kwa hiyo, naomba kushauri katika Bunge hili Tukufu, ikiwezekana Bajeti ya mwaka huu tuipitishe bila kikwazo ili Wizara hii iweze kupata hela za kutosha kwa ajili ya wafanyakazi wa Afya ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri na wao wenyewe waweze kupata marupurupu yao wanayostahili kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la Wizara ya Afya, naomba nizungumzie suala la usalama wa raia. Pamoja na malalamiko mengi ambayo yanaliendea sana Jeshi la Polisi lakini mimi binafsi ningependa kupongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanazozifanya ukiondoa watumishi wachache ambao sio waaminifu. Jeshi la Polisi limefanya kazi nzuri, limeweza kukamata silaha katika Mikoa mingi tu ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro na Mikoa mingine.

Wakati mwingine kuwakamata majambazi wa hatari ambao ukikutana nao uso kwa uso wanaweza kukuua na tumeshapata taarifa kwamba hata askari wamekufa kwa sababu ya kupambana na majambazi. Kwa hiyo, wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu kwa sababu hawana vifaa vya kutosha, hawana magari ya kutosha na vifaa vya mawasiliano vya kutosha. Kwa hiyo, ningependa niwapongeze katika hili. *(Makofi)*

Lakini pongezi zangu naomba niwapongeze pale waliposimamia utulivu wakati wa mchakato mzima wa Kampeni ya Uchaguzi na hata siku ya kupiga kura. Kama sio Jeshi la Polisi pengine idadi hii ya Wabunge waliokuwemo katika Bunge hili wasingepatikana au tusingeweza kushinda kwa kura za vishindo kwa sababu baadhi ya vyama vilishaanza kupanga mipango ya vurugu ili kuwatisha wananchi wasiweze kwenda kupiga kura. Jeshi la Polisi lilisimama kidete sisi wenyewe ni mashahidi, kule Zanzibar tumeona kwenye *Television* jinsi gani Jeshi la Polisi lilivyofanya kazi yake. Kwa hiyo, ningeomba tuwapongeze na tuwape moyo na kuiomba Serikali iwaongezee Bajeti ili waweze angalau kupata vifaa vya kuwasaidia katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la mwisho, ninayo mengi kwa sababu muda hautoshi. Suala hili nazungumzia katika masuala ya miundombinu. Pale kwenye jimbo langu Morogoro ni kwamba Mji wa Morogoro umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu mbili hizi upande wa kushoto na upande wa kulia, lakini kiunganisho chetu ni daraja la Mto wa Morogoro. Daraja hili bahati nzuri upande wa kushoto wa daraja ndiko ilipo Mahakama, Hospitali ya Mkoa na Idara nyingine muhimu na upande mwingine wa kulia wa Mji ndiko walikokuweko wananchi wengi wa Manispaa ya Morogoro. Kwa hiyo, wananchi wa Morogoro waliokuwa wengi upande wa kulia wanalazimika kwenda kushoto kwa ajili ya kwenda kupata huduma hospitalini na hasa ukizingatia Morogoro hatuna Hospitali ya Wilaya tunayo Hospitali ya Mkoa tu ambayo ni hospitali moja ambayo ndiyo wananchi wote wa Morogoro wanaitegemea hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba kiunganisho chetu cha daraja hili, daraja hili tayari limeshakuwa bovu lime-*crack* kutokana na masika

yaliyopita miaka michache. Hili la kwanza. Lakini pia Morogoro sasa hivi kuna ongezeko la magari na wananchi pia wameongezeka. Kwa hiyo, kuna msongamano mkubwa sana wa magari ambao wote wanategemea kuvuka katika daraja hili moja. Sasa wakati umefika angalau tutengeneze daraja lingine kwa sababu ya kuondoa kero hizo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri wa Miundombinu aweze kuliangalia hili ili aweze kutuokoa wananchi wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu pamoja na wewe kuwa Naibu Spika. Tunawatakieni kila la kheri. *(Makofi)*

Vile vile naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wetu kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi yetu katika Awamu ya Nne na vile vile kwa namna alivyoanza kazi vizuri. Wote tunaona tunashuhudia kama ameanza kazi vizuri. Mimi wakati ule wa uchaguzi niliuliza swali, mwananchi mmoja aliuliza swali akasema Bwana Mzindakaya hebu tupe tafsiri ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Nikasema ichague CCM ndiyo utapata majibu hayo. Kweli huyu raia amenipigia simu akasema ameona kweli kwamba ni ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Sasa katika hiyo hiyo mimi nataka kutoa maelezo kidogo. Nakubaliana na dada yangu Mheshimiwa Getrude Mongella, lakini mimi nisingewashauri Wabunge mkakubali Serikali kwenda *speed* halafu Wabunge tubaki nyuma, itakuwa kosa kubwa sana. Kwa sababu baadaye watu watagundua kwamba hakuna haja ya kuwa na Mbunge kama Serikali itafanya kila kitu. Ninyi ndio mko karibu na wananchi. Mtakuwa mnajua matatizo mengi zaidi kuliko Serikali yenyewe. Kwa hiyo lazima twende *speed* moja ama sivyo ikiwezekana tuwatangulie, msikubali Serikali kututangulia, mtapata shida. Maana uwezo wa kujua mambo mnao mkubwa sana Waheshimiwa Wabunge. Mimi nashauri twende pamoja kwa *speed* hii hii kwa sababu na kule tunapokwenda tumetumia wote *slogan* hiyo hiyo sasa haiwezekani Rais akaenda *speed* kali, Wabunge tukabaki nyuma. Lazima tumsaidie na Mawaziri waende vile anavyokwenda, huo ndio ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo fulani ambayo ningependa niyaseme kabla na mimi nitasemea kilimo tu sitasema mambo mengine mengi. Lakini nataka niseme jambo moja kwamba tuliposamehewa madeni kila mwezi tulikuwa tunalipa kama nitakosea naomba Wizara ya Fedha wanisahihishe kwa kila mwezi tulikuwa tunalipa madeni ya nje dola milioni 5 kila mwezi. Sasa tangu tuliposamehewa madeni fedha hizo bila shaka imekuwa ni pato kwa Serikali.

Kwa hiyo, napenda tupate maelezo hizi fedha kwa sababu tulishapitisha Bajeti na sasa hii Bajeti hizo fedha ni ziada, ningependa tupate maelezo hasa kama hivyo ndivyo

zinatumika kwa namna gani maana hatujaletewa Bajeti ya nyongeza ili tukubaliane namna ya kuzitumia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vile vile liko jambo limejitokeza hapa nchini, nalo ni kosa tu, ni unyonyaji. Wafanyabiashara wengi Dar es Salaam sasa wanauza vitu vyao kwa kutumia dola. Mimi ninao ushahidi nimekuja na makaratasi. Mtu akifika kwenye duka wanamtoza kwa dola ambapo sio kweli biashara ya ndani ya nchi yetu lazima iwe kwa *Tanzania shillings,* haiwezi kuwa kwa dola na huu ni wizi wa wazi wazi. Sasa mimi naomba Serikali ifuatilie jambo hili kwa sababu wananchi wanaanza kudhulumiwa. Maana kama kwa mfano mtu aliagiza vitu kutoka nje kwa dola lakini alitumia fedha za Tanzania kununua dola. Sasa ikiwa yeye ananunua vitu kwa *rate* ya shilingi 1,100 miezi sita au saba iliyopita. Kama dola zimeongezeka thamani huyu mwananchi ananyonywa ni wizi wa wazi wazi kibiashara, kwa hiyo, mimi naomba Serikali ichunguze jambo hilo.

Sasa baada ya hayo ningependa nizungumzie jambo moja tu la kilimo lakini kabla jambo hilo la kilimo naomba niishukuru Serikali.

Kwanza naomba na mimi mwenyewe niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kwela kwa kunichagua kuwa Mbunge. Nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu mkubwa sana. Sasa mwaka 2001 Rais wetu wa Awamu ya Tatu alipotembelea jimboni kwetu aliahidi wananchi kwamba watatengenezewa barabara ya kutoka Mnyangarua kwenda mpaka Kilimatinde, barabara hiyo haijatengenezwa mpaka sasa. Mimi nashukuru Mwenyezi Mungu kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ni ya CCM kwa hiyo naomba ahadi ya Rais itekelezwe kwa sababu mwaka jana tulijibiwa kwamba tumecheleweshwa kuleta kwenye Bajeti, nina hakika safari hii itawahi kuwekwa kwenye Bajeti na kila mara tunapokwenda sisi watu wanaposema Rais aliahidi unaona aibu. Sasa hakuna Rais wa nchi yoyote duniani anayetamka jambo halafu lisiwe, hii ni kasoro kubwa sana katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niishukuru Serikali pia kwamba kwenye Jimbo letu Bonde la Rukwa linategemewa sana, hatuna barabara nzuri lakini naishukuru Serikali kwamba imepata msaada kutoka Denmark na wanatengeneza barabara kutoka Kilimatinde mpaka Muze. Sasa mimi naomba pia Serikali watueleze utekelezaji umefikia wapi. Maana uzuri wa bahati kwamba barabara hii itatuunganisha na wenzetu wa Mbozi kutoka Mloo mpaka daraja la Mto Momba. Hilo ninaomba nishukuru maana vile vile kushukuru ni ustaarabu.

Baada ya hayo naomba niseme jambo moja ambalo hatuwezi kukubaliana sana upande wa Serikali. Ni hivi hii njaa ambayo jana Wabunge mmechukua saa nzima au saa mbili kubishana humu juu ya njaa tunaitafuta wenyewe. Hii njaa ni yetu tunaitafuta wenyewe. Wala hakuna haja ya kulalamika kwamba nchi ni jangwa hapa. Tanzania haijapata kuwa jangwa. Ikitokea hakuna mvua basi hakuna mvua lakini kuna nchi ambazo tangu Mungu ameumba hazijapata kuona mvua, Misri ni mojawapo. Misri ni nchi ambayo wanatumia Mto Nile. Juzi nilikuwa na Balozi wa Egypt akawa ananieleza mipango yao ya namna ya kubadilisha jangwa kuwa ardhi ya kulima. Tuliwahi sisi kwenda Misri, Tanzania tukaenda kuomba wataalamu wa Misri kuja kutusaidia na kuendeleza umwagiliaji maji. Nchi yenye Mito na Maziwa tumekwenda kuwaomba watu

wa jangwani kuja kutufundisha namna ya kutengeneza umwagiliaji maji. Nasikia walikuwa katika mkoa mmoja siku moja, mvua imenyesha wakasikia radi ngumu, mtaalamu mmoja akaandika barua akasema hapana kama mimi nimekuja kufanya kazi katika nchi ambayo radi zinaunguruma kama umeme naomba mimi niondoke niende kwetu. Sasa tunacholia ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwa nini tunalia. Kwa sababu gani Tanzania yote mimi nilishakuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Ukitoka Dar es Salaam unapita Rufiji unakwenda mpaka Minepa mpaka wapi kupita Milima ya Udzungwa ardhi yote hiyo ukiiona na majani yanayoota ni mpunga tu, ndiyo. Mwalimu Nyerere wakati wa uhai wake alitengeneza ile reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Zambia na ikatengenezwa *paper* mradi unaitwa *Uhuru Corridor*. Ile reli ilitengenezwa kwa ajili ya kutusaidia kubeba mazao ya kulisha Dar es Salaam ndiyo ilikuwa nia. Leo ukifika kule hakuna kitu ni majani tu. Mvua inanyesha inakwenda yenyewe. Sasa nani anasema hii nchi ina tatizo. Tatizo ni sisi wenyewe. Kwa sababu kila mtu ni mhutubiaji wa kilimo. Kilimo hakiwezi kwenda kwa hotuba, haiwezekani. Nani amepata kuhutubia mahindi ohoo, yakaota, yataotaje kwa hotuba. *(Makofi)*

Lazima tupange na tupange kwa kuchagua, mimi naishauri Serikali. Mwaka juzi tulipopata njaa kama hii Wabunge tuliomba. Mimi niliomba hapa Waziri Mkuu akakubali, Wabunge wote tukasema lazima tupewe siku mbili kutafuta mbinu ya kujitoa hapa. Hatukukutana, wakatupuuza. Leo mambo yamerudi pale pale. Kilimo ninachoshauri mimi Serikali hii inajua mikoa ambayo tayari inapata mvua kila mwaka hakuna ukame, kwa nini hatuendi huko kwenda kupanga mipango na kulima na programu za utekelezaji.

Kwa hiyo, mimi shamba langu ninalolima silimi kwa hotuba. Hivi ninavyozungumza mke wangu alikuwa anakuja hapa amefika pale na kuruhusu kwenda kuanza kupanda ngano kwa sababu ni tarehe ya kupanda sasa. Kwa hiyo, lazima tuwe na mipango, Mikoa ichaguliwe. Mkuu wa Mkoa, Ma-*DC* na wenzake wote ninyi mnapewa malengo mlime tani kadhaa hapana kusema eka. Msiwaambie watu kulima eka waambieni tunataka tani kadhaa watajua wenyewe eka moja inatoa gunia ngapi.

Kwa hiyo, mipango isiyo na programu ya utekelezaji ni kupoteza muda tu. Pili, tujue zana gani tunayotumia. Waheshimiwa Wabunge nani atakataa, Rais mwenyewe mtu mwaminifu amekubali kwamba kilimo cha Tanzania ndiyo kilimo kinacholimwa kwa jembe la babu na babu. Wajapan hivi tunavyozungumza wana ziada ya chakula ya miaka saba. Japan hakuna mkulima mwenye eka mia, mimi nimefika. Wakulima wa Japan eka 5, 10 mwisho 20. Lakini *modernization* ya zana za kufanyia kazi wanavuna *minimum* gunia 32 kwa eka.

Mimi nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wale wananchi wa Morogoro wanajua nilikuwa nalima pale Dakawa kulikuwa na *irrigation Kafa,* ikafa ile. Nilikuwa napata gunia 42 kwa eka. Kwa sababu mimi ni kiongozi wa Mkoa lazima nionyeshe njia.

Kwa hiyo, mimi nasema nimeamua niseme jambo hili moja tu la kilimo. *Inflation* imetokea hapa kutokana na upungufu wa chakula, takwimu za Benki Kuu ziko hapa

nilikuwa nazisoma lakini pia inaonyesha kwamba baadhi ya mazao yamezidi kushuka chini kwa mfano korosho. Korosho ni zao ambalo wananchi wa Kusini walikazana likapanda sana. Sasa korosho imeshuka chini kabisa kwa takwimu zilizo hapa kwa mfano tulishafika mwaka uliopita korosho tani 96 ziliuzwa sasa tumeuza tani 34,000 inatisha, hivi hasa mnaohusika mkishajua takwimu hizi ni za Benki Kuu hivi tukizisoma tunasemaje, tunanyamaza tu hatuulizi kwa nini imetokea. Benki wameeleza matatizo na mojawapo ni *pricing*. *Pricing* kasoro yake ni hivi Tanzania hii hakuna mkulima hata mmoja anayejua bei ya kulima kahawa, korosho hata kulima mahindi. Serikali yenyewe haijui.

Kwa hiyo, mkulima wa Tanzania bei yoyote anayopewa ni sawa tu maana hata Serikali haijui gharama ya kuzalisha. Sasa kitu cha kwanza ambacho Serikali ikazane ni kujua *production cost* ya kila zao kwa mkulima ili *input* hii inayosema ijulikane gharama yake. Wakulima hawa tunaposema bei ya korosho nzuri mnalinganisha na *production cost* gani ambayo nyinyi Serikali mnajua mmeifanya. Na kazi ingefanyika kule kule Wilayani maana tuna wasomi, kwa hiyo hakuna anayejua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania naomba tuite mkutano wa Wakuu wa Wilaya na Mkoa tuulize ni Mkuu wa Mkoa gani na Bwana Shamba wake wanaowajua wakulima kwa majina. Maana zamani wakati wa mkoloni Bwana Shamba anatembea na orodha ya wakulima na atawatembelea kwa majina na atarekodi *performance* ya kila mkulima leo nani afanye hivyo. Hata Wakuu wa Mikoa wanahutubia mlime wananchi hajui mkulima ni nani. Nani amechukua takwimu za Mkoa wake kusema huyu ni mkulima analima eka hizi anapata kiasi hiki. Hilo ndio tatizo la nchi yetu.

Kwa hiyo, naomba mwisho niseme naomba tutoke huko. Njaa hii tumeitafuta wenyewe kwa sababu Tanzania haina ukame. Pili, kutokana na *speed* ya Rais wetu mimi nashauri watu wahame kwenye maofisi twendeni tukaishi tufanye kazi vijijini na hii ndiyo kazi moja ya Wabunge. Mimi nawaomba Wabunge Mungu awajalieni, mtu asiwatengenishe na raia. Watu waliokuwa wanasaidia kuleta Mapinduzi katika maendeleo ni Wabunge na ushahidi tunao. Mashule yamejengwa Wabunge, zahanati zimejengwa Wabunge na Wabunge wengi mmekuwa mnatumia fedha yenu ya mfukoni kuleta maendeleo. Lakini badala ya watu fulani wenye akili kuchukua *data* na kuandika na kusifu juhudi zenu mnatukanwa tu hadharani. Sasa utu uko wapi, hivi Tanzania vyombo vyetu huwa havisifu, kusifu ni dhambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge tutembeleane Majimbo kwa Majimbo. Yako mambo ya kujifunza hapa hapa Tanzania wala huna haja ya kwenda Amerika. Watu wetu wa Serikali ninyi wote Wabunge ni mashahidi. Mawaziri, Makatibu Wakuu kwenda Ulaya ni karibu kuliko hata Sumbawanga.

Kwa hiyo, nchi hii mnaachiwa ninyi, Wabunge mhangaike na wananchi waliowachagua. Hawa hawa watakuja huko kwa sababu kwenda Amerika ni karibu kuliko kwenda Sumbawanga. Watu watakaokwenda kwa wananchi ni ninyi na mimi nawaombea Mwenyezi Mungu awajalieni awape afya njema na mtu anayewalaumu Wabunge anachuma dhambi kwa Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Nianze na mimi kwa kutoa pongezi mbalimbali. Nampongeza Rais wetu, Waziri Mkuu, Mawaziri, Mheshimiwa Spika wetu na wewe Naibu Spika pamoja na sisi Wabunge tujipongeze kwa sababu nikiacha Kambi ya Upinzani, sisi katika CCM tunafahamu kwamba yeyote aliyopo hapa amepita katika tanuri la moto. Kwa hiyo, tunayo haki kabisa ya kujipongeza. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa jimbo la Kalenga kwa kunichagua mimi kupitia CCM. Nawashukuru sana viongozi wa CCM katika Jimbo langu, Mkoa wangu na Wilaya yangu kwa jumla. Lakini niwashukuru zaidi wapiga kura katika jimbo hilo katika Kata zote 11 za Nzihi, Ulanda, Kalenga yenyewe, Kihwele, Mseke, Maboga, Wassa, Mgama, Lumuli, Ifunda na Magulilwa. Ninawaahidi wote kwamba nitafanya kadri nitakavyoweza kushirikiana nao katika maendeleo yao ili tuhakikishe kwamba itakapofika mwaka 2010 Chama chetu kiweze kushinda tena. Ninajua sasa hivi kuna ukame mkubwa umetuelemea, sio sisi tu ni nchi nzima. Kwa sasa Serikali inajua na inafanya kila linalowezekana kusaidia sehemu mbalimbali na nitakaporejea baada ya Bunge hili ninaahidi kwamba nitashirikiana nao katika kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu naomba niseme kwamba naunga mkono hotuba ya Rais wetu moja kwa moja. Mimi kama mnavyoniona huku juu nimekwishaota mvi. Nimefanya kazi katika *administration* ya nchi hii katika awamu zote pamoja na nyingine ambayo hatuizungumzii sana ya Waingereza. Nimeona aina mbalimbali za *administration* lakini *style* hii mpya ya Rais Kikwete kwa kweli inastahili sifa. *Style* hii mimi pamoja na uzoefu wangu sijapata kuiona. Tulizoea kutawala lakini Rais huyu anafika kwa watendaji wake na anaonyesha njia, anawaelekeza matumaini yake, malengo yake na nini anategemea kutoka kwao. Faida yake kubwa wacha ya kuwapa hamasa ya kufanya kazi lakini inasaidia kupima kadri tunavyokwenda. Tunakwenda kufuatana na malengo tuliyowekewa na kama hatuendi hivyo tufanye nini kurekebisha. Hiyo ndiyo *administration* ambayo mimi nafikiri ni nzuri sana na kwa kweli mimi naridhika moja kwa moja na hotuba hii iliyojaa ufasaha, yenye busara, inayoona mbali na ina ushawishi na hoja nzito nzito sio ya kulazimishana sio ya mabavu kama tulivyozoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inafuatana na utekelezaji ambao wenzangu wengi wamekwishazungumzia. Si rahisi kumwona Rais wa nchi mwenye mamlaka makubwa kiasi hicho ametembelea hospitali, anaangalia wagonjwa sio ndugu zake lakini ni raia. Nakumbuka picha moja nilimwona amekaa na mgonjwa mmoja, hii si rahisi. Amefika sehemu mbalimbali kwenye matatizo Kariakoo na kila mahali. Hili nafikiri ni funzo kubwa hata kwa sisi viongozi wengine tuliozoea kukaa mezani. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *style* ni nzuri ya kwenda kwa watendaji na kuonyesha njia. Kila Wizara iliyotembelewa au chombo kilichotembelewa nafikiri na wao wameona faida ya utaratibu huu kwa sababu na wenyewe wanawekwa sawa waweze kujua nini wanatarajiwa kufanya katika muda fulani. Kama nilivyosema hiki ni kipimo

ambacho kitatumika mbele ya safari tulipatana hivi je tumetekeleza au hatukutekeleza. Huyu ni Rais wa watu na nina hakika kabisa tukiendelea kwa mwendo huu ile dhana ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya itazaa matunda pengine muda mfupi zaidi kuliko tunavyofikiria. Pamoja na sifa hizi zote mimi ningependa kusemea mambo kama mawili, matatu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza linahusu ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri za Wilaya. Nakumbuka Rais katika kutembelea Wizara ya Fedha aligusia masikitiko yake kuona fedha za *Road Fund* za barabara zinaliwa hovyo hovyo na nadhani aliwataka watafute utaratibu wa kuzuia ulaji huo. Mimi nafikiri ni vizuri pia tuone kwa nini inafanyika hivyo. Utaratibu wa kutoa *tender* katika Halmashauri mimi nafikiri hauridhishi. Tenda hutolewa na kikundi cha wafanyakazi wataalamu wanaoitwa *Tender Board* ya pale. Kazi ya Halmashauri ni kuidhinisha tu fedha mwanzoni lakini hiyo *Tender Board* kazi yake baada ya kuchambua hizo tenda zilizopokelewa wanatoa kadri wanavyoona inafaa na wewe Halmashauri au tuseme kwa maana ya Diwani na Mbunge ambaye naye ni Diwani hawana fursa ya kuona utendaji ule. Hawawezi kuhoji kwa sababu utaratibu ndio huo. Mimi nafikiri wakati umefika ni vizuri tubadilishe utaratibu huo. Halmashauri sio tu iidhinishe fedha lakini iidhinishe na hizo *contracts* wasiachiwe tu wataalamu kwa sababu hii inajenga mwanya mkubwa sana wa rushwa. Sehemu nyingi ninazozijua mimi rushwa katika Halmashauri iko katika msingi huo wa kutoa tenda mbalimbali. Ili Madiwani pamoja na sisi kama Madiwani tuweze kusaidia Halmashauri kudhibiti mambo haya, nashauri utaratibu huu uchunguzwe upya ili kusudi tusaidie kupiga vita rushwa ambayo kama tujuavyo imeenea sehemu nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo lingine ningependa kuzungumzia ni *local* yaani la jimbo langu na linahusu ajira ya vijana. Hivi karibuni kuna wawekezaji wa humu humu ndani au tuseme wa pale pale jimboni walikuwa wametengeneza kiwanda kikubwa sana cha kutengeneza sigara. Walitumia mkopo wa shilingi bilioni 4.8. Wametengeneza sigara zinaitwa nyati. Lakini walipoanza tu kutengeneza wakapambana na vita kubwa sana kutokana na Kampuni nyingine ya sigara, wakapelekwa Mahakamani na kadhalika. Ule mchakato umesababisha kiwanda kile kisilipe madeni yake ya fedha iliyokopwa.

Kwa hiyo, kiutaratibu ikabidi kiwanda kile kisimamishwe na sasa kimefungwa. Kufungwa kwake kuna maana ya kupoteza ajira ya vijana kama 600 hivi. Mimi nafikiri wakati tunapowapa moyo wawekezaji kutoka nje tusisahau wawekezaji kutoka ndani. Hawa ni wawekezaji kutoka ndani lakini baada ya kutumia fedha nyingi sana tena za Serikali kwa sababu walikopa huko sasa kiwanda kile kimekufa wamebaki na madeni na vijana wetu 600 wameacha kazi.

Mimi nashauri kwamba jambo kama hili ni kinyume na sera zetu. Kwa hiyo, ni vizuri nishauri kwamba pengine ni vyema wakati tunapowabembeleza wawekezaji kutoka nje pia tuwape msukumo wawekezaji wa humu humu nchini. Kwa hiyo, naomba Serikali ichunguze jambo hili ambalo kwangu ni sawa na hujuma ya uchumi. Jimbo langu halina kiwanda chochote hicho ndicho kilikuwa cha kwanza, sasa kimekufa hata kabla hakijazaliwa. Sasa hawa watu wanataka kuwekeza katika vitu vingine lakini wana hofu

kwamba pengine watapigwa vita vile vile. Kwa maana hiyo naomba Serikali izingatie umuhimu wa kuwalinda wawekezaji wawe wa ndani au wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kugusia tu ni juu ya mbolea. Mbolea ni pembejeo muhimu sana katika kilimo kokote nchini. Si miaka mingi mbolea hii tunayonunua leo kwa shilingi 15,000 mpaka 20,000 na kwingine zaidi ya hapo tulikuwa tunanunua kwa shilingi 700/= kibegi kile cha kilo 50. Leo kibegi kile kile unanunua kutegemeana uko wapi. Jimboni kwangu bei inabembea toka 15,000/= mpaka 25,000/=. Hata hizi wanazosema ruzuku kwa kweli hazikuleta tofauti, ruzuku imepunguza 1,000/= tu katika mfuko au 1,500/=. Mimi nafikiri hii haijatusaidia hata kidogo. Mimi nafikiri kuna haja ya kutazama suala hili upya. Kwa vile muda umekwisha niishie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Galinoma, namwita Mheshimiwa Chacha Wangwe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa hii nafasi. Napenda kukupongeza kwa kuipata hiyo nafasi ya kuwa Naibu Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge hili, ni jambo la kihistoria, lakini naamini ya kwamba ulistahili kutokana na *merits* zako wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Pia ningependa kumpongeza Spika wetu, Mheshimiwa Samuel Sitta, ambaye falsafa yake ya *Standards and Speed* inanivutia sana, kwa sababu kweli vitu vinatakiwa kwenda katika *standards* na kwa *speed* inayostahili. Ninapoongea hivyo ninamaanisha kwamba ninatambua kwamba uongozi wa Bunge hili ni mzuri. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi wote Waheshimiwa Wabunge tuliopo hapa kuwa hapa katika kipindi hiki, katika historia hii, kwa sababu ana sababu ndiyo maana tumekalia hivi viti na pia ningependa kuwapongeza wananchi wa Tarime kwa ujasiri wao na uamuzi wao wa makusudi wa kunichagua mimi Chacha Zakayo Wangwe, niliyekuwa napambana na vigogo waliokuwa wanajinadi kwamba wao wana fedha nyingi na wana uzoefu mkubwa sana wa kuharibu uchaguzi lakini kwa nguvu za wananchi wa Tarime yaani nguvu ya umma nipo hapa leo. Nawashukuru sana wananchi wa Tarime. *(Makofi)*

Napenda kuzungumzia suala la Baba wa Taifa. Mimi namshukuru sana Baba wa Taifa, kwa kulilea hili Taifa katika misingi ya ukweli na haki na kutokana na hali hiyo nataka kuwakumbusha wanaCCM waliomo humu kwamba wasije wakadhani Mwalimu Nyerere ni mali yao. Mwalimu Nyerere ni mali ya Watanzania na watu wote wa dunia wanaopenda haki na ukweli na mimi ndiye aliyenifundisha na kuniweka katika misingi ya kuelewa siasa na ukweli, kazi ambayo huwa naifanya mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mwalimu alililiweka hili Taifa katika misingi mizuri isipokuwa nadhani kuna hitilafu ambayo imetokea ndiyo maana hata kabla ya kifo

chake Mwalimu Nyerere aliunga mkono kuwepo kwa vyama vingi katika nchi hii. Hilo halina ubishi kwa sababu aliwahi kushiriki katika Uchaguzi mwaka 1995 na akampigia kura Mbunge aliyekuwa amegombea kwa tiketi ya *NCCR- Mageuzi.* Kwa hiyo, mtazamo wa Mwalimu ulikuwa ni mpana zaidi kuliko wengi tulionao leo ambao sera yao ni kuwanyanyapaa viongozi na vyama vingine ambavyo ni tofauti na Chama cha Mapinduzi

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi uliopita naamini wengi tumeushuhudia, kila mwananchi ameushuhudia kila mgombea alishuhudia kilichoendelea, kwa hiyo, pamoja na mambo mengi matamu ambayo yatakuwa ni mambo ya sisi kujigamba lakini ukweli wake unafahamika. Aliyechaguliwa kwa haki anajijua na watu wanamjua, aliyejichagua vinginevyo pia anajulikana mpaka ndani ya roho yake anajijua. Kwa hiyo, hilo nisingependa liwe suala la mjadala. Ila ninaamini ya kwamba sisi wote tumekuwa hapa kama Wabunge kipindi hiki na ni lazima tushirikiane kwa kuwatetea wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengi ambao wameumia katika kipindi hicho cha uchaguzi.Wengine wamepoteza maisha yao. Katika Jimbo langu watu wamekufa, wamepigwa, wamekatwa na mapanga, lakini hizo fujo zote hazikufanywa na vyama vya upinzani, zilikuwa zinafanywa na wale ambao wanaamini ya kwamba ni lazima wabaki madarakini kwa gharama yoyote ile. Hili nalo naliona ni kinyume na maadili aliyotufundisha Mwalimu Nyerere kwa sababu *democracy* katika nchi yetu imefikia kwamba sasa ni demokrasia ya vyama vingi na viko hapa, wala havitaondoka ila tunazidi kujifunza ya kwamba udikteta na mawazo ya kidikteta bado yanaendelea kuwepo. Lakini yataisha kwa muda wake. *(Makofi)*

Nakishukuru sana Chama changu cha CHADEMA ambacho kwa ujasiri mkubwa kimeamua kwamba kitakuwa jukwaa mbadala la kueleza mawazo ya wananchi na sambamba na CHADEMA vyama vingine vyote vya Upinzani ambavyo mpaka leo vinaendeleza kutetea wananchi na kutoa mawazo ya wananchi bila woga katika hali ngumu ya vitisho na kejeli. Lakini mpaka leo tuko hapa baadhi lakini ndiyo ishara ya kukomaa kwa vyama vingi kwamba wananchi wataendelea kuwakilishwa katika majukwaa tofauti tofauti. Kwa hiyo, nawapongeza na kuwapa moyo kwamba waendelee kuwa na msimamo huo huo. *(Makofi)*

Mimi binafsi na chama changu tunatambua ya kwamba Rais Jakaya Kikwete ni Rais wetu wote na tunamtambua na hata siku alipokuwa anatangazwa, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Freeman Mbowe alikuwepo, alimkumbatia. Kwa hiyo, inaonyesha ukomavu tulionao wa kuelewa hali ya kisiasa na kutambua ya kwamba tunachohitaji ni kupiga hatua ya kwenda mbele na pia tunamuunga mkono Rais Jakaya Kikwete, sio kinafiki kwa sababu kama wanavyofanya baadhi ya watu kumtajataja na kumuunga unga mkono eti kwa sababu wanatarajia kwamba watapata labda kuteuliwa katika kufanya kazi fulani kwa hiyo, wanamtajataja kinafiki. *(Makofi)*

Sisi tunataja kikweli na kwa dhati kwa sababu tunafahamu ya kwamba Mheshimiwa Rais Kikwete ana nia njema na hiyo imejidhihirisha kwa wananchi wote. Pia tumekubali kwamba kwa sababu ni mtu ambaye ni *product* ya Mwalimu Nyerere

ambayo hata sisi pia ni *product* hiyo hiyo, kwa hiyo, tunajijua tu *in action* tukionana kwamba yule ni mtu ambaye yuko *committed* na tunaamini ya kwamba yale aliyoyasema katika Hotuba yake hii ambayo leo hii tunaichambua atajitahidi kuyatekeleza ingawa kutakuwa na vikwazo vingi kutokana na wale ambao wako *against* lakini wanajifanya wako karibu naye sana.

Mimi kama mwanachadema sio kwamba sielewi mambo ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu nimetoka humo na mambo ya Chama cha Mapinduzi ambayo mimi nataka kuyajadili hapa sio vikao vyenu ila ni ile *slogan* yaani kauli mbiu ambayo Mheshimiwa Kikwete ameitoa ya ari mpya, nguvu npya na kasi mpya.

Kwanza naomba kutoa mtazamo kidogo kwa sababu naona vyombo vya habari na baadhi ya viongozi wa Chama cha Mapinduzi hawajaelewa mpangilio kabisa wa hii *slogan* jinsi ulivyo yaani wengine wanasema kasi mpya, nguvu mpya, wengine wanasema nguvu mpya, kasi mpya. Lakini nadhani kulingana na hotuba hii, hii inamaanisha kwamba ari yaani lile wazo na nguvu inafuatia. Sasa ile nguvu nikii-*define scientifically,* nguvu inakuwa *defined* kama *mass times capacity squared*, kwa hiyo, nina maana kwamba hiyo nguvu ndiyo sasa itaongezea na *speed* na *speed* lazima iwe na *velocity* na *direction*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaelewa Rais wetu anataka tufanye nini, kwa hiyo, tunamuunga mkono isipokuwa pia ningependa kuwaeleza wenzangu wa Chama cha Mapinduzi ya kwamba tukubaliane kwamba lile neno Chama cha Mapinduzi, mnalichukua *for granted.* Lakini Mwalimu aliposema Chama cha Mapinduzi alikuwa anamaanisha *revolution,* tukubaliane ya kwamba mapinduzi hayakutokea katika nyanja zile ambazo Mwalimu alitarajia. Kwa mfano, mapinduzi hayajatokea kwenye kilimo Tanzania, mapinduzi hayajatokea kwenye viwanda Tanzania, mapinduzi hayajatokea kwenye elimu. Kwa hiyo mkiji-*compare* sana na watu kama China au Korea, Cuba, au *USSR,* kwa sababu wao wanaonyesha wazi wamepiga hatua katika hayo mambo na wanachofanya ni *modernization.*

Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi huwa naangalia kuna neno la *modernization.* Inaonekana hamjachukulia *serious* hili neno la *modernization,* sasa tuna-*modernize* nini kama hiyo *revolution* haikufanyika. Kwa hiyo, mlitafakari vizuri hilo neno mnapokuwa mnalitumia, kwamba hamko *serious.* Muongelee masuala ya *economic base,* mfahamu kwamba ile *mode of production* kama imebadilika kutoka *socialism* sasa *mode* ile inayotaka kutumika sasa ni ipi na *base* yake ni ipi. Sasa kama viwanda hatuna, tumeshindwa ku-*conserve* mpaka hata rasilimali zetu. *(Kicheko/ Makofi)*

Kwa mfano, sidhani kwamba Wachina waliwaita wazungu kwenda kuwapa dhahabu na almasi na nini ndiyo wakaweza kuendelea. Hizo ndizo rasilimali ambazo tunatakiwa tuzitumie ili tuweze kuzalisha, sasa tunazitoa, na hiyo ndiyo *grievance* kubwa ya Jimbo langu la Tarime. Kwa sababu sisi tumezungukwa na rasilimali nyingi, kuna mbuga ya wanyama, badala yake watu wangu wanapigwa risasi mle kwa sababu kwamba wamechunga ng'ombe kule, tuna migodi wazungu wanachimbua dhahabu pale

usiku na mchana wanaondoka nayo tunaangalia. Nasema hata kama hatukusoma hawa watu wanatuibia, hii ni mali yetu.

Vile vile vitu kama Ziwa, hifadhi ya mazingira, sasa katika hifadhi ya mazingira nilikuwa na mchango kidogo kwamba katika ile *slogan* ya Mheshimiwa Rais ambayo amezungumzia nguvu, nadhani tusiweke umeme wa *hydro- power* kuwa kwamba ndiyo *priority.* Hatutaweza. Kwa sababu idadi ya watu wanaotumia umeme Tanzania ni asilimia saba tu na kwa sababu hiyo sisi tungetia mkazo zaidi katika *biogas,* wakulima wetu wapunguze mifugo lakini tutengeneze *biogas* kwa ajili ya nguvu za nishati, itatokana na mifugo, inatoa samadi, *biogas* ni kitu *viable* kabisa kwa hiyo muwe mnatafuta ushauri hata kwa sisi wapinzani kwa sababu hii ni hazina kubwa ya watu ambao wako tu *dormant* hapa, muwatumie vizuri viongozi wetu hata wale walioshindwa Urais, wanaweza kuwapa mawazo. Wapo, ni viongozi wa nchi hii na ni wenzenu vile vile.

Kwa hiyo sera ya ubaguzi ambayo Rais ameikataa humu nadhani muizingatie, kwa sababu suala la ile kutubaguabagua amekataa Rais. Sisi tunamuelewa Rais, mjue mnatubagua bagua muelewe kwamba na sisi, vile vile ni wadau katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea kumalizia, naomba kuzungumzia suala la kilimo. Kilimo tunapata maji mengi tu kwa mvua na ninaamini mvua zitanyesha tena, lakini tunapoteza maji mengi sana kwa kushindwa kuya-*conserve*. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa heshima uliyonipa ya kutumia muda wa dakika kumi katika kutoa hoja yangu na mimi nakuahidi nitazingatia muda huo. *(Makofi)*

Awali kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameitoa kwetu sisi Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu. Kwa kweli hotuba hii ni nguzo ambayo inatoa *direction* ya utendaji kazi katika nchi yetu katika awamu hii ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi sana kuwa Waziri Mkuu. Tunaimani naye sana kwa sababu ameanza vizuri kwa mtazamo huo wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika. Mimi namfahamu sana Naibu Spika wetu ni mama mmoja hodari, jasiri sana katika kufanya kazi na anapokaa mbele pale mimi huwa ninajivuna, najisikia sifa kubwa sana kwamba kweli anatuwakilisha vizuri kama kundi la wanawake. Nampongeza vile vile Mheshimiwa Spika, ambaye anatuongoza vizuri hapa Bungeni. Nichukue fursa hii kwa kifupi pia niwapongeze sana na kwa kuwashukuru sana kina mama wa mkoa wa Mbeya ambao walinichagua kwa kura nyingi sana, nije niwa wakilishe hapa Bunge kwa asilimia 97.3. Kwa hiyo, kwa kweli nawashukuru mno na

ninaahidi kuwatumikia vizuri katika muda wangu huu wa miaka mitano, kwa sababu sasa nina nafasi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.*(Makofi)*

Naomba sasa nichangie machache tu katika hotuba hii, kuna mengi yamezungumzwa lakini nigusie moja katika suala la huduma za jamii, nalo linahusu elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zilizofanyika katika nchi hii ni kubwa sana na mafanikio makubwa sana ambayo yameonekana katika Serikali yetu. Suala la elimu kupitia mpango ule wa *MMEM* ulizaa matunda mazuri mno na kutokana na hali hiyo basi elimu tunaichukua na tunakubali kabisa kwamba ndiyo elimunguzo kubwa sana ya kukuza uchumi katika Tanzania. Matokeo mazuri ya *MMEM* yametufikisha na kutuweka katika sura na matatizo ya kuwa na wanafunzi wengi ambao wamefauru kwa hali ya juu sana lakini wanashindwa kupata nafasi ya kuingia *form one.*

Mimi nilikuwa na ushauri mdogo kwamba ninaelewa Serikali yetu ina mikakati mizuri tu na mikubwa ambayo imejiwekea kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wananchi wenyewe mashirika na madhehebu mbalimbali ili kupata nafasi za wanafunzi waliokosa nafasi.

Ningependa nishauri kwamba pengine tungeziangalia hizi shule binafsi hata kama hao wanafunzi wamesoma katika shule za Serikali lakini tuwaombe hawa watu binafsi wenye shule. Tuwaombe wachukue hawa wanafunzi wengine waliobaki lakini Serikali itoe *subsidy* kwenye shule hizo, walau hata kama ni kwa kipindi cha miaka miwili mpaka miaka mitatu, inawezekana ikatosha, wakati Serikali itakuwa imeshajiandaa kujenga shule zetu za kutosha lakini watoto wetu watakuwa wemeshaingia katika shule. Jitihada za Serikali kama zinaendelea basi ziendelee, lakini hawa sekta binafsi nao watusaidie na wakubali kushirikiana na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala la kukuza uchumi. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amezungumza vizuri sana kuhusu suala la kukuza uchumi na hasa uchumi unaoshirikisha raia wengi. Hilo ni suala zuri sana na napenda niligusie kidogo. Serikali ya awamu iliyotangulia ilishatoa maelekezo kwamba kila Mkoa, kila Wilaya ijitahidi kwa namna moja ua nyingine, kuwashirikisha wananchi wake kujaribu kuanzisha vituo vya uwekezaji, kuanzisha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne, namshukuru analiendeleza hilo nalo ni la muhimu sana, kuanzia ukurasa wa 33 mpaka ukurasa wa 35 analizungumzia, na mimi nimefurahi. Katika Ibara ya 4 ya ukurasa wa 35 amesema wazi kwamba katika kutekelezwa hili ataitaka Mikoa ianzishe vituo vya kufanikisha uwekezaji. Mkiisoma vizuri mtaliona hilo, katika Mikoa vile vile kuanzishwe Mabaraza ya Biashara ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vyombo muhimu sana katika kukuza uchumi. Kwa hiyo nakubaliana naye kwa asilimia mia, kwamba iwapo Mikoa yetu, Wilaya zetu, itajitahidi kutekeleza hili basi wananchi wetu watakuwa wemeshirikishwa sana katika kukuza uchumu katika maeneo yao.

Labda nitoe mfano mdogo tu kuelezea namna hili lilivyofikia nafasi nzuri, kwa kuwa lilianza mwaka wa 2003/2003 kuna baadhi ya mikoa imeshaanza kulifanyia kazi hilo la kuanzisha vituo vya Mikoani vya uwekezaji ili vituo hivyo viwe ni nafasi nzuri ya watendaji kujaribu kuainisha maeneo mazuri yanayoweza kufaa kwa uwekezaji. Ukiachilia mbali vile viwanda vingi ambavyo vimekufa katika Mikoa.

Mmoja katika Mkoa ninaoufahamu ni Mkoa wa Kilimanjaro, ulianzisha, kituo cha uwekezaji ambacho, kiko chini ya Kanda ya Kaskazini. Lakini pamoja na juhudi hizo naona *impact* yake haionekani kwa sababu matunda yake hayaonekani na hayawezi yakaoneka kama vituo hivi havipatiwi fedha, hakuna *resources*. Haiwezekani vikaenda tutabaki tunafanya *dialogue* mwisho hakuna *impact*. Watu wanajiuliza kwa mfano kwamba kama kuna vituo hivi vya Kanda na Mikoa sasa matokeo yake nini? matokeo wangeyaona kama tungeweza kuwezesha hivyo vituo vikapata fedha.

Sasa ningeliomba, dalili nzuri iliyoanzishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyepita kwa kuunga mkono kwa kutoa fedha, mwaka jana aliahidi hapa kutoa fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya vituo vya uwekezaji vya Mikoa, Fedha hiyo mimi nishahidi haijaweza kuoneka, sijui kama kuna Mbunge ameiona hapa au ameiona huko Mikoani.

Katika Mikoa iliyoanzishwa kama Kilimanjaro hakuna, fedha hiyo sasa kama hakuna basi hakuna *impact*, lakini fedha imetolewa ukiwauliza watendaji wanasema kwamba haziwezi kutolewa fedha hizo kwa sababu sheria hakuna. *Fine* kama hakuna sheria basi ni changamoto kwa Bunge hili, changamoto kwa Serikali kuangalia sasa kauli hii ya Marais wetu na kusisitiziwa sasa hivi na Rais Kikwete kweli ni kauli ambayo lazima iungwe mkono na sisi Wabunge. Lakini pia na Serikali kwa maana ya Hazina kwanza kwa Wabunge kwa kupitisha sheria ya kuvitambua vituo hivi pamoja na Mabaraza ya Biashara ya Mikoa.

Tukishafika hapo, itakuwa rahisi sana kwa vituo hivyo kufanya kazi na kuweza kuendelea kuchangia uchumi wa kaya, uchumi wa wananchi, uchumi wa taifa kwa ujumla. Maeneo ambayo yanaweza yakaangaliwa itategemea na utashi wa Mikoa na Wilaya yenyewe na itategemea vipaumbele vilivyowekwa na Mikoa na Wilaya zinazohusika.

Mathalani mkiweka kipaumbele kwenye utalii kwa mfano, kwenye elimu bora, basi vituo hivi vidogo vitaainisha maeneo hayo na kutafuta wawekezaji kupitia hivi vituo, halafu wawekezaji wataweza kuchangia uchumi wa Mikoa yetu, uchumi wa kaya zetu na uchumi wa Wilaya zetu. Kwa hiyo naomba sana Bunge hili au Serikali ilitazame hili *seriously* kwamba kauli hii isiende patupu.

Kwa hiyo naomba sheria itungwe ya kuvi-*legitimize* hivi vituo vilivyoko katika Mikoa na baadaye vitakwenda katika ngazi za Wilaya *and then* vitaleta ahuweni katika kukuza uchumi, katika maeneo yetu. Leo hii tunazungumzia hapa uhaba wa ajira, vingekuwepo vituo katika Mikoa katika Wilaya ajira hizi zingepatikana huko huko katika Mikoa katika Majimbo yetu, na wananchi wangeweza kufanya vizuri.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi tukirudi hapa, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na wengine wakaangalie orodha. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06: 59 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza asubuhi, orodha yetu ya wachangiaji imebandikwa kwenye sehemu ya matangazo. Kwa hiyo, nimefanya mabadiliko kidogo tu kwa kuanza na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, ni mwenzetu yule ambaye haoni. Sasa kwa sababu mpaka atengeneze mambo yake kwenye ile ya vidole, basi nimeona tu nimwingize kwa sababu yeye alikuwa ameomba leo, orodha ilifungwa jana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Kahama, akifuatiwa na Hafidh Ali Tahir.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata wa kuiongoza nchi yetu. Pia, nampongeza Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa nchi yetu. Vile vile, nampongeza Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuongoza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano.

Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Awamu hii ya Nne ya Uongozi wa nchi yetu. Pia, sina budi kushukuru Chama changu kitukufu, Chama cha Mapinduzi kwa kuniwezesha kupata nafasi hii kupitia Jumuiya yetu ya UWT kutoka tangu kule Zanzibar kwenye kura za maoni, Mkoa wa Mjini Magharibi, pia na Baraza Kuu la UWT kwa kunichagua ili na mie niwe Mwakilishi, Mbunge katika Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajenda yangu ya pili kabla sijaingia kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, kuna kitu kidogo mimi kinanikereketa hapa kinapozungumzwa, kwa sababu hii nchi ni yetu na wananchi ni wetu. Kwa hiyo, huwa kidogo nasikitika na ningeomba wakati mtu anapotoa mchango wake wa kuelekeza, asitumie njia ya kulaumu. Tuelekezane kwa busara. Palipokosewa mtu atoe ushauri kwa lugha nzuri, lakini siyo kulaumiana au kutumia maneno ya kukomoana. Kwa hiyo, hiki

kitu ni chetu sote, palipokosewa pafahamishwe vizuri, paelekezwe kwa kutumia lugha ya busara, siyo kutumia maneno ya kukomoana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiingia kwenye ajenda iliyokusudiwa ya kuchangia kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa kweli nikiwa nawakilisha Jimbo la Watu wenye Ulemavu, nimefarijika sana na hotuba hii kutokana na pale kwenye ukurasa wa 13 hadi wa 15, katika maneno kumi yale, kuna sehemu ina maneno kumi ikianzia kifungu cha kwanza amani na utulivu katika nchi yetu na mambo mengine. Lakini katika mambo kumi hayo kuna sehemu ya mwisho ile aliyozungumzia kuhusu Makundi Maalum, wakiwemo watoto, wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo na mimi nikiwa Mwakilishi wa watu wenye ulemavu katika Bunge hili, nimefarijika sana kuona hotuba ya Mheshimiwa Rais ukilinganisha na Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005, nayo imezungumzia sana masuala ya watu wenye ulemavu na ndiyo yale yale ambayo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake yamo.

Kwa hiyo, ni imani yangu na kwa niaba ya watu wenye ulemavu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala haya kwa vile kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi yamo na yamezungumziwa na mwenyewe Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake, bila shaka watu wenye ulemavu watashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi tu ambayo bado watu wenye ulemavu hayajashughulikiwa, kwa mfano; kuna hii inaitwa *Standard Rules*, inazungumzia mambo ya *equalization of opportunity* yaani Kanuni 22 za Watu wenye Ulemavu. Katika Kanuni hizo, yamo mambo ya makazi, ajira na mambo mbalimbali ambapo pia kwenye Ilani ya Uchaguzi yamezungumziwa. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwa niaba ya watu wenye ulemavu wa Jamhuri hii, yote hayo yatazingatiwa na yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala lingine. Kuna huu Mkataba wa Watoto, Serikali yetu iliuridhia; kuna Mkataba wa Wanawake *(SHIDAU)* iliuridhia; lakini ukija kwenye Mkataba wa Watu Wenye Ulemavu, bado Serikali haijauridhia au bado haujashughulikiwa. Ni imani yangu kwamba Wizara inayohusika kwa kutilia mkazo na mkakati wa haya yaliyozungumzwa kwenye Ilani ya Uchaguzi na hotuba ya Mheshimiwa Rais, yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya mwanzoni na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote kuwa hapa na tumeweza kukaa vizuri mpaka sasa hivi na afya njema na aendelee kuwa na sisi tumalize mwaka huu wote salama.

Pili, niko hapa pia kutaka kuwashukuru ndugu zangu wa Mkoa wa Dar es salaam akinamama ambao wameniwezesha kurudi tena katika nafasi hii ili niweze kuwatetea. Natoa shukrani zangu kwa ndugu wote wale hasa wa Chama Cha Mapinduzi na ndugu

wengine wa Vyama vingine ambao walitoa kura zao nyingi sana kwa kuhakikisha Rais Jakaya Mrisho Kikwete anashinda kwa kishindo kikubwa.

Kwa hiyo, natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, lakini pia natoa pongezi zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Dr. Shein naye katika kurudisha nafasi yake aliyochaguliwa kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, pongezi nyingine zimwendee Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindi huo wote, kwa wote hawa watatu ulikuwa ni ushindi mzuri ambao ulionyesha kabisa kuwa wananchi wa Tanzania sasa wamekomaa kisiasa na kuwa hawataki kuwa na lugha mbaya za matusi na vile vile hawataki kuwa na vitisho vya aina yoyote na wanapenda amani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa mwenzetu ambaye alikuwa Mbunge Mwenzetu na tunaye hapa, Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuchaguliwa kwake kuwa Waziri Mkuu.

Vile vile, natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Spika, Samwel Sitta kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu wa Bunge hili. Natoa pia pongezi nyingi sana kwako wewe mwenyewe Makamu wetu, mdogo wangu Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Hatukuwa kabisa na wasiwasi na uchaguzi wako, maana yake tunajua unajua kazi yako kimahiri kabisa.

Lakini naomba pia nitoe shukrani kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupitia tanuri kubwa, matanuri yamewasumbua, lakini Mwenyezi Mungu amewajalia mmechaguliwa na mko hapa. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mawaziri wetu wapya na Manaibu Waziri walioteuliwa. Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia wafanye kazi yao vizuri. Nasema poleni na ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nataka pia kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Dar es salaam nitoe pole zangu za dhati sana kwa Mheshimiwa Jina ambaye nadhani wengine pia tumesahau kuwa alitutoka dunia na yeye alikuwa miongoni mwetu akina mama Wabunge wa Viti Maalum. Alikuwa katika Bunge lililopita na pia alikuwa amechaguliwa, amekwishapita kuingia katika Bunge hili, lakini Mwenyezi Mungu alichukua roho yake. Mwenyezi Mungu amjalie alale mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nichukue muda huu sasa kutaka na mimi kutoa mchango wangu kuhusu hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Hotunba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa hotuba nzuri sana, ilikuwa ni ya makini sana ambayo kwa kweli iligusa maeneo mengi ya muhimu sana katika Wizara mbalimbali. Mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini mimi ningependa nitoe mchango

wangu katika maeneo matatu, nayo ni maeneo ya ushirika, uwezeshaji na maji kwa ufupi tu.

Katika Ushirika, hasa ilikuwa katika ukurasa wa 39 na 40. Mimi mwenyewe kwa kweli ninaelewa vikundi vingi sana vimejitokeza katika kuanzisha vikundi vya mikopo vya kuweka na kukopa ambavyo wengi wao ni wanawake waliojitokeza, wafanyabiashara mbalimbali, wakulima na wengine ni vijana. Lakini katika vikundi hivyo, pamoja na juhudi zote walizokuwa wamefanya, bado ninaona Serikali inahitaji kuweka mkazo maalum kabisa katika kuanzisha na kuimarisha Vyama hivyo na hasa kwa wanawake na vijana. Mpaka sasa hivi, pale ambapo pameanzishwa vikundi vya wanawake katika maeneo mengi niliyoyatembelea mwenyewe, kwa kweli yameboreka sana. Kwa mfano; Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Rukwa, Njombe na Mafinga. Hayo ni maeneo mengi ambayo ninajua yamepiga hatua na akina mama wa pale wameboreka sana.

Kwa maana hiyo basi, inafaa kuwasaidia waweze kupata misaada zaidi na hasa katika vile vikundi vinavyoanza. Vinahitaji misaada sana katika eneo la mafunzo hasa na pia vinahitaji misaada katika *seed capital* ambayo ni kitu muhimu sana na pia katika majengo kwa sababu huwezi ukaanzisha kikundi kikakua haraka haraka bila kuwa na jengo maalum la kufanyia shughuli za biashara kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nataka kusema pia kwamba tunashukuru kuna mfuko wa Taifa wa *SELF* ambao umesaidia kwa kiwango chake. Lakini, ingetoa upendeleo maalum, *SELF* pamoja na Mifuko mingine ya Fedha ingetoa upendeleo maalum kabisa kwa vikundi vya wanawake. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu vikundi vya wanawake ndiyo hasa wengi wao bado wako nyuma kiuchumi. Lakini sababu nyingine ya pili, wanawake tunaelewa vizuri sana, ni wachapa kazi hodari, lakini wanajua kutunza pesa yao wanayoipokea. Isitoshe wamekuwa wengi waaminifu katika marejesho. Hiyo ni ukweli kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie tatizo la soko. Kutafutwe ufumbuzi hasa wa kupitia *Display Centres* ambazo wanaweza wakapata takwimu mbalimbali na shughuli za biashara mbalimbali kutoka nje na ndani ya nchi na wanaweza wakapata *address* mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, uwezeshaji wa wananchi hasa wazawa ni muhimu sana na hii imezungumzwa katika *page* 33 mpaka 34. Lakini lengo kuu liwe kujenga kundi kubwa hasa mimi ninachoona la *middle class. Middle class* hii itafanya shughuli za kiuchumi Vijijini pamoja na Mijini. Tusiangalie upande mmoja wa Mijini, lakini tufikirie Vijijini pia. Pia itawezesha kuongeza ajira kwa wananchi wote kwa pamoja na kukuza mahitaji na shughuli za bidhaa nje ya nchi yetu na pia ndani ya nchi yetu. Kundi hili la *middle class* pamoja na Vyama vya Ushirika ndivyo vitaongeza kasi ya kupunguza umaskini. Ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, pia nashauri Serikali ichukue hatua ya makusudi kabisa ya kuanzisha *registrars* wenye mwelekeo wa kujiendeleza kufikia

kiwango cha *middle class*. Hao basi watakapopatikana wasaidiwe kwa mitaji, mafunzo na pia wasaidie kutambua miradi yenye faida na manufaa na ubunifu. Kama tunavyojua wenzetu wengi sana wanafanya biashara bila kubuni vitu vipya. Tunabaki na biashara zinazofanana zile zile za siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ningependa kushauri kuwa Vyama vya Wafanyakazi navyo vishauriwe kabisa kuanzisha vitengo vya uchumi katika maeneo yao ambavyo unaweza ukaviita *economic wings*. Hivi vitengo vitakuwa vya muhimu sana na pia sehemu ya mapato ambayo itapatikana katika hivi Vyama iwezeshe basi hizo *economic wings* na zenyewe kununua hisa katika Makampuni kwa kupitia *Dar es Salaam Stock Exchange* ambayo itawasaidia katika kuwaletea mapatao zaidi. Vile vile, *economic wings* hizo zitakuwa kama vyombo vya kuanzisha viwanda vipya kwa ubia wa wawekezaji wa nje wanapokuja hapa nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba viongozi wa *SACCOS* waweze kupatiwa nafasi ya mafunzo zaidi kujifunza kutoka nchi nyingine kama vile nchi za Lesotho, *South Africa* ambako wenzetu wameendelea sana katika mambo ya ufumaji. Vile vile vifaa vya usanii. Mara nyingi mimi nimekwishakutana na wengine *Women Investment Companies* ambao wanaweza wakatusaidia tukaboresha kabisa maeneo yetu ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nazungumzia mambo ya maji. Jamani ufumbuzi wa maji na matatizo ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kweli umekuwa ni kero kubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam wapatao milioni 4. Ufumbuzi huo ungefikiriwa katika sehemu mbalimbali. Jambo hilo liwe ni jambo la dharura. Nilikuwa nikifikiri isingekuwa vibaya kuchimba bwawa kubwa la maji ya kutosha kule *Upper Ruvu*. Au kama si hivyo basi, ningeshauri angalau kuchimba mfereji wa maji kutoka Mto Rufiji ambao siyo mbali na Mkoa wa Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kupigiwa kengele ya pili. Baada ya hayo, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia wenzangu kutoa shukrani kwa kunipa nafasi hii na mimi nafanya kazi hiyo. Lakini kwa sababu ya muda, niende haraka haraka katika kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa Ushindi mkubwa na wale wote ambao wamechukua nafasi katika Serikali hii ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Itifaki izingatiwe. Lakini, shukrani za pekee nazipeleka kwa wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, Jimbo la Dimani ambao ndio walionifanya nikaja hapa katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Raha leo miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambayo ndiyo hoja iliyoko mbele yetu hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubali pamoja na wenzangu kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Lakini, baada ya hapo kwenye kitabu hiki chote ukikiangalia, mimi nitakuwa ninazungumzia Ukurasa wa 17, 18 na 19 peke yake. Ninazungumzia kurasa hizo makusudi ili nijitosheleze na yale ambayo Mheshimiwa Jakaya Kikwete ameyasema katika hotuba yake lakini pia yamesemwa katika michango mbalimbali iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo ambayo Mheshimiwa Kikwete ameyasema, ni pale aliposema kwamba anasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba. Hili limezungumzwa sana lakini kwa bahati nzuri, kati ya wachangiaji ambao walikuwa wamechangia katika hotuba hii, walimwuliza maswali Mheshimiwa Kikwete kuhusiana na mpasuko huo wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako, ninukuu kidogo hayo maswali ambayo yanahusiana na hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kiongozi wa Upinzani alikuwa anamwuliza Mheshimiwa Rais Kikwete: "Je, ni historia ipi Mheshimiwa Rais alitaka kuizungumzia ambayo yeye anaiona kwamba imeleta na inaendelea kuleta mpasuko huo wa kisiasa Zanzibar?" Swali la kwanza. "Au ni ile historia ya baada ya Mapinduzi inayoendelea hadi leo katika kuigawa Zanzibari?" Pili; "Au ile historia ya upande mmoja wa kushika hatamu na kujiona peke yao na ndiyo yenye haki ya kutawala Zanzibar na kufaidika na matunda ya Serikali?" Tatu; "Au ni historia inayosema tulipata nchi kwa mapanga na hatuko tayari kuitoa nchi hiyo tuliyoipata kwa kumwaga damu kwa vipande vya karatasi na maneno?"

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maswali matatu. Lakini, napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa anazungumzia kusononekana si kwamba alikuwa hafahamu Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri alifanya kazi sana Zanzibar. Rais wa Jamhuri, alikuwa Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar. Anaifahamu vizuri Unguja, anaifahamu vizuri Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpasuko ulioelezwa hapa upo katika masuala haya matatu na hapa ndiyo mpasuko wa Zanzibar ulipo na katika Bunge hili umejitokeza hadharani kwamba hapa ndiyo penye mpasuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumza suala la kwamba Je, Mapinduzi ndiyo yaliyosababisha mpasuko huo kama swali la mwanzo lilivyosema?

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Zanzibar haikuja baada ya Mapinduzi. Historia ya Zanzibar imekuja miaka mingi nyuma. Kama zilivyo nchi nyingine katika Afrika, Zanzibar wananchi wake walitawaliwa na Wakoloni. Zanzibar wananchi wake waliteswa sana na Wakoloni. Tokeo la Mapinduzi ni moja katika mambo ya kuwaokoa wananchi wa Zanzibar katika madhira haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu anapozungumza kwamba Mapinduzi yameleta udhalimu Zanzibar, maana yake unatuambia sisi Wazanzibari huungi mkono Mapinduzi ya Zanzibar.

Meshimiwa Naibu Spika, hapa pana mpasuko kwa sababu kwa Zanzibar kama unafika pahali huyaungi mkono Mapinduzi ya Zanzibar, hakuna Mzanzibari hata mmoja atakayekubali. Kwa sababu Wazanzibari wote wanafahamu kwamba kitendo cha kupindua Serikali ya Sultan Zanzibar, ni kitendo cha kuiokoa Zanzibar na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaozungumzia suala la Mapinduzi ya Zanzibar kwamba wanaona labda ni ya kidhalimu, lazima tukumbuke Mapinduzi ya Zanzibar katika Dunia si ya kwanza. Katika nchi ambazo ziko katika Bara la Afrika, hivi sasa ambazo zinaendelea kutawaliwa na wale waliopindua, si Zanzibar peke yake.

Mhesimiwa Naibu Spika, Mapinduzi ya Misri, sote tunakumbuka wakati wa Firauni, Wananchi wa Misri wakachukua hatua ya kupindua na wanaendelea kutawala mpaka sasa, hakuna anayepiga kelele. Misri nchi ndogo! Lakini twende kwenye Mapinduzi ya Marekani. Mapinduzi ya Marekani yamewaokoa wananchi wa Marekani na wananchi ndiyo wanaendelea kutawala mpaka leo, hakuna anayezungumza. Iweje leo, Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yamewaokoa wananchi iwe ni Mapinduzi yanayoleta udhalimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii si sahihi na haiungwi mkono na Wazanzibari na Watanzania walio wengi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo haitoshi, suala la pili ameulizwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete lilisema "Au ni ile historia ya upande mmoja ya kushika hatamu na kujiona peke yao ndiyo yenye haki ya kutawala Zanzibar na kufaidika na matunda ya Serikali?"

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala kama haya yanaongeza mpasuko ndani ya mpasuko. Haya si masuala ya kuulizwa katika Bunge kama hili kwa sababu mambo haya yako wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuambiwa nani ambaye hajafaidika na Mapinduzi au matunda ya Serikali ya Zanzibar kwa waulizaji wa aina hii, ni dhamiri ya Wapinzani. Mheshimiwa, kwa Zanzibar Wapinzaini wakubwa ni *CUF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CUF* wameshafaidika na matunda ya Mapinduzi; *CUF* Zanzibar wameshakuwa viongozi wa ngazi za juu; *CUF* Zanzibar wameshawahi kupata nafasi ya Uwaziri Kiongozi Zanzibar; *CUF* Zanzibar Sudi Yusufu Mgeni ameshakuwa Waziri Zanzibar, Hamad Rashid aliyetoa tamko hili hapa alishawahi kuwa Waziri katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Abubakar alishakuwa Mwanasheria Zanzibar! Lakini hiyo haitoshi kwa lugha inayotumika humu kwa maana ya kugawa Wapemba na Waunguja.

Mheshimiwa Dr. Omar Ali Juma - Mpemba, alishawahi kuwa Makamu wa Rais katika Jamhuri ya Muungano. Dr. Ali Mohamed Shein hivi sasa ni Makamu wa Rais katika Jamhuri ya Muungano katika vipindi viwili. Faida gani inatakiwa na ndugu zetu Wapemba? Hawa ni viongozi kutoka Pemba?

Kinachotakiwa pale Zanzibar ili isionekane kwamba kuna mpasuko, basi lazima Rais atoke Pemba. Hii si sahihi! Mheshimiwa, Urais hauchagui pahali wala hauna zamu. Maana laiti ungekuwa Urais wa Jamhuri ya Muungano una zamu, tuhesabu Mikoa mingapi na Marais watakuwa wangapi! *(Makofi)*

Lakini tunatafuta nani anafaa na nani atuongoze. Kama tutarudi kwa Mheshimiwa Mwalimu Julius Nyerere, anasema kwamba Rais atatoka popote, awe wa dini yoyote, kama tunahisi huyu ataweza kutuongoza. Ikiwa ni Muislam, basi awe Muislam, Muislam. Akiwa ni Mkristo, Mkristo. Anasema hatutafuti Padri. Sasa na hawa wenzetu wasilazimishe kuwa Rais lazima atoke Pemba, awaache wananchi wachague Rais kutoka katika visiwa vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usihesabiwe mpasuko kwa sababu ya hili. Hili lilikuwa liko wazi. Ustahimilivu ni kitu kikubwa. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa hivi sasa aligombea urais akakosa, lakini tutazame historia yake imetoka wapi. Ustahilimivu umempeleka hapa alipo sasa na kwa hili tumpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama huna ustahimilivu utakosa, kama alivyokosa Seif Sharrif Hamad. Seif Sharrif Hamad alikuwa ni Waziri Kiongozi chini ya Idrisa Abdul Wakil. Mzee yule alikuwa tayari anakaribia kuondoka, alipoambiwa ampe nafasi Mheshimiwa Idrisa akakataa. Alipokataa, hapo ndipo ustahimilivu ulipomshinda, ukamshinda urais na urais unaletwa na Mungu. Mungu kama hataki uwe Rais huwi. Sasa ni lazima tukubali na hatusemi kwamba mpasuko huu ni wa kupangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 19 anazungumzia mfano mmoja, anasema: "Mambo yaliyotokea Zanzibar yanatugusa sote, pengine leo ni zaidi kuliko ilivyokuwa katika historia wakati ulipokuwepo msemo kuwa zumari ikipigwa Zanzibar wanacheza mpaka watu wa Bara."

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi ninachokwambia ni kwamba, masuala ya Mapinduzi ya Zanzibar na chokochoko na hayo mapengo tunayoambiwa zumari yake inapigwa Oman haipigwi Zanzibar. Zumari linapigwa Oman wanacheza *CUF* wa Zanzibar. Ni lazima tujigawa! Kama hatukuwa kitu kimoja ni lazima tujigawa na ni lazima Wazanzibari tuwe kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema historia inatoka mbali Zanzibar. Historia inatoka kwa viongozi waliopinduliwa Zanzibar. Kuna kiongozi anaitwa Ali Mukhsin Baruan. Huyu ni kiongozi ambaye yupo mpaka sasa na huyu ndiyo anayeleta chokochoko. Kiongozi huyu katika kila sherehe za Mapinduzi yeye ni lazima ataleta

waraka Zanzibar na kuelezea kwamba Mapinduzi si halali na wananchi wote wasiunge mkono. Zumari linapigwa Oman wanacheza Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na shukrani katika kuchangia hoja.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu mpaka siku hii ya leo. Pili, nawashukuru wapigakura wa Jimbo la Mbinga Mashariki kwa kunipa kura nyingi na kwa kweli kukipa Chama cha Mapinduzi kura nyingi sana. *(Makofi)*

Tatu, ningependa pia kumshukuru mgombea urais wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa safari yake aliyoifanya Mbinga na kusaidia sana matokeo haya mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa ushindi wa Rais wetu na Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa namna ya pekee pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na hatimaye kuthibitishwa na Bunge letu Tukufu. Naomba pia nimpongeze Spika wa Bunge kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, lakini pia nikupongeze wewe kwa namna ya pekee kwa sababu umeweka historia katika nchi yetu ya kuwa Naibu Spika wa kwanza mwanamke. Mwisho niwapongeze Wakuu wa Mikoa walioteuliwa na Rais, pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema awali kabisa kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwanza utakuwa wa jumla, lakini nitamalizia kwa kuupeleka katika Jimbo langu la uchaguzi la Mbinga Mashariki na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ametoa hotuba nzuri sana kwa lugha nyepesi na kuifanya ieleweke kwa kila mwananchi katika nchi yetu. Amefanikiwa kueleza mambo magumu sana, lakini kwa lugha nyepesi na laini. Hatua hii imewafanya wananchi waweze kuwa na imani na Rais wetu na chama chetu na Serikali yetu. Hotuba hii, imethibitisha ule usemi uliopo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi "Maisha bora kwa kila Mtanzania" kwamba inawezekana *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia tuliyonayo leo, wataalam wanajitahidi sana kufanya vitendea kazi viwe rafiki wa mtumiaji *(user friend)*. Ukiangalia kompyuta, ukiangalia mashine zote ni hivyo. Sisi Mwenyezi Mungu ametupa fursa hii ya kuwa na Rais na Waziri Mkuu ambao ni marafiki wa wananchi. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linathibitishwa na utendaji wao wa kazi katika siku 40 tu. Hotuba ya Mheshimiwa Rais katika mambo mengine imeona tatizo kubwa ambalo

pengine halijaangaliwa kwa muda mrefu, nalo ni mishahara midogo ya watumishi katika Serikali na katika umma. Mishahara hii ni midogo kiasi kwamba hata wawekezaji wetu wanapokuja nchini hapa wanakuwa na hamu ya kutaka kulipa mishahara mikubwa, lakini wanapoangalia mishahara yetu na wenyewe wanalegeza kamba kwa sababu wanataka faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais anapokuja na hoja hii inaleta faraja kwa kila mwananchi na uwezekano mkubwa wa maisha bora kwa kila Mtanzania. Ningependa kuwashauri Watendaji kuhusu suala la mishahara kwa sababu inapokuja katika suala la mishahara itaundwa Tume, lakini baadaye mapendekezo ya Tume hayatatekelezwa. Yamekuwa hayatekelezwi kwa sababu inaonekana ni gharama. Lakini wote tunaelewa kwamba katika uzalishaji kitu kikubwa ni binadamu. Ni rahisi sana kutumia fedha nyingi kwenye kompyuta, kwenye mashine, lakini linapokuja suala la kutumia hela kwa ajili ya kile kilicho muhimu zaidi, inakuwa ngumu. Natumaini kwa waraka huu wa Mheshimiwa Rais na katika hoja hii, msimamo huu utabadilika na Watendaji wataangalia jambo hili kwa makini zaidi ili wafanyakazi wa Tanzania wapate mishahara inayowafanya kuwa watu wenye utu na kuwaletea maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato ya Serikali na matumizi yake, naomba nichangie kwa upande wa matumizi. Mheshimiwa Rais amezungumza mengi na hasa amegusia masuala ya masurufu na kadhalika. Pengine kuna nyaraka nyingine zinatolewa kuelezea sehemu nyingi zaidi za kubana matumizi. Mimi nichangie hapo kidogo. Je, kuna uwezekano wa kuangalia kupunguza matumizi kwa upande wa misururu ya magari ya Serikali na Mashirika ya Umma? Zipo taratibu zinazotawala magari ya Serikali na magari ya umma. Ni kwa kiwango gani taratibu hizi tumezifuata ili tuweze kupunguza matumizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inaelezea pia amani na utulivu. Katika suala hili Waheshimiwa Wabunge wamechangia ufanisi wa polisi na kadhalika. Naomba nichangie kutoka kwenye kona nyingine. Sera zetu zinaweza zikasaidia sana kuleta amani au kuleta shida zaidi. Kwa mfano, kule Mbinga kuna machimbo ya madini mbalimbali, kuna Vijiji vya Masuguru, Ngembambili, Amani Makolo na vinginevyo.

Kingine ni Darpoli kwa Mheshimiwa Komba. Kule kuna vijana ambao ni wachimbaji wadogo wadogo, lakini mpaka sasa hawana uhakika kama wataendelea kuishi katika machimbo yale kwa sababu wanatishiwa kwamba huenda maeneo hayo yakachukuliwa na wawekezaji. Je, upo uwezekano wa Serikali kuwahakikishia wananchi hawa waendelee kuishi katika maeneo hayo? Kwa sababu kuishi kwao kule kunaleta amani sana katika Vijiji vyetu. Vibaka katika Vijiji wameondoka, mbuzi zinaweza zikakaa salama, ng'ombe wanaweza wakakaa salama na hata ubakaji umepungua.

Kwa hiyo, kuna haja sana ya kuwahakikishia wananchi hawa umuhimu wa kuendelea kuishi katika maeneo hayo badala ya kutilia umuhimu kwa mwekezaji mmoja ambapo hata maslahi yake katika mambo ya madini bado yana maswali mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia juu ya kilimo. Jana tumetumia muda mrefu kuongelea suala la njaa na ugawaji wa chakula. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba Mkoa wa Ruvuma haumo katika *list* ya kupewa chakula hicho kwa sababu wanacho chakula cha kutosha. Ningependa kumshauri Waziri wa Kilimo ajaribu kuangalia, siyo kwamba Ruvuma hatuna njaa, tunayo njaa isipokuwa ni ya aina nyingine. Njaa yetu kule ni mbolea. Wilaya ya Mbinga ilikuwa inahitaji mbolea kadri ya tani 8,000 lakini mpaka sasa imepelekewa tani 1,500 tu. Njaa ambayo tulizungumzia jana inatokana na njaa ya mbolea. Tupewe mbolea ili njaa hii tuliyoizungumzia iondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda na miundombinu, hapa ningependa kuzungumzia *vicious circle.* Mkoa wa Ruvuma haupati maendeleo kwa sababu kila tunapotaka kupeleka maendeleo tunaambiwa hakuna barabara nzuri, hakuna viwanda, hakuna hiki; tunawaomba Watendaji waangalie kwamba miundombinu ndiyo kitu cha kwanza kinachoweza kuleta mambo mengine. Kwa hiyo, kama ilivyo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi, barabara ya lami kutoka Songea mpaka Mbambabay, tungeomba utekelezaji wake uanze mara moja, ikiwezekana waanze Songea na waanze Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la umeme, kama nilivyozungumza katika Semina, Mbinga pamoja na kuwa na sifa zote za watu wanaofanya kazi, kahawa nzuri, nyumba za kisasa, hakuna umeme! Mheshimiwa Rais katika hotuba yake anazungumzia *ICT.* Tutakuwaje na *ICT* wakati hatuna umeme! Nafikiri Wizara zinazohusika zitaangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia suala la umeme. Kule Mbinga kuna mgodi wa makaa ya mawe. Wajerumani walikuwa wanavuna hayo makaa na sasa yameachwa hivi hivi katika eneo la Mbuyula na sasa yanaungua kwa muda wa miaka miwili na huo moto haujazimwa. Tungeomba hatua za haraka ziweze kuchukuliwa kuangalia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niangalie suala la mikopo. Mabenki yetu yanatoa riba kubwa sana kwa mikopo. Kwa wafanyakazi riba ni asilimia 20, kuna gharama gani? Kuna *risk* ipi? Wabunge wanapata mikopo, lakini Bunge linapeleka mishahara hii katika Benki, Benki inaingia gharama gani mpaka wafanyakazi wapate kulipia gharama kubwa kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu UKIMWI, wakati uliopita kulikuwa na mjadala mrefu kati ya Watendaji mbalimbali na Mashirika ya Dini. Binafsi naona kama watu wa dini ni *partners* katika jambo hili. Tungeomba tuwaone katika mwelekeo huo ili sote kwa pamoja tuweze kutatua hili tatizo gumu badala ya kuona kama vile ni maadui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za jamii kwa upande wa elimu, hivi sasa Mkoa wa Ruvuma una mvua; tungeomba fedha za MMES ziweze kupelekwa katika Sekondari ili Sekondari hizi ambazo zipo kila Kata ziweze kuezekwa ili nguvu za wananchi zisije kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu barabara. Barabara zetu kule ni mbaya sana, hata Mheshimiwa Komba alipokwenda sehemu moja ilibidi gari lake aliache *silence* kwa sababu alichukua gari ambalo linaweza likaenda kule na watu kule walikuwa wanajiuliza; *ligali lidala ligosi?* Yaani hili gari ni dume au jike? Kwa sababu hawajawahi kuona gari!

Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia maeneo ya Mikoa ya Kusini kwa sababu ndipo sasa raslimali kubwa ziliko na hazijawahi kutumika. Naomba tuanze kuangalia Kusini badala ya kuangalia sehemu nyingine katika kipindi hiki kwa sababu uhai na uchumi wa Tanzania unategemea sana Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa kuokoa muda.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa Bungeni, ni vyema basi nikatoa pongezi za dhati kabisa kwa ushindi alioupata Mheshimiwa Rais Kikwete katika uchaguzi uliofanyika. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikupongeze wewe pamoja na Spika mwenyewe kwa jinsi tulivyowachagua. Ni kitendo cha aina yake, kwani wote mlipata kura zote za ndiyo. Hongereni sana. Tuna imani kwamba mtatufanyia kazi nzuri sana ya kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Waziri Mkuu. Waziri Mkuu mimi namfahamu vizuri, tumekuwa naye kwa miaka mitano hapa, lakini tulipata bahati ya kusafiri naye kwenda Misri. Matendo aliyoyaonyesha tukiwa Misri ni ya maajabu sana! Ni Mawaziri wachache sana wanaoweza kufanya hivyo. Kwa ujumbe aliofuatana nao, yeye alikuwa ni mtu wa kwanza kupiga hodi na kuwajulia hali. Ni heshima ya pekee aliyotupatia. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanakamati tulianza kubashiri kwamba huyu mtu anastahili kupandishwa cheo. Mheshimiwa Kikwete amemwona na amempandisha, hongera sana, tuna imani atatufanyia kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaendelea kutoa pongezi kwa sababu huo ndiyo wajibu wangu. Nimeagizwa hivyo na wananchi wa Misungwi nifanye hayo kwa niaba yao. Kuna hao Mawaziri, hakukosea kabisa Mheshimiwa Rais kuwachagua, ni Mwenyezi Mungu amemshushia neema na akawapata hao Mawaziri wetu waliochaguliwa. Hongereni sana Mawaziri na tuna imani mtafanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo alichokifanya Mheshimiwa Kikwete cha kwenda kuwatembelea wananchi wa kawaida Kariakoo ni cha maajabu sana na kimetutia moyo Watanzania wote. Rais anajishusha mpaka kwa watu wa kawaida kuona hali ya chakula ilivyo. Lakini nadhani walishea mawazo na Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka safari moja nimeona picha wamekaa wawili wakiwa *Airport* ya Dar es Salaam wanateta ni mwaka 1995 wakiwa wametoka kuchukua fomu nadhani ya kugombea Urais wakati huo. Wamekuwa wavumilivu na baadaye imefika mahali wamekubali. Nadhani wamezungumza kuachiana wafanye kazi kwa pamoja katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo alichokifanya Mheshimiwa Kikwete na juzi juzi tu kitendo alichokifanya Mheshimiwa Lowassa alipokuwa Meatu cha kwenda kuwaona wananchi wa kawaida jinsi wanavyoteseka ni cha maajabu sana. Alipaswa apumzike ale raha kidogo, lakini bado ameondoka kwenye Bunge hili na kwenda kuangalia wananchi. Mbali ya wananchi, aliamua kwenda kuangalia mpaka mifugo, akachukua fimbo kuangalia hali ya mifugo ilivyo. Hongera sana ndugu yangu Lowassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, hebu nijaribu kujielekeza kwenye suala la chakula. Hali ya chakula ni mbaya sana. Wananchi wa Misungwi wana ukame wa ajabu. Mwaka jana Misungwi hatukupata chakula, mvua hazikunyesha. Skimu yetu ya Igongwa nadhani Mheshimiwa Waziri wa kipindi kilichopita Mheshimiwa Keenja ni shahidi, pale Igongwa hawakupata chakula kabisa. Hali ni mbaya kweli! Tunaishukuru Serikali yetu imetutangazia kwamba hatutakufa na njaa, lakini pia tuendelee kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misungwi tumepata tani 329 kwenye awamu ya kwanza, tumegawa kwenye kaya ndani ya Vijiji 44, hali ni mbaya mno. Kila kaya iliweza kupata wastani wa kilo 16 au kilo nane, wataishije wananchi hawa? Serikali mtuangalie. Awamu ya pili mmetupatia tani 436, bado kuna Vijiji vingine kama 34 hivi, Misungwi ina Vijiji 78. Mabuki katika awamu ya kwanza haikupata, Misungwi hawakupata, Misasi hawakupata, Usagara hawakupata na sehemu nyingine ndiyo zenye wakongwe zaidi. Nashukuru awamu hii watapata, lakini hakitoshi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, muwaangalie wananchi wa Misungwi wana hali mbaya mno, chakula ni tatizo. Waliopata mahindi tarehe hizo mpaka leo hii hawana kitu, kilo nane au 16 watafanya nini? Ninaiomba Serikali iwahudumie wananchi wa Misungwi, wananchi wa Kwimba na Watanzania wote kwa ujumla walio na matatizo ya njaa wapewe chakula.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kupendekeza mambo manne hivi ya ugawaji wa chakula. Aina ya kwanza, kitolewe chakula cha bure kwa watu wasiojiweza. Mimi nilishiriki kwenye matatizo ya kugawa chakula pale Inonelwa, nimekuta akinamama

wameshindwa kununua gunia la mahindi. Nilinunua kwa niaba yao na wakaniomba mimi ndiyo niwe mgawaji wao. Kilo 8 kwa kila mtu ni hali ya shida kweli!

Aina ya pili ya chakula kile cha Shilingi 50, kitolewe upesi na kwa wingi. Aina ya tatu, tunaomba tupewe chakula cha kazi. Wananchi wapo lakini wamekosa namna ya kufanya kazi, mvua hainyeshi. Kama chakula cha kazi kitakuwepo, watafanya kazi za maendeleo na baadaye watalipwa chakula. Watu wa Caritas wameanza kuleta pale ng'ombe, wamewapa kazi ya kuchimba lambo. Watu wamelipwa chakula na angalau wameweza ku-*survive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana kitolewe chakula cha kazi ili maendeleo mengine yasisimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina ya nne ya chakula ni chakula kinacholetwa na wafanyabiashara. Unapoambiwa Shilingi 300 unaona ni hela kidogo sana, izidishe mara gunia, kwa maana ya kilo 100 utakuta ni elfu 30. Mwananchi wa kawaida hawezi kupata elfu 30 jamani. Serikali iendelee kuzungumzia na wafanyabiashara kama alivyofanya Mheshimiwa Rais tuwaombe wawe na huruma.

Aidha, Serikali iwape ruzuku kiasi fulani angalau bei ishuke ije kwenye Sh.200/= kwa kilo, angalau itakuwa nafuu kidogo kwa wananchi. Tunaomba sana tufanyiwe hilo ili angalau tuweze kuwavusha wananchi wetu na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwenye suala la miundombinu. Katika ugawaji wa chakula bado tuna matatizo ya barabara zetu. Ipo barabara toka Misasi kwenda Mbalika, ilitengewa pesa kama Shilingi milioni 40 na mkandarasi aliishachaguliwa tayari, lakini mpaka leo haijatengenezwa. Chakula kwa ajili ya watu wa Kasololo kwenda Matale kimeteremshwa Nduha wakafata wenyewe kwa mguu, ni mateso. Pesa zipo, mkandarasi yupo, lakini hajaja kujenga.

Naomba Serikali ilifanyie kazi hilo. Namjua Dr. Mahanga kazi zake na yeye inaonekana ana kasi mpya. Kwenda kukaa kwenye *Ferry* pale sijui alienda saa ngapi? Hiyo kasi basi iendelee mpaka huko Misungwi ili aweze kutuletea neema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la hali ya usalama nchini. Hali bado siyo nzuri. Tunavyosikia matangazo kwa jinsi Dar es Salaam wanavyovamiwa, hiyo ni rasha rasha kwa huko, hali ni mbaya Misungwi. Tarehe 20 mwezi wa Kwanza mfanyabiashara mmoja pale Misasi amevamiwa saa mbili za usiku, amepigwa risasi kifuani akafa hapo hapo, wakaendelea kurusha risasi hewani. Wananchi wa Misasi walijitahidi, lakini hawakufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, tulishaomba vitendea kazi, gari iliishanunuliwa na kuelekezwa iende Misungwi, mpaka sasa hivi sijui iko wapi! Waziri

wa kipindi kilichopita tulimweleza pale Misungwi. Tumepiga simu Misungwi hatujapata msaada wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wananchi wa Misungwi wamekamata majambazi wa Misasi, wamekamata bunduki tatu, tumepiga simu, lakini ni mkweche wa gari uliopo Misungwi, gari mpya sijui bado iko wapi! Hatutendewi haki sisi wananchi wa Misungwi. Tunaomba gari yetu iliyonunuliwa kwa ajili ya Misungwi ifike Misungwi isaidie wananchi wa eneo hilo la Misungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nigusie kwenye fidia za watu ambao wamekumbwa na kazi nzuri ya kujenga bomba kwa ajili ya kupeleka maji Kahama na Shinyanga. Ninaipongeza Serikali kwani imeanza kulipa kwa awamu ya kwanza Shilingi milioni nane na sehemu kwa ajili ya watu 38, milioni mbili kwa ajili ya watu 12 na jana tu baada ya kusumbuliwa na watu wengi sana, kati ya Ilalambogo, Isenengeja, Ibinza na Mwawile zaidi ya watu 197 walikuwa wanadai fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mkuu wa Wilaya yetu ya Misungwi Ndugu Masaga ana *style* ya kuwalipa, amewaita na anaendelea kuwalipa kwa *style* yake zaidi ya milioni 38.

Kwa hiyo, Serikali yetu inafanya kazi nzuri ya kuwafidia wananchi wetu. Lakini bado kuna kipande kingine cha kutoka Mwawile kwenda Mwamashimba, wananchi wana matatizo sana kwenye eneo hilo, wafidiwe upesi ili waweze kupata hizo pesa kwa ajili ya kununua chakula.

Pia, kuna Shilingi milioni nane na sehemu, ziko pale Wilayani Misungwi, hazina maelekezo zifanye nini. Tunaiuliza Wizara, hizi pesa ni kwa ajili ya nini maana hazina maelekezo. Kwa hiyo, Wizara ishughulikie upesi ili angalau tuweze kuona kwamba hizo pesa ni za fidia au ni za shughuli gani, ziko pale Misungwi zinasubiri shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nasimama kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo naiunga mkono asilimia zote. Lakini kabla sijaenda huko, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa ushindi mzuri, mkubwa, mnono alioupata pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Waziri wetu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze kwa namna ya pekee hawa Viongozi wetu Wakuu wa Serikali kwa namna tofauti kabisa. Katika muda mfupi sana ambao wameanza kufanya kazi wameonyesha maajabu na kwamba Watanzania bado wanashangaa.

Mheshimiwa Rais kwa taarifa za jana kwa taarifa ambalo tunalo la njaa kuonekana mitaani akiangalia, akiba ya chakula kwenye masoko ya kawaida ya wananchi

wa chini, Watanzania wengi wamefurahi na wamejua moyo wa Mheshimiwa Rais na akiwa anakubaliana na Watanzania hawakufa na njaa. (*Makofi*)

Pia, Mheshimiwa Waziri Mkuu, juzi tu alikuwa Mkoani kutembelea maeneo hayo ambayo yana matatizo ya njaa na ukame na anakwenda chini kabisa anajishusha kwa wananchi kule kijijini. Nimeona picha moja walikuwa wanamchezea ngoma sehemu za Bariadi huko. Kwa hiyo, wananchi wana imani sana na wanapenda sana kumwona kiongozi wao wanasahau hata shida yao wanamwonyesha furaha hiyo, naomba viongozi muendelee hivyo hivyo kwa kasi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mawaziri, Wakuu wa Mikoa ambao tayari wameshateuliwa kuchukua nafasi hizo. Lakini niwapongeze sana Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe Naibu Spika, kwa kuteuliwa kuwa viongozi wetu hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi sasa kwa kasi hii kali sana ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, inawapa changamoto kubwa viongozi waliofuata wakiwemo Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwa bahati mbaya sana tumeanzia pabaya, tumeanzia kwenye njaa.

Kwa kasi pekee iliyoonyeshwa na viongozi kuhusu tatizo la njaa, sina hakika kama kasi hii wataiweza wafuatao na inabidi wafanye hivyo kwa maana Mawaziri na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwa mfano sitashangaa kuona kwamba pengine Waziri wa Kilimo na Chakula, naye alikuwa hajafika kule sokoni kujua *stock* ya chakula, pengine hata hapa hapa Dodoma, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, pengine naye alikuwa hajafikiria kufanya hivyo, pengine hata Mkuu wa Wilaya ikiwemo Wilaya yangu pengine hajafika kuona vile Vijiji ambavyo havina chakula na ukame unaotisha. Sasa wafanye hivyo kwa sababu imeshaonyeshwa njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka na mimi nijielekeze kwenye tatizo la njaa. Lakini kabla sijafanya hivyo napenda niwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Nyang'hwale kwa kunichagua tena kwa mara ya tatu kuwa Mbunge wao. Napenda niwashukuru sana. Lakini napenda niwape pole sana kwa tatizo letu kubwa la njaa pamoja na ukame ambalo sasa hivi linatusibu hususan katika Jimbo langu katika Wilaya ya Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika hapa kidogo kuona kwamba kwenye mgao wa kwanza Wilaya ya Geita haikuwemo. Lakini nataka nieleze kwamba Jimbo la Nyang'hwale lina hali mbaya sana ya njaa. Jimbo la Nyang'hwale hali yake ya hewa siyo nzuri, maana yake inapakana na Wilaya ya Misungwi, inapakana na Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Wilaya ya Kahama. (*Makofi*)

Haya maeneo yote yana hali mbaya ya njaa. Wilaya ya Misungwi tayari imepata mgao huu wa kwanza na wananchi wangu wamekuwa wakiniuliza kwamba kwa nini sisi hatumo kwenye mgao wa kwanza? Chakula kiko wapi? Wanaona Misungwi majirani zetu wanapewa lakini wa Nyang'hwale kule Tarafa ya Msalala, Tarafa ya Nyang'hwale

hawamo kwenye mgao wa kwanza. Sasa hapa nina mashaka pengine takwimu zinazoletwa na wataalam, ambao kwa muda mrefu sana hasa wataalam wa Idara ya Kilimo wamekuwa wakikaa tu ofisini na kusubiri takwimu au kugeuza hizo hizo zilizoko kwenye mafaili na kuzileta huku Serikalini. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kufanya makosa kwamba Wilaya ina chakula kumbe haina chakula. Au eneo fulani lina chakula kumbe halina chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi kulikuwa na njaa, mimi niliwahi kumwona Waziri anayehusika lakini baadaye Mkuu wa Wilaya kwa taarifa alizokuwa ameletewa, alizileta huku akasema Wilaya ya Geita ina chakula, lakini sehemu ya Wilaya ya Geita ambayo ni Jimbo la Nyang'hwale Tarafa ya Msalala na Nyang'hwale hapakuwa na chakula. Kwa hiyo, sasa nina wasiwasi na pengine takwimu hizi pengine ndio zimetupeleka kwa mgao wa kwanza kutokupewa wananchi wa Nyang'hwale na wananchi wa Msalala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya huku hali ni mbaya sana. Sasa hivi zaidi ya nusu wanaume katika kaya katika Tarafa ya Msalala Nyang'hwale hawapo kwenye kaya zao, wameenda maeneo yenye nafuu wa chakula kutafuta chakula na wanakwenda kule sasa hawana fedha. Kwa hiyo, wanakwenda kule kufanya kazi kwa wananchi wenzao ili wapate chakula. Kule kazi zilizoko ni za kulima na kulima sasa hivi haiwezekani kulima wote wale kwa sababu mvua hazinyeshi vizuri kwa hiyo wamekuwa kule wakisubiri kuzunguka na kutangatanga kutafuta ni wapi wanaweza kubahatisha kibarua au kufanya kazi ili apeleke nyumbani kwenye familia yake kunusuru maisha ya watu. Sidhani kama taarifa za Wilaya, Taarifa za Idara ya Kilimo zimeeleza hali halisi juu ya matatizo haya. Nashawishika kusema kwamba Serikali ikubali taarifa wanazotoa sisi Wabunge kwa sababu ndio hali halisi, hali si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kiletwe chakula cha msaada kile chakula cha kupewa wananchi bure wasio na uwezo kabisa na kile chakula cha Shilingi 50 kwa kilo na kile chakula ambacho kinauzwa kwa bei ya kawaida. Lakini kwa sababu mvua pengine zinaweza zikanyesha ni vizuri chakula hiki hicho kikaletwa na mbegu za mtama serena au pengine uwele, mazao ambayo yanaweza kuwanusuru wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale na wananchi wa Geita katika hali hii ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipendekeze mambo yafuatayo kwa Serikali katika kuangalia hii hali:-

Kwanza kabisa watendaji wetu huko chini wafanye kazi kwa kasi ambayo Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wameonyesha. Nakumbuka wakati wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi walikesha, siku mbili hawalali wana kazi ambayo waliifanya kwa utaratibu. Kwa sasa hivi watendaji wa kata, kuanzia kule Wilayani wafanye kazi kwa kasi ya Tume ya Uchaguzi, wakeshe wakitafuta taarifa na kutekeleza yote ambayo yanaamuliwa na Serikali ili wananchi wasife njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba Serikali nayo kwa upande wake izipokee taarifa hizi kwa haraka na ifikishe mahali panapohusika kwa hali ya dharura.

Tatu, Serikali ipeleke chakula haraka kwenye maeneo hasa yanayosemewa na Wabunge hapa ndani hata kama takwimu hazijafika au hazijakamilika, pelekeni chakula haraka likiwemo Jimbo la Nyang'hwale Tarafa ya Msalala na Tarafa ya Nyang'hwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba ugawaji wa chakula hiki ambao nilikuwa naomba sana Serikali, ihakikishe kwamba kinawafikia wananchi kwa maana ya Kata, kifike kwenye Kata pamoja na mbegu zifike kwenye Kata au kijiji, Serikali isimamie hilo. Kuwe na utaratibu unaotakiwa wa kufuatilia. Naomba hapa sana Waheshimiwa Madiwani wahusishwe. Kuna mambo mengine madiwani wakiingia na Wabunge wanasema ahaa mnaingia jikoni nyinyi wana siasa. Kwenye njaa hakuna siasa. Kwa hiyo, mturuhusu twende kule tutasimamia na Madiwani wasimamie na wananchi wale watendaji wabovu. Wakiwajua watendaji wabovu wawaseme kwa viongozi wao kwa Mkurugenzi na kadhalika. (*Makofi*)

Najua kuna tatizo kwenye Halmashauri, kuna hili dude linaitwa Tume Taa ambalo linalinda sana Watumishi wa Halmashauri wanaofanya maovu. Madiwani wanasema huyu hatufai, au Mkurugenzi anasema huyu mtumishi hatufai lakini akienda Tume Taa anasema anarudishwa. Sasa tunaomba Tume Taa, muwe wenzetu mnafanya kazi Tanzania hii na kwa niaba ya Watanzania mheshimu maamuzi ya Halmashauri zenu kwa sababu kule ndiyo kuna matatizo na wao ndiyo wanaojua Watumishi wabovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependa kusema kwa hali tuliyonayo ngumu ile michango na misako isiyo ya dharura kwa sasa hivi kwenye maeneo yenye njaa, ingesitishwa kwa muda. Wananchi hawawezi kuwa na uwezo wa kulipa michango kwa kidogo walichonacho waruhusiwe waweze kununua chakula ili wasife kwa njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa *NGOs* kwenye maeneo zinazofanya kazi watu binafsi, Mashirika ya dini kama vile *CALITAS* na hata wenye migodi hawa kuna wakati fulani kuna hela, kuna mafungu ya kusaidia jamii wanazofanya kazi nao sasa hivi wajielekeze kutusaidia kutununulia chakula.

Lakini pia watu binafsi, wapo wafanyabiashara na hususan wa Nyang'wale wanaokaa nje ya Jimbo, watumishi mbalimbali wananchi mbalimbali, mje pale tusaidiane mwenye uwezo wake kule aje, mje tusaidiane kusaidia wananchi hawa ambao wanasumbuka sana, najua mna moyo wa kufanya hivyo na mlionyesha hivyo baadhi yenu wakati wa uchaguzi mlikuja kule na sasa hivi njooni sasa wale waliokuwa wanawapigia kura wale wana njaa njooni na hela zenu mlizonazo tusaidiane wananchi wale wana njaa ili wawapigie kura tena mwaka 2010. Njoo tusaidiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kwamba mji wa Geita una shida ya maji, sasa hivi ndoo ya maji inanunuliwa kwa Shilingi 100 mpaka 150. Ni maji ambayo siyo salama. Maji ambayo yana *typhoid* yana wadudu na matatizo mengine yanayosababisha magonjwa ya tumbo. Mji wa Geita, umefurika kwa sababu ya kuwepo

mgodi wa Geita wa dhahabu na watu wa mgodi tumejaribu sana kuwaambia na sasa hivi wanasema wanachimba visima kusaidia tu tatizo dogo la maji.

Kwa hiyo, kwa kuwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa Waziri wa Maji na tatizo la Geita analifahamu naomba sana sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo tatizo ambalo unalifahamu kwa watu ambao ni zaidi ya 100,000 ambao hawana maji ambao wanategemea mashimo waliyochimba kwenye *plot* zao wanaita visima vifupi wakati ni mashimo, maji ambayo hayana uhakika na hayatoshelezi, basi Serikali itufikirie sana. Tunashukuru tunapongeza Kahama na Shinyanga wamepata maji ambayo yanatoka Ziwa Victoria na sisi tunaomba maji kutoka Ziwa Victoria. Tunashukuru sana. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia hadi hii leo niko ndani ya Bunge hili Tukufu. Lakini kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibakwe ambao kwa dhati yao wameona kwamba nastahili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu za kwanza ni kwa Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa na wa heshima alioupata. Lakini pia pongezi zangu za pili ni kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Amani Abeid Karume kwa ushindi mkubwa wa kishindo na wa heshima kwa CCM aliopata, hakuna namna yeye ni Rais tu na ataendelea kuwa Rais mpaka mwaka 2010. (*Makofi*)

Lakini pia, nichukue nafasi hii, kwa kukupongeza wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa kuchaguliwa na sisi Wabunge na kwa umakini mkubwa ambao unauonyesha katika kuifanya kazi yako hii. Lakini pia unifikishie salama hizi kwamba pia nampongeza Spika wetu wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anaiendesha kazi hii kwa uzuri na hakika ananikosha nakusudia kuiga baadhi ya vitu kwa sababu ana-*summarize* mambo na anatupeleka kwenye *target*, nampongeza sana. (*Makofi*)

Lakini pia niwapongeze sote tuliongia katika Bunge hili ninawapongeza sana kwa namna ambayo wote mmeweza kupitia katika vizingiti hivyo na kufika ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kama walivyofanya wenzangu ningependa nichukue nafasi hii kupongeza hotuba nzuri na yenye kiwango cha hali ya juu iliyotolewa na Mheshimiwa Rais, wakati akihutubia Bunge hili Tukufu. Mimi binafsi kwa hakika ninapata faraja kwa hotuba aliyoitoa maana imevaa kikamilifu katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa lugha rahisi.

Lakini pia, ninayo baadhi ya maeneo ambayo nitayazungumzia, lakini nianze na lile ambalo hasa limenisukuma na mimi nipate kuomba nafasi hii ya kuchangia hotuba hiyo. Tangu lianze wazo la kuhamishia Makao Makuu Dodoma, ilikuwa ni baada ya uhuru na nina hakika wakati huo mimi nilikuwa bado sijazaliwa. Hadi hii leo tangu ile *implementation* yake ilipoanza ilianza miaka ya mwanzo mwa 1969. *CDA* ilianzishwa

kwa kutumia sheria ya Mashirika ya Umma na kwa *CDA Establishment Order* ya mwaka 1973 kwa kazi hii. Kazi kubwa ya kwanza ya *CDA* ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Makao Makuu yanahamia Dodoma. Niseme kutoka Dar es Salaam maana yake Ofisi nyingi za Serikali ziko Dar es Salaam. Lakini hii bado mpaka leo haijawezekana. (*Makofi*)

Mimi nadhani kwa kuwa sasa ni miaka mingi imepita, Serikali ni vizuri ionyeshe msimamo wake, maana yake naona hata zile dalili za kwamba ile nia ya dhati ipo ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma kama vile inapungua. Ndiyo maana suala hili halizungumzwi sana.

Maana Wizara zilizoweza kuhamishiwa hapa mpaka sasa ni chache sana na pengine zinaweza zikawa ndizo hizo kwa kipindi kirefu na hivyo nia hii inaendelea kufutika siku hadi siku. Mimi ningependa nishauri Serikali kwamba kipindi hiki cha sasa kama kweli tuna nia sababu zile zile zilizosababishwa tukusudia kuhamishia Makao Makuu Dodoma ni kwa sababu ya kuwezesha utawala bora basi Serikali iweke udhati wake katika hili na tuhakikishe kwamba kasi ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma inaongezeka kwa ari mpya na nguvu mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili katika mchango wangu ni juu ya suala la chakula. Kuzungumzia njaa sasa imeshakuwa ni *fact* kwamba kila mmoja anajua tayari nchi yetu imekumbwa na balaa la njaa. Lakini mimi niende zaidi ya hapo na nizungumzie namna ambavyo suala la njaa linashughulikiwa katika *level* ya kuanzia Mikoa, Wilaya, Kata, Tarafa hadi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tangu tulipopata mgao wa kwanza na wa pili tukatangaziwa tangu tukiwa Dar es Salaam kwenye semina kwa mfano Wilaya ya Mpwapwa tumepewa tani 135 hadi kufikia juzi chakula hicho kilikuwa bado hajasambazwa kwa walengwa. Sasa njaa tafsiri yake jamani ni hatari maana yake njaa ni kifo.

Lakini njaa inapochukuliwa kama ni mtu tu ukimvalisha shati akivaa basi leo amevaa anakaa hivyo hivyo kwa siku hata wiki au ngapi ni tofauti na njaa kwa sababu tunaposema kuna njaa maana yake watu wanaumwa njaa, basi uharaka huu ni vizuri ukawa mkubwa hasa katika *level* hizo nilizozungumzia kuanzia Mkoa, Wilayani hadi Tarafa na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, hata namna ya mgao wa chakula ambacho tumepata kwa kweli hakitoshi, hakitoshi kwa sababu kwa mfano awamu hii ya pili Vijiji vilivyopata chakula katika jimbo langu ni Mtera, Kisima, Singonari, Lukole na awamu ya kwanza vilipata Chelendu na Winza. Vijiji hivi ni miongoni mwa Vijiji 44 vya jimbo langu. Sasa hivi hawa wengine wana njaa, hawa hata wakipata inasaidia nini. Sasa kama ni *operation* basi tungeona u-*busy* kwamba magari yanakwenda yanachukua chakula, ingekuwa tunaona kwamba hili ni janga.

Lakini inaonekana kwamba kwa kweli ni tathimini, tathimini. Kama tathimini zimekamilika basi kwa kweli iwe *operation* kwamba chakula kipelekwe kwa kasi kubwa na kifike kwa walengwa kwa haraka sana. Maana yake hizi *break*, mkoani *break*, Wilayani sijui Kamati ya Maafa na kadhalika izungumze wakae wapange wafanye hili. Kwa kweli huu utaratibu utasababisha watu wetu wafe kwa njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Tanzania ni nzito sana kwamba hakuna atakayekufa kwa njaa. Sasa ahadi kama hii inapokuwa inapata vizingiti visivyo rasmi kuchelewesha mara oho hela hakuna, unajua mimi sijajua pesa ya kufanya hivi kwa kweli mimi nadhani hili liangaliwe na Waziri anayehusika na ahakikishe kwamba inaposemwa chakula kimetolewa basi ichukue siku moja, mbili kimeshafika kwa walengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mawasiliano. Mawasiliano ni tatizo katika sehemu kubwa ya nchi yetu. Lakini tuchukue zile ambazo zinakuwa na tatizo kubwa zaidi la kugawa hata kati ya Tarafa na Tarafa. Kwa mfano katika jimbo langu la Kibakwe Tarafa ya Rudi hawawezi wakapitia ndani ya jimbo kupitia Kibakwe kuja Mpwapwa lazima wapitie Dodoma. Wakitoka Dodoma ndiyo waende Mpwapwa, wakitoka Mpwapwa ndiyo waende Kibakwe.

Kwa hiyo, Makao Makuu ya Jimbo hakuna pale wanaopita kutoka kwenye hilo Jimbo moja. Tatizo kubwa pale ni korongo moja la Chitala. Chitala limegawanya Jimbo la Kibakwe na watu wanapitia Dodoma ili kuweza kufika Mpwapwa na kisha wafike Kibakwe. Sasa hili ni tatizo na hasa kwa Wafanyakazi ambao tunafahamu kwamba mishahara yao ilivyo na hivyo wanapozunguka hivyo wanamalizia fedha yao nyingi ya mshahara katika safari na siyo katika kukidhi mahitaji yao muhimu. (*Makofi*)

Mimi ningeomba Serikali, Waziri wa Miundombinu tuangalie na sisi tuweze kupata daraja la Chitala. Lakini pia hata namna ambavyo barabara zetu za Vijijini zinavyoshughulikiwa kwa kweli ni kama tunasafisha barabara maana kuziambia Halmashauri zitengeneze barabara ni kama tunasafisha tu, wanapitisha tu greda wanasafisha lakini siyo kutengeneza barabara. Halmashauri inapewa milioni labda 16 mnagawana pengine katika Wilaya, Majimbo mawili milioni 5.5 inatengeneza barabara ya wapi? (*Makofi*)

Mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais Kikwete, ameahidi kwamba ataongeza mfuko wa *Road Fund* na pengine hii inaweza kutusaidia. Lakini niseme tu kwamba kwa kweli barabara maana yake ni daraja na barabara inatengenezwa kwa kuchukua kifusi pembeni na kuweka juu pale kuweza kuinyanyua juu na siyo kwa kukwangua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kilimo. Kilimo cha Tanzania ni cha kinadharia sana, kwa sababu maneneo yanasemwa sana, maana mmezungumza kutokea uhuru na sisi tuliokuwa tumezaliwa baada ya uhuru tumekuja na sisi tumeingia humu na sisi tunazungumza tu. Tutaendelea kuzungumza mpaka lini? Kilimo chetu ni cha kinadharia mno. (*Makofi*)

Haiwezekani trekta inayotakiwa kwenda shamba inabeba takataka Dar es Salaam, halafu tunasema sisi tunataka ku-*manifest* kilimo. Yaani ni faida kwa trekta kubeba uchafu Dar es Salaam kuliko kwenda shambani kulima kijijini. Sasa hii kwa kweli inaonekana kama hatuko *serious*. Mimi niseme kwamba ningeomba Serikali ya sasa ya Awamu ya Nne, itilie mkazo kilimo. Kwa mfano, nilikuwa naongea na wananchi wananiambia hata mbegu, wanaisikia tu kwenye radio kuna mbegu, ukienda Kibakwe, pale pale hakuna mbegu, ukija Mpwapwa hakuna mbegu haziko.

Sasa unasema mwananchi huyu alime, analima vipi? Anapanda nini, hakuna mbegu bora. Mabwana shamba wanaokwenda kule tunakwenda kuwaua tu kule kwa sababu unampeleka kule hana kazi hana anachofanya anabakia anakunywa komoni mpaka afya inakuwa mbaya anakufa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningesema mchango wangu juu ya suala la kilimo kwa kweli mkazo na mtazamo mpya juu ya kilimo ufunguke sasa ili uweze kuleta manufaa na tija kwa sababu ndiyo njia pekee inayoweza kutukomboa sisi Watanzania na kwa sababu wengi tunaishi Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu nilitaka nimalizie kwa kusema ninaomba sana hizi shule zetu za kata tulizozianzisha wengine tuna shule za namna hiyo tu, hatuna shule zile za wakati ule wa zamani. Kwa hiyo, katika shule hizi angalau walimu wapelekwe kwa *speed* inayostahili kwa sababu hayo majengo yapo *form one* na *form two* wameanza kwa hiyo, wapelekwe walimu kwa kasi, shule ina mwalimu mmoja tu, atafanya nini?

Matokeo yake kule tutabakia wote hatukusoma. Huu usomi tuangalie kisomi maana kuna wengine huko hatukusoma. Mimi mwenye *degree* moja naonekana ndiyo msomi wa kutisha, lakini hapa kuna ma-*doctor* wako humu. Lakini ningependa kusema tu kwamba Serikali sasa na hasa hii Wizara hii ya Elimu na mafunzo ya ufundi, ningependa kushauri kwamba kwa kweli watie mkazo mkubwa katika kuhakikisha kwamba wanaajiri walimu kwa haraka sana. Hata afyazahanati zimejengwa kila kitu safi, lakini madaktari hakuna. Unakuta nesi ndiyo anaye- *prescribe*, kwa kweli hii si sawa na ningependa niseme tu kwamba hata Wizara ya Afya, pia ihakikishe inaajiri madaktari wasomi wake wengi wanatafuta kazi. Walimu wako wengi wanatafuta kazi. Mimi niseme tu jana nilisema mtu anachangia kwamba tukachukue walimu Uganda sijui mimi najua tunao walimu wengi wanatafuta ajira. tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunitamka na mimi niweze kuchangia kwa mara yangu ya kwanza katika Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote humu ndani hadi leo hii tuko hapa na tunaweza kuchangia mada mbalimbali. Pia napenda niwapongeza Watanzania wote kwa ujumla walivyojitokeza katika chaguzi zetu na kumchagua Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwenye Uchaguzi wa kihistoria ambao haujawahi kutokea katika nchi yetu. (*Makofi*)

Pia napenda nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuliyempitisha kwa kishindo na hatimaye kuweza kuapishwa kuwa Waziri wetu Mkuu. Hali kadhalika nampongeza Mheshimiwa Spika kwa ushindi wake wa kishindo na wewe mwenyewe ukiwa mwanamke wa kwanza kuwa Naibu Spika wa Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Vile vile napenda niwashukuru na niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Bila kusahau wapiga kura wetu hasa wanawake wa Mkoa wa Pwani, walionichagua kuwa mwakilishi wao, vile vile wanawake wa Tanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba Uchaguzi wa mwaka huu ulikuwa Uchaguzi ambao umesimamiwa kidedea na wanawake katika kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nichangie mambo mawili matatu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ambayo naiunga mkono hiyo hoja kwa asilimia mia moja.

Kwanza, napenda nianze na suala la Afya. Katika awamu ya tatu. Serikali yetu ilijitahidi kwa kila hali kuhakikisha huduma za afya zinafika mpaka Vijijini.

Lakini nataka nikuhakikishie tatizo kubwa lililokuwa katika hizo zahanati au vituo vya afya au hata kwenye hospitali zetu za Wilaya ni kwamba kuna uhaba wa dawa na uchangia ambao unakuwa ni kikwazo kwa wananchi wetu ambao hawana uwezo hasa akina mama. (*Makofi*)

Sisi tunazungumzia suala la maisha bora kwa kila Mtanzania, lakini bado unakuta vifo vya akina mama na watoto ndiyo vingi kwa sababu wengi wao hawana uwezo, wengine wanakwenda kwenye vituo vya afya au kwenye zahanati zilizokuwa kwenye maeneo yao wanashindwa kuchangia au wana uwezo wa kuchangia lakini unakuta dawa hamna au daktari mwenye fani ya matatizo hayo mwenye uwezo wa kuwahudumia akina mama anapelekwa tu labda *medical assistant* au mhudumu wa afya ndiye anapewa kazi ya kuwasaidia akina mama.

Sasa mimi nilikuwa naomba Wizara husika ijaribu kuliangalia suala hili ione itasaidia vipi katika kuwakomboa akina mama na hasa watoto ambao tunategemea kuwa ni viongozi wetu wa kesho kama siyo leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama hao hao bado wana matatizo makubwa sana, akina mama hao ndiyo wa kwanza katika kuchangia kuhudumia wazee, watoto, au kuhudumia kila aliyekuwa karibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa naona ni vema suala hili likaangaliwa kwa makini na kuweza kulipatia ufumbuzi. Mama huyo huyo ana mzigo mkubwa wa kutafuta maji. Suala la maji kwa nchi yetu bado ni tatizo kubwa. Mimi natoka Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Pwani, umezungukwa na mito, tuna Mto Ruvu, tuna mto Rufiji, lakini cha kusikitisha baadhi ya kata ambazo nyingine ziko jirani kabisa na mito hiyo hazina maji mpaka sasa hivi.

Sasa ni vema suala hili Serikali ikaliangalia kwa makini kuweza kutafuta mikakati kabambe ya kuweza kuchimba visima vya kutosha, kuwe na uvunaji wa maji ya mvua pamoja na kwamba mwaka huu tuna matatizo ya mvua, lakini hicho kisiwe kigezo ni vema tukaangalia ni jinsi gani tunaweza kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu ya namna hiyo ili kuweza kusaidia katika suala la kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachotaka kuchangia ni suala la elimu, tunazungumzia hakuna maendeleo bila ya elimu lakini baadhi ya kata zetu katika mikoa mbalimbali hazina shule za sekondari na tumejenga shule nyingi za msingi ambazo zimetoa watoto wengi wa kwenda shule za sekondari wengine mpaka leo hii hawajapata hiyo nafasi.

Nataka tu nitaje baadhi ya mikoa ambayo ina uhaba wa shule pamaja na jitihada za wananchi wanaochangia katika kujenga hizo shule, lakini mimi naomba Serikali iliangalie suala hili ione kama kuna uwezekano wa kuwasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kujenga shule nyingi za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa hiyo ni Dar es Salaam ambayo ina idadi kubwa ya wakazi lakini mpaka sasa hivi ina shule za sekondari 21, mkoa wa Lindi una sekondari 26, Pwani ina sekondari 35, Rukwa ina sekondari 38, Tabora ina sekondari 35, Kigoma ina sekondari 42 hatuwezi kufika, la msingi tuombe Serikali iangalie na kutoa kipaumbele kwa mikoa ambayo mpaka sasa hivi ina sekondari chache ili tuweze kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo kwa kuwapa elimu watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazingatia sana suala la kuokoa muda naomba nifike kwenye *agenda* yangu ya mwisho kuhusu suala la chakula. Tunazungumzia suala la chakula lakini hatuangalii maeneo mengine, tumeweka msisitizo katika kugawa chakula tunajua wananchi wetu huko waliko wengi wao ni maskini kipato chao ni kidogo. Asubuhi watoto wanaamka wanaenda shule hatujui kama watoto hao wamepata riziki asubuhi ya kuweza kuwafikisha wao mashuleni na kusoma, ni vema tuangalie na kuweka mkakati angalau turudishe ule mtindo wa zamani, tupeleke misaada shuleni wapikiwe uji watoto ili na wao wachangamke waweze kupata masomo vizuri, tusiangalie tu kwenye majumba tuangalie na mashuleni ambako watoto wetu wanakwenda kusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mimi sijajua utaratibu uliowekwa na Serikali katika suala la ugawaji wa hivi vyakula vinavyopelekwa katika mikoa. Mimi ninavyofahamu madiwani na Waheshimiwa Wabunge ndio watu wa karibu sana na wananchi, sasa sijui kwa kiwango gani madiwani na Waheshimiwa Wabunge wameshirikishwa katika suala la ugawaji wa vyakula. Watendaji wapo pale kesho, kesho kutwa wanaweza wakapata *transfer* lakini lawama zote atakayebeba ni diwani na Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwe makini katika suala hili, tuangalie ni jinsi gani tutaweza kufuatilia suala la ugawaji wa chakula na tuone chakula hicho kinawafikia wahusika kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa Bungeni hapa tarehe 30 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibiti wilayani Rufiji kwa kuweza kunichagua mimi kuwa Mbunge wao na kwa kuweza kumchagua kwa kura nyingi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kama walivyotangulia wenzangu kuwapongeza viongozi wote waliochaguliwa katika awamu hii ya nne kuanzia Waziri Mkuu, Mawaziri pamoja na sisi Wabunge na Madiwani kule tulikotoka. Lakini mimi nianzie kwa kuchangia suala zima la elimu na hasa nianzie na elimu ya msingi lakini niseme tu kuwa ninaunga mkono hoja ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake aliyotoa tarehe 30 kuanzia ukurasa wa 40 hadi 42 alikuwa anazungumzia ni namna gani awamu ya nne inavyotaka kuboresha elimu kuanzia ya msingi, sekondari na mpaka elimu ya Chuo Kikuu. Sasa sizungumzii sana elimu ya msingi kwa sababu kwa kiasi kikubwa imeboreka, mimi napenda kuzungumzia elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu ya sekondari shule nyingi zimefunguliwa na wananchi na hazikuanzia tu mradi wa MMES ulipoanza, zilianzia huko nyuma karibuni kuanzia miaka ya 90 na kitu mpaka kufikia mwaka 2005. Lakini mimi kama Mbunge nilitaka kuona matokeo ya shule hizi ambazo wananchi wamezianzisha, mara nyingi shule hizi ambazo zimeanzishwa na wananchi shule za kutwa matokeo yake ni mabaya sana, si matokeo mazuri na ndio maana yamemvutia Rais mpaka kuamua katika moja ya vipengele ambavyo alivyoviweka katika hotuba yake ni kuboresha elimu, elimu yetu iwe bora zaidi, kuna kasoro katika elimu lakini iwe bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule zetu nyingi za sekondari ambazo zimeanzishwa na wananchi mara nyingi zinawakatisha tamaa baadhi ya wazazi ambao wanawatoa vizuri watoto wao kuwenye shule za msingi, walimu wetu wa shule msingi wanafanya kazi kubwa sana, kazi nzuri.

Lakini wanapofika sekondari matokeo yake wakifika kidato cha pili zaidi ya asilimi 60 au 70 ya wanafunzi hao wanafeli, wazazi wametoa fedha zao nyingi kuwasafirisha wanafunzi wao kuwapeleka kwenye hizo shule, lakini matokeo yake wanarudi wote huku nyumbani wengine wanarudi kwa ujauzito, wengine wanarudi kwa kushindwa mtihani kutokana na sababu kubwa ya kutokuwa na walimu. Unakwenda kwenye shule ya sekondari ina wawili *form one* mpaka *form three*, hivi walimu wawili watafundisha namna gani mikondo miwili ili kuwa-*keep busy* wale watoto kila siku ya Mungu waweze kupata vipindi ambavyo vitakavyowafanya wasishughulike na masuala mengine, hawawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna jitihada kubwa sana za kuanzisha shule zetu hizi za sekondari ambazo ni za wananchi za kutwa katika kila kata. Sasa ujenzi wa shule za seondari bila ya kwenda sambamba na upatikanaji wa walimu bado elimu bora kama alivyotaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitofikiwa. Ni lazima ujenzi wetu wa shule za sekondari ziende sambamba na upatikanaji wa hao walimu.

Sasa kwa upande wa walimu upatikanaji wake mimi nashukuru Wizara ya Elimu mwaka jana, sijui kama ilikuwa imefanya majaribio au kitu gani sielewi, mwaka jana. Wizara yetu ya Elimu ilianzisha mpaka wa kuwafundisha walimu waliomaliza kidato cha sita na hasa waliopata *division two* na *three* kwa muda wa mwezi mmoja pale Chuo cha Ualimu Morogoro. Wale walimu walifundishwa na Wizara ikawatawanya walimu hao katika shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, walichofundishwa pale ni mbinu za kufundishia tu, hawa vijana waliomaliza *form six* tayari kitaaluma wana elimu ya kutosha, lakini wanachokosa ni mbinu za kufundishia. Sasa Wizara mwaka jana mwezi Julai iliamua kuwafundisha hao walimu kwa muda wa mwezi mmoja na nina imani kabisa kwa muda wa mwezi mmoja kama wakifundishwa vizuri na kwa sababu mimi mwenyewe ni mwalimu wana uwezo kabisa wa kwenda kufundisha masomo yale ya *form one* mpaka *form four* vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nina ombi kwa Wizara ya Elimu, suala hili ni nyeti la kuanzisha kwa shule za sekondari wakazi tusiwakatishe tamaa kwa kuwapeleka wanafunzi shuleni, wanakwenda kule bila ya kupata elimu ya kutosha ili waweze kupata elimu bora. Naomba Wizara ya Elimu ijitahidi kuhakikisha kuwa inawachukuwa vijana waliomaliza *form six* wanakwenda kusoma kwa muda mwezi mmoja kupata zile mbinu za kufundishia ili waweze kwenda mashuleni na shule zetu ni nyingi sana na wakifika mashuleni waweze kuwafundisha hawa vijana wetu, kinyume cha hivyo hawa wote ambao tunawaingiza kwenye hizi shule za sekondari hawatakwenda popote na tutakuwa kama vile tunatwanga maji kwenye kinu hatuna tutakachokipata, tuwaandae walimu wa kutosha kwa mara moja tuwapeleke kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie tena katika suala hili kwa maeneo mengine katika nchi yetu kama alivyosema mchangiaji mwenzangu wa mwanzo Mheshimiwa George Simbachawene kuna baadhi ya maeneo elimu bado ni ndogo mojawapo ni Jimbo letu la Kibiti na mikoa yote ya Kusini. Maeneo hayo elimu ni duni hakuna walimu pamoja na maeneo mengine hayana walimu lakini hayo maeneo hayana walimu, walimu waliokuwepo ni wachache sasa naiomba Serikali kwa miaka ya nyuma wafugaji wenzetu wale wa Arusha waliopewa nafasi ya kupelekwa *intake* nzima ya walimu ikapelekwa Loliondo, ikapelekwa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tunaomba walimu ambao wanaandaliwa basi tuwaandae kuwapeleka maeneo ya mikoa ya kusini ambayo wanafunzi wa shule za msingi wanafaulu kwa wingi kwenda sekondari lakini hakuna, tuwapeleke huko ili na sisi watu wa mikoa hiyo ya kusini tuweze kufaidika katika karne hii ya sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie tena kwa upande wa miundombinu, kwenye upande wa miundombinu. Naishukuru Serikali ya awamu ya tatu pamoja na hii ya awamu ya nne inakazia sana suala la kuhakikisha kuwa usafiri katika maeneo mengi unakuwa mzuri kwa kutengeneza barabara na kutengeneza madaraja. Lakini katika baadhi ya maeneo kuna hali ngumu sana ya usafiri, maeneo haya ni yale ya kata nne zilizokuwa kwenye delta za mto Rufiji. Kwenye *delta* za mto Rufiji ambao kamba wanapatikana kwa wingi mpaka hivi leo usafiri ni mgumu, hakuna walimu, hakuna waganga, hakuna watumishi, watumishi waliokuwepo ni wachache na utakaowaona kule asilimia 98 ni wenyeji wa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba sana tunapolizungumzia suala la miundombinu basi hebu tutafakari ni namna gani tutakayoweza watu wa delta ya mto Rufiji zaidi ya 20,000 waweze kupata na wao usafiri wa uhakika wa kuweza kufika kwanza upande wa pili ambapo ndio tunaita nchi kavu huku na waweze kufika makao makuu ya jimbo lao na makao makuu ya wilaya. Usafiri wa kwetu kule tofauti na madaraja, kule madaraja hayawezi kutumika tunataka usafiri wa boti kubwa ziweze kutumika kuwasafirisha wananchi pamoja na watumishi ili waweze kufanya kazi kule. Sasa hivi ni kero mwalimu ukimpangia kwenda kufanya kazi kwenye delta kwenye maeneo hayo haendi, matokeo yake kwa zaidi ya miaka 27 kuna baadhi ya shule kwenye delta hazijafaulisha hata mtoto mmoja kwa zaidi ya miaka 27 mpaka mwaka huu zipo shule nyingi hazijafaulisha hata mtoto mmoja walimu hawaenda na kuna jumla ya shule 17 zilizokepo katika eneo hilo la delta. Ninaomba Wizara ya Ujenzi ituangalia na sisi watu wa maeneo ya delta kutupatia usafiri wa uhakika ili kuwavutia watumishi pamoja na wananchi wa kule waweze kupata huduma nzuri ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la MKURABITA, Serikali yetu ya awamu ya nne kwenye ilani yake ya uchaguzi imeamua kurasimisha ardhi pamoja na biashara za wananchi wetu waliokuwa vijiji ili waweze kupata nafasi ya kukopa kwenye mabenki yetu. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili lipewe kipaumbele kwa sababu wananchi sasa hivi wanayo mashamba makubwa ya mikorosho,

wana mashamba makubwa ya mazao mengine ya minazi lakini hawana fursa ya kwenda kukopa. Tunaomba utaratibu maalum utolewe ili pengine tukitoka hapa tujue tutaeleza namna gani kuhusiana na mpango huu ambao upo kwenye ilani yetu ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kuwa kuna mpango mzima wa kuwasaidia kutoa mikopo kwa vijana pamoja na akina mama, huu mpango ninaomba uwe wa kitaifa utangazwe hadharani siyo upitishwe chini kwa chini ili kila wilaya, kila mkoa, kila jimbo uweze kupata mikopo hii kwa sababu vijana ndio nguzo ya nchi yetu, akina mama ndio wamama zetu na wenye nafasi kubwa sana waliotuchangia kufika hapa tunaomba mikopo hii itolewe kwa kuangalia kwa uaminifu vile vile kwa uadilifu kuhakikisha inawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa mara ya kwanza kabisa katika Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya njema hadi leo hii. Kwa heshima na tahadhima napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wa kimbunga alioupata, napenda vile vile kumpongeza Makamu wa Rais Dr. Ally Mohamed Shein kwa ushindi mzito waliotupatia Chama chetu cha Mapinduzi. Vile vile napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar kwa ushindi alioupata, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi mzuri wa Baraza la Mawaziri kadhalika nampongeza Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa kwa umahiri iliyochambua kwa kina masuala muhimu ambayo yanapaswa kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kupata ushindi wa kura nyingi na kupitishwa na Bunge Tukufu bila ya kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kumpongeza Mwanasheria Mkuu na Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote kwa kushika nyadhifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mwakilishi wa Jimbo la Namtumbo, nimeguswa na hotuba ya Rais katika ukurasa wa 29 hadi 31 wa kitabu cha hotuba aliyoitoa wakati akizindua Bunge hili tarehe 30 Desemba, 2005. Mheshimiwa Rais alisema naomba kumnukuu: “Kilimo kitaendelea kuwa mhimili wa uchumi wetu, sekta hii inayoajiri watu wengi na ndio inayotuhakikishia upatikanaji wa chakula, bidhaa za kuuza nje na malighafi za viwanda. Vile vile uhai na maendeleo ya sehemu kubwa ya wananchi yatategemea kilimo”. Mwisho wa kumnukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Wananchi wa Jimbo la Namtumbo takriban wote wanategemea kilimo, katika msimu wa kilimo uliopita wa mwaka jana wananchi wa Jimbo la Namtumbo walizalisha tani 68,447 za mahindi, tani 3,710 za tumbaku kati ya tani 5,100 za tumbaku zilizozalishwa katika mkoa wa Ruvuma. Wananchi vile vile wa Jimbo la Namtumbo walizalisha tani 29,638 za mpunga, lakini bado wananchi hao wanakabiliana na hali duni ya maisha hasa wa kule vijijini. Kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika naomba Serikali awamu ya nne ilitizame suala la kilimo cha mkataba kwani kilimo cha mkataba katika Jimbo la Namtumbo ambao tunaozalisha tumbaku na ndio zao letu la biashara wakulima tunapunjwa sana. Wakulima wanapunjwa sana kwenye bei ya tumbaku na upunjaji huu unaanzia kwa wale wapangaji bei *classifies,* hawa wapangaji bei hawamshirikishi mkulima wa tumbaku wakati wanaichambua tumbaku ile na kupanga *grade* ya tumbaku ile ili bei yake ijulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima anapoipeleka tumbaku ile katika soko ikishachambuliwa na *classifies* basi yeye anakuja kuambiwa tu *grade* ya tumbaku ni hii na matokeo yake anapata bei ambayo siyo matarajio yake, hivyo kunung'unika na kupunjwa na kumfanya asiwe na nguvu ya kuendelea kuzalisha kwa wingi tumbaku hiyo. Tunaomba Serikali pale inapowezekana wakulima washirikishwe katika kuona tumbaku waliyopelekwa kuuzwa inakuwa na ubora gani na inawekwa katika *grade* gani ili mkulima jasho lake lisipotee kwa kupunjwa na faida iwe kwa wote kwa mkulima, mnunuzi na mfanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwamba Serikali imejitoa kwenye biashara lakini ina uwezo wa kuweka utaratibu ili mkulima asinyonywe tukumbuke zao la tumbaku linachangia kiasi kikubwa pato katika Jimbo la Namtumbo mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla. Takwimu zinaonyesha katika kipindi cha 2004/2005 wakulima wa zao la tumbaku katika Jimbo la Namtumbo walizalisha tumbaku yenye thamani ya shilingi bilioni 2,318,750,000 na walichangia ushuru wa Halmashauri milioni 115,937,500 na vile vile katika kiwanda cha sigara kilichangia pato la Serikali katika kodi zake zaidi ya bilioni 40 na kuna watanzania wengi wambao wanafanya kazi katika viwanda vya sigara. Hivyo bila ya wakulima hao wa tumbaku viwanda haviwezi kuwepo, hivyo ni muhimu sana kwetu sisi na Serikali kushirikiana kuwafanya wakulima hawa wapate nguvu ya kuendelea kuzalisha na katika umaskini na kuwawezesha kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile Serikali ya awamu ya nne ilitilie mkazo wa kutambua gharama za wakulima katika uzalishaji wa mazao ya chakula, katika bei ya mazao ya chakula kwa ajili ya hifadhi ya Taifa ya chakula iendane na hali halisi ya gharama za uzalishaji ili mkulima nae apate faida na kupata uwezo wa kuendelea kuzalisha. Mfano halisi katika msimu uliopita 2004/2005 katika kituo cha Hifadhi ya Chakula ya Taifa Songea gunia moja la mahindi la kilo 100 lilikuwa linanunuliwa kwa shilingi 12,000. Lakini gharama ya kulisafirisha gunia hilo kutoka katika kata ya Lusewa kilomita 200 kufika katika kituo cha kununulia mahindi ni kati ya shilingi 2,500 na 3,000

na nauli ya mkulima huyo ni shilingi 7,500 na gharama ya uzalishaji wake kwa ujumla ni shilingi 8,100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu hizi mkulima wa kawaida hataweza na kumudu maisha yake, ataendele kunyonywa na atauza mahindi yake pale pale alipo. Naomba kuishauri Serikali iangalie gharama za mkulima wa mahindi na vile vile vituo vya kununulia mahindi hayo yasogezwe karibu na wakulima hasa mahindi ambayo yananunuliwa kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

Kuhusu elimu Mheshimiwa Rais alizungumza katika ukurasa wa 40 naomba nimnukuu: "Hakuna Taifa litakalopata maendeleo bila kuendeleza elimu na hivyo kuendeleza elimu nchini itakuwa *agenda* muhimu ya Serikali ya awamu ya nne", Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, MMES imeshaanza lakini naomba kukumbusha Serikali ya awamu nne iangalie zaidi maeneo ya pembezoni hususan wilaya zetu mpya kama ya Namtumbo. Wilaya yetu ya Namtumbo ina upungufu wa walimu 332 na ina shule za msingi 92 na pia ina shule za sekondari saba na tuna shule za sekondari za kata ambazo tumejenga tano, lakini ziko katika linta karibu na kuezekwa katika kiwango cha boma. Lakini hatuna uwezo, wananchi wa Jimbo la Namtumbo kwa nguvu zao wamefikisha hapo hawana uwezo wa kuezeka na kumalizia shule zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kupitia Wizara ya Elimu, huu mpango wa MMES utuharakishie ili tuweze kumalizia shule hizo kwani mwaka 2005 katika Jimbo la Namtumbo wanafunzi waliofaulu na kupata nafasi ya shule ni 862 lakini waliofaulu na wakakosa nafasi kwa uhaba wa shule za sekondari ni 1,805 hivyo kuna nafasi kubwa sana….

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi walau na mimi nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nataka na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wake na Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa walioupata kwenye uchaguzi mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa kwanza kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Monduli na pili kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sina shaka atafanya kazi nzuri kwa sababu namfahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Spika pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kutuongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza wote waliochaguliwa na walioteuliwa kwa nafasi mbalimbali.

Mwisho, naomba nitumie nafasi hii na mimi niwashukuru wananchi wa Jimbo jipya la Babati Mjini. Nilikuwa Mbunge wa Jimbo la Babati Mashariki lakini baada ya Mkoa wa Manyara kuundwa na Mji wa Babati kupata Halmashauri ya Mji basi Jimbo likapatikana na mimi nashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge wa kwanza kwa kuanza na Jimbo hilo jipya la Halmashauri ya Mji wa Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kweli imebainisha majukumu ya msingi. Kwanza ameeleza yaliyotendwa na awamu zilizopita. Alieleza majukumu ya Awamu ya Kwanza yalikuwa nini, Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu. Lakini vile vile kwenye hotuba yake hii ameainisha vizuri sana majukumu ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 13, Mheshimiwa Rais ameeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 imetamka bayana majukumu mawili ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwanza amesema kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Lakini la pili amesema kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umaskini. Haya ndiyo majukumu mawili ya msingi yaliyoelezwa kwenye Ilani ambayo Mheshimiwa Rais ametaka Serikali ya Awamu ya Nne ijielekeze huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mengi ambayo tungependa kuyasema basi nadhani tuseme machache kwenye maeneo ambayo kwa kweli tunaona ni muhimu hasa katika hatua hii ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kusema ukitaka kujua sura nzuri ya Serikali, anza pale vijijini, nenda kaangalie Serikali za Vijiji. Mimi natoa ushauri wa kwanza kabisa, jukumu la kwanza liwe katika sehemu ya utawala bora twende tukaangalie muundo wa Serikali za Vijiji na namna gani tunaweza tukaziwezesha zile Serikali kufanya kazi zake maana Serikali za Vijiji ndio kitovu cha maendeleo. Kwa hiyo, tuanzie pale ili kila mtu akifika pale chini aone kabisa kwamba sura ya Serikali ndio hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukienda vijijini, Serikali za Vijiji zinalaumiwa kweli kweli hazifanyi mikutano lakini hivi kweli tumewawezesha kiasi gani? Hazifanyi mikutano, hawatoi taarifa kila baada ya miezi mitatu kama wanavyotakiwa lakini tumewawezesha kiasi gani? Kwa hiyo tuangalie pale namna ya kuwezesha Serikali za Vijiji zifanye kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuangalie Halmashauri za Wilaya, nadhani muda umefika sasa tuondokane na mtindo wa kuweka fedha nyingi kwenye bajeti huku juu, huku ambapo kazi kubwa ni kuratibu sera, fedha zije kwenye Halmashauri za Wilaya, zije kule. Madaraka yote karibu tumeyapeleka pale na kama hatupeleki fedha za kutosha kule lakini huku juu tunabakiza fedha nyingi halafu tunasema tunaratibu, kila kitu tunasema kikatekelezwe na Halmashauri za Wilaya kwa kweli nadhani hii azma iliyotajwa hapa hatutaweza kuifikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kabisa kwamba tuwe na sura mpya namna ya kutengeneza bajeti zetu na tuone pale Halmashauri za Wilaya tunaweza tukaziwezesha namna gani. Kwa mtindo wa kutoa Sh.150mil kwa barabara, Halmashauri zina barabara karibu 10 maana yake ni kwamba unaweza kutumia Sh.15mil kwenye barabara, hivi kweli tutakuwa tunazungumza habari ya maendeleo? Kwa hiyo, lazima tufikirie sana ni namna gani tutabadilisha mtindo wetu wa kufanya kazi na kupeleka maendeleo kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo vile vile nilitaka tuangalie hivi Mkurugenzi tumempa majukumu mangapi? Hivi Wakurugenzi wa Wilaya sasa hivi ukienda kweli wanafanya zile kazi za Ukurugenzi au wanafanya kazi za mikutano tu, kuwa Wenyeviti wa mikutano mbalimbali? Kila siku wako kwenye mikutano, ratiba toka siku ya kwanza mpaka mwisho wa mwezi wako kwenye mikutano kwa maana hiyo hawana nafasi yoyote ya kusikiliza au kushughulika na maendeleo ya Wilaya zetu.Ni muhimu Serikali iangalie sasa eneo hili lirekebishwe namna gani ili Wakurugenzi wawe na kazi ya kusimamia maendeleo. Hili ni jambo muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameonyesha mtindo mpya kabisa wa kufanya kazi, amekwenda kwa kila Waziri. Sasa nashauri na nini Waheshimiwa Mawaziri njooni kwetu muongee na sisi. Mheshimiwa Rais ameongea na ninyi na ninyi sasa mtuite mmoja baada ya mwingine, kila Mbunge na Jimbo lake tuwaeleze mambo yetu na ninyi mtueleze ya kwenu. Huo ndio mtindo mzuri ili tusikae hapa miaka mitano unakuta Mheshimiwa Mbunge kila hotuba akipata nafasi kwenye bajeti barabara yangu fulani, maji, miaka mitano inapita maji hajapelekewa barabara hakuna, hebu na sisi tuwaeleze tunataka nini katika miaka mitano na ninyi mtueleze uwezo wenu wa kutusaidia katika miaka mitano ni upi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kabisa kila Waziri watufuate tuongee nao na sisi tuwaeleze ya kwetu. Nina hakika kama tutakwenda hivyo hata maswali yatapungua. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Yes!

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Maana tutakuwa tumeelewana kwamba miaka mitano Mheshimiwa Waziri labda wa Nishati na Madini nimemueleza kwamba nataka umeme kwenye mji wa Babati, kwenye maeneo fulani na yeye anasema mimi kwa kweli kwa uwezo wangu nadhani nitafikia hapa. Basi nitakuwa sina haja ya kuuliza mimi

nitakuwa naangalia tu kila mwisho wa mwaka umekwenda vipi, tumefikia wapi. Kwa hiyo, nashauri hivyo kila Wizara kwa kweli ihakikishe imepata vipaumbele kutoka kwa kila Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 kwenda 2000 tulifanya baadhi ya mambo haya hasa kwenye sekta ya nishati na madini. Nakumbuka kwenye upande wa nishati na madini vijiji vingi katika kipindi hicho ndivyo vilivyoweza kupata umeme mpaka mwaka 2002 baadaye TANESCO ndio hiyo haikushughulika tena kuhakikisha kwamba vijiji vinapata umeme. Lakini kila mwaka tulikuwa tunaona kabisa kwenye hotuba ya Waziri vile vijiji ambavyo vilikubaliwa vinaingizwa na kweli vinawekewa umeme na Waziri anatoa taarifa na unakuta tunasonga mbele. Hii ni kwa sababu tuliweza kukaa na wale Waheshimiwa Mawaziri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo mengine ambayo kwa kweli yamesemwa kwenye Ilani mengine yanahitaji yaanze sasa. Kwa mfano yameguswaguswa hapa kidogo haya masuala ya kuwawezesha wananchi hasa mpango wa MKURABITA ambapo tumekubali kwamba tutarasimisha rasilimali pamoja na biashara za wananchi. Sasa hivi vijana, tumesema vijana tutawawezesha, vijana wanafanya kazi nyingi sana utakuta vijana wanajishughulisha na kazi mbalimbali, wengine wana gereji ndogo ndogo za baiskeli njiani, wengine ni *shoe shiners* na nini, kwa hiyo wanazo kazi nyingi sana, wanatengeneza madawati, wanatengeneza meza, stuli ni nani hasa anaratibu vitu vyao hivi ambavyo kwa kweli vinasaidia kuwapa ajira? Sasa kwenye mpango huu wa MKURABITA nilidhani tuanze mapema tusije tukarudia ule mpango kwamba fedha zilitengwa kwa makundi na wanawake pamoja na vijana tukahamasisha vikundi vingi sana lakini vingi mpaka tumemaliza vipindi vyetu vikundi hivyo havikupata hiyo mikopo, tusirudi huko. Tuanze sasa na tujue kwamba vikundi ni vingapi na uwezo wetu ni upi. Tukifikia hapo nadhani kwa kweli itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine niseme kidogo tu juu ya huduma za jamii. Mimi nimepata bahati ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Huduma za Jamii na nashukuru walionichagua na kwa maana hiyo tutashughulika sana na mambo haya ya afya na elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya, nadhani ni vizuri Wizara ya Afya sasa ikaangalia mambo fulani fulani kwenye sera hasa sera zile za uchangiaji. Wananchi wanashindwa kabisa kulipa fedha kwa ajili ya matibabu, tumeweka mambo mengi, mifuko ya SHF na nini lakini hii sera ya uchangiaji hebu tujiulize ni vema tukafika mahali tukajiuliza inachangia kiasi gani, ni kiasi gani hasa kama sio asilimia 0.000 na je kulinganisha na kero zake ni vema iendelee kuwepo au isiendelee? Kwa hiyo, kuna mambo ya kuangalia sana kwenye eneo hili la afya. Kama wananchi walifika mahali wanashindwa kulipa ada za Sh.2,000 kwa watoto wao wa shule za msingi sasa kweli wana uwezo wa kulipa matibabu kila siku? Ni lazima tuangalie. Je, huu mchango kwenye sera hii unasaidia namna gani? Kuna mambo mengi sana ya kuangalia kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la elimu, elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu, kuna mambo mengi sana na mengi yanalalamikiwa, mambo ya mitaala na

nini. Kwenye Wizara ya Elimu, utakumbuka katika Bunge lililopita tulikuwa na matatizo makubwa sana hasa ya madai na matatizo ya kero za muda mrefu za Walimu na tukizingatia kwamba Walimu ni karibu 50% ya watumishi wa nchi hii. Sijui kama Serikali imeanza kufanyia kazi kero ambazo zilikuwa zimeainishwa kwenye Tume ambayo ilikuwa imeteuliwa na Waziri Mkuu, kuna mambo mengi ya kujifunza pale.

Tuna haja pengine ya kuangalia sheria zetu mbalimbali, ile ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, Na.25 ya Elimu ya mwaka 1978 na Sheria zile za Serikali za Mitaa, Na.7, Na.8, Na.9 ya 1982, kuna haja ya kuangalia mambo haya kwa undani sasa. Hiki ndio kipindi kizuri cha kuangalia kwa kweli kama tunakwenda vizuri kwenye maeneo hayo au namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo kero za bima za Walimu zilizoiva. Deni liliwahi kufikia Sh.3.5bil sijui mpaka sasa kama Walimu wamelipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuungana mkono na wale wote ambao wamesimama hapa wakatangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, nami nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuzungumza kwa mara ya kwanza tokea tuanze Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kunikubali kuteuliwa kuwa Mbunge na hatimaye kuweza kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Kwamtimpura. Vile vile napenda nitoe shukrani za dhati kabisa kwa wananchi wangu walionichagua wa Jimbo la Kwamtimpura ambalo liko Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile napenda nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete. Vile vile nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa kabisa wa kishindo ambao ameupata. Vile vile nimpe pongezi Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge bila kujali kambi gani wamepitia hatimaye kuingia ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi tena za dhati sana kwa hotuba nzuri kabisa ambayo Mheshimiwa Rais aliisoma hapa mbele yetu na sote ni mashahidi kutokana na mtitiriko mzima ambao Mheshimiwa Rais alikuwa akisoma hotuba hii na sote ni mashahidi kwamba pale mwanzo alipokuwa akianza na takribani kila alipokuwa akiendelea tulikuwa hatukuchoka kuendelea kupiga makofi kwa namna hotuba ilivyokuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yangekuwa ni mashairi tungesema ule urari wa mizani katika mashairi yale ulikuwa umetimia sana. Kwa hiyo, haya tunayoyazungumza sote humu kwa kweli ni nyongeza ndogo ndogo tu lakini kila kitu kilikuwa kimebebwa

ndani ya hotuba ile na ilikuwa imetoa mwelekeo mzuri sana wa mwanzo mzuri ambao Mheshimiwa ameanza wa kuingoza nchi hii na mifano hivi sasa tunaanza kuiona kwa bidii na juhudi aliyoanza nayo na huko tunakoelekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo yaliyozungumzwa, mimi nitakuwa nagusia kidogo kidogo. Kama nilivyosema ile hotuba imejitosheleza sana lakini kwanza nami nianze kidogo tu kwa kuligusia hili suala la siasa ambalo ameligusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa anazungumza bahati nzuri kuna mwenzangu katoa ufafanuzi mzuri sana hapa wa hali ya siasa ya Zanzibar. Siasa ya Zanzibar na hii ya huku Tanzania Bara ipo tofauti kidogo, hata aina ya upinzani, upinzani huu tulio nao huku upande wa Tanzania Bara unaonekana ni upinzani wa kimaendeleo zaidi kuliko ule ambao tunakutana nao sisi upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ambayo yanajitokeza baada ya uchaguzi, kutotambuliwa kwa Serikali, Rais pamoja na viapo ambavyo tunakula sisi humu, maana yake wengine tunaapa kwamba tutailinda na kuihifadhi hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini tunasahau ndani ya Katiba hiyo imeitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sote tumekula kiapo kuikubali Katiba hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nigusie kidogo hili suala linalojitokeza kwa upande wa siasa zetu sisi kule upande wa pili wa Jamhuri. Wakati mwingine utasikia mtu anapiga kelele za maonevu anaonewa lakini ukichunguza kwa ndani huyo mpigaji kelele yeye ndiye kuchokonoa mahali, kaenda kuchokoza lakini anaanza yeye kupiga kelele kwa hiyo yule aliyekuwa hajaona ile hali iliyojitokeza pale anahisi yule mkubwa ndio kaanza kumchokoza yule mdogo kumbe yule mdogo ndio kaanza kumkanyaga huyo mkubwa na hatimaye ndio yakajitokeza hayo ambayo yanaonekana. (*Makofi*)

Hii imefanana sana na hadithi ya mtoto, watoto wadogo wawili wanapokuwa wanacheza mmoja mkubwa mwingine mdogo, inaweza kutokea yule mdogo akamchokoza kaka au dada yake lakini kwa sababu kwa kutaka kurudiwa yule labda kwa kutiwa adabu yule mdogo akawahi kupiga kelele wewe mzee ukiona sasa unamgeukia yule mkubwa wewe unataka kumfanya nini huyu mwenzio? Ndio hali ya siasa ambayo tunakwenda nayo lakini ni hali ambayo wenyewe tumeshaizoea na tustahimiliwe kwa sababu safari na siku zinakwenda kama tunavyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kuongelea sana huko, nitoke huko. Katika ukurasa wa 22, Mheshimiwa Rais aligusia suala la rushwa. Lakini sasa mimi kila nikikaa najiuliza, sijui tunaanza kuchora wapi mstari baina ya rushwa na takrima. Kwa sababu wakati mwingine pengine Mheshimiwa anaweza kutoa kitu mahali kidogo sana lakini kitu kile kikawa ni rushwa lakini mwananchi wa kawaida akatoa mahali pale pale tena kikawa kikubwa zaidi kisiwe rushwa. Lakini zaidi tunatafsiri kwa kuona lengo la kutoa kile kitu unachokitoa baadaye unatarajia kufanya kitu gani.  Mara nyingi vitu ambavyo tunavitoa tunapokaribia katika chaguzi, vitu vile mara nyingi sana vinahesabiwa kwamba

ni rushwa pamoja na kwamba uliwahi kutoa ahadi siku za nyuma lakini labda kwa kuwa siku zinamalizika unataka kuziba yale mapengo usije kuulizwa maswali kwa kukamilisha zile ahadi zako unajikuta sasa kwamba ile ahadi utekelezaji wake unahesabiwa kuwa ni rushwa. Sasa hapa ndio pana *debate* kubwa sana inabidi tukae kitako tuanze kujiuliza jamani rushwa inaanzia wapi na inaishia wapi na hii takrima inaanzia wapi, wapi tunachora mstari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa ni gumu sana. Rushwa kwa maana ya rushwa hata kama tutakwenda kwa upande mmoja tu wa rushwa tukiacha pembeni takrima maana yake nathubutu hata kusema hili tatizo tulilonalo la UKIMWI naona kama tunaweza kupata dawa lakini rushwa ikakosa dawa kwa kipindi kirefu. UKIMWI unaweza kupata dawa baadaye maana sasa hivi tumeanza kupata dawa za kuongeza umri, kuna mambo yanatiatia moyo lakini kwenye rushwa kila siku vinaanza kuja vitu vipya mara unaambiwa hiki sasa hivi ukifanya ni takrima mara hii takrima hatuitaki tena tunarudi tena kwenye masuala ya rushwa.

Nigusie jambo lingine dogo vile vile. Jambo hili Mheshimiwa Rais kaligusia katika ukurasa wa 53 nalo ni suala la michezo. Mheshimiwa inauma sana kuna mashindano makubwa yanatokea lakini sisi Tanzania tumekuwa washangiliaji wa mashindano hayo na sio washiriki. Inauma kwa sababu hivi sasa hivi ndani ya Tanzania watu wamegawana timu, mimi nachukulia suala la mpira wa miguu kwanza, watu ndani ya Tanzania wana timu huko Uingereza, kuna mtu mpenzi wa *Manchester United* hapa, *Arsenal* lakini timu zetu za Tanzania tumezisahau na hii yote inatokana na ukweli kwamba tumeshindwa kupiga hatua kuweza kufika mahali kuweza kupata moyo. Lakini hili tunaliangalia juu hili linatoka mbali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo zamani kulikuwa na utaratibu wa michezo katika *school* lakini sasa hivi suala hilo limeondoka kabisa. Shule zetu sasa hivi hakuna michezo lakini tukumbuke wale wanariadha na wanamichezo katika fani nyingine za michezo waliowahi kuleta sifa nchi hii ukichunguza historia zao walianzia mashuleni. Kwa hiyo kule ndiko tunakoweza kupata chimboko la wale wanamichezo ambao hatimaye wanaweza kutuwakilisha na sisi tukawa na jina kama hizo nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri Serikali kwa makusudi kabisa ikarejesha hili suala la michezo mashuleni. Suala la michezo ni muhimu na wenzetu katika nchi nyingine kwa mfano Marekani huko mtu anapata *scholarship* kutokana na kipaji chake cha mchezo tu anapata fursa ya kuendelea kusoma kwa hiyo na sisi tungeweza kuandaa mazingira kama hayo ili kuweza kunyanyua na kuibua vipaji vya michezo kutokana na vijana wetu na hatimaye tutaachana na kushangilia timu za Uingereza na kwingineko na kuanza kushangilia vijana wetu na hatimaye na bendera yetu sisi ikawa inapepea kwenye maeneo mengine tukawa tunashangilia kama hili kombe linalomalizika hivi karibuni la Klabu Bingwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kengele inanikumbusha muda nilionao ni mchache sana, nigusie suala la usalama wa raia. Mimi nitawaunga mkono wale wote ambao wamesimama hapa wakatoa pongezi zao sana kwa Jeshi la Polisi kutokana na

wimbi la masuala ya ujambazi lililojitokeza. Kuna watu kwa makusudi kabisa wamesimama na kuanza kuwalaumu. Nadhani hapa tusimame tukawalaumu Polisi kwa sababu wanajitahidi sana lakini tukubali vile vile kwamba zana ambazo wanazitumia ni duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kabisa Polisi kwenda kukabiliana na jambazi mwenye silaha ukaenda na rungu, hata mimi ningekuwa Askari ningekimbia, nisingekaa., unakwenda kukabiliana na jambazi mwenye silaha. Tuige mifano ya maeneo mengine, tuanze kuwanyang'anya virungu Askari wetu tuwakabidhi silaha katika kukabiliana na suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Marekani katika Jimbo la California kuna wakati fulani walikwenda majambazi wenye silaha, *AK 47* zilitumika wamekwenda kuibia Benki, kama haya matukio yanatokea hapa kwetu sisi. Polisi wakati huo katika mji walikuwa wanatumia bunduki hizi za marisao hizi, *pamp action* walishindwa kuwakabili wale kwa sababu wale majambazi wanatafuta na njia wanayotaka kupita hata kama kuna Askari watapita pale pale kwa sababu Askari wale watakapoanza kupiga bunduki zao Askari wote hulala chini majambazi wakapita na walikuwa wamejiandaa uzuri sana. Kwa hiyo hali kama hiyo baadaye wakaa kitako wenzetu wakaangalia wakaona hapana haiwezekani kabisa sisi hawa Askari wetu wanalinda halafu wale majambazi wana silaha ambazo ni bora zaidi. Sisi cha kufanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba Askari wetu, kwa sababu silaha wanakamatwa nazo majambazi, tuangalie aina ya silaha wanazotumia majambazi tuwape Polisi wetu silaha bora zaidi kuliko hizo walizonazo majambazi ili waweze kuwakabili na hatimaye wimbi hili litaondoka na sio silaha tu tuwape na mafunzo ya kuweza kukabiliana na hii. Askari wetu wanajitahidi lakini wamezidiwa na wala hawalaumiki kukimbia, mtu yeyote atakimbiza roho yake anapokabiliana na hali kama ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi zangu sana kwa namna wanavyojitahidi lakini hali ya vifaa sio nzuri kwa hiyo Serikali iwafikirie ili waweze kukabiliana na majambazi. Mimi naamini wanaweza kuliondosha hili tatizo lakini Serikali iwafikirie, tuwabadilishie zana walizonazo tuwape zana ambazo wataweza kukabiliana na majambazi hatimaye raia wa kawaida naye ataweza kufanya mambo yake bila ya kuwa na hofu.Sasa hivi hata kwenda Benki kila mmoja anaogopa maana yake kama ingewezekana hawa Benki wakatuwekea vibanda humo njiani tukawa tunatumia kadi tusiende kabisa kule, wabaki wao na makaratasi yao, mtu unakwenda kufungua akaunti kwa makaratasi halafu mchezo umekwisha, maana sasa hivi hali inatisha, Askari wabadilishiwe zana walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Rais na natoa pongezi sana kwa namna alivyoweza kutoa hotuba nzuri na kwa maana hiyo hotuba hii naiunga mkono, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili nami niungane na wenzangu kutoa mchango kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwanza kwa ushindi wake mkubwa ambao ameupata kwenye uchaguzi uliopita lakini pia nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa ushindi mnono na wa heshima kubwa alioupata. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa ushindi alioupata ambao ni heshima kubwa kwa Chama chetu cha Mapinduzi. Pia nikupongeze sana wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Bunge hili Tukufu kuwa Naibu Spika kwa kura nyingi sana. Lakini pia nami niungane na wenzangu kwa kutuma salamu za pongezi kumfikishia Spika wetu kwa ushindi wa kishindo alioupata hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za pekee, naomba nizifikishe kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kwanza na Mheshimiwa Rais lakini pia kwa kupitishwa na Bunge hili Tukufu kwa kura nyingi sana. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Shukrani na hongera nyingine nazifikisha kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Rais wetu, Mheshimiwa Kikwete. Lakini pia niwapongeze sana Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa walioteuliwa toka miongoni mwetu kuwa katika mstari wa mbele kuunda Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze kwa namna ya aina yake Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuweza kuchaguliwa na wananchi kwa kuaminiwa wakapewa hizo dhamana za kuja kuwasilisha hapa Bungeni, nasema hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ambayo haifananishwi, naomba niwashukuru na kuwapongeza sana wapiga kura wa Jimbo la Sengerema ambao bila wao mimi leo nisingekuwa nimesimama hapa kuweza kutoa mchango katika hotuba hii ya Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, natoa shukrani na pongezi nyingi sana kwa wapiga kura wa Jimbo langu la Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, naomba sasa nami nichangie machache kwenye hotuba hii. Kwanza naiunga mkono kwa asilimia zote mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hotuba iliyokuwa imeandaliwa kwa makini na ni dira tosha kutuelekeza sisi kama wawakilishi wa wananchi kutekeleza majukumu ya kusukuma gurudumu la maendeleo la Taifa letu.

Katika mchango wangu, naomba nianzie na ukurasa wa 23 wa hotuba hii nzuri na inayoonyesha uchungu wa kweli wa maendeleo ya Taifa letu.

Pale kwenye mikakati ya kupambana na rushwa katika Taifa letu, yenye lengo la kumhakikishia kila Mtanzania maisha bora na kuijenga Tanzania yenye neema. Naomba ninukuu machache katika hili kabla sijaanza kutoa mchango wangu, niko kwenye kipengele cha mikataba. Mambo ya rushwa yapo mambo …

**NAIBU SPIKA:** Sogea zaidi kwenye *mic* tafadhali.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nanukuu baadhi ya maneno ambayo yamo katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wetu katika ukurasa wa 23 inayosema katika harakati za kupambana na rushwa yapo mambo miwili mengine ambayo tutayaangalia kwa karibu, la kwanza ni mikataba. Tutaangalia upya taratibu za mikataba mbalimbali inayoingiwa na Serikali, Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea kwa niaba ya kuongeza uwaji na uwajibikaji, mikataba ni mwanya mkubwa wa rushwa hasa zile kubwa kubwa, nadhani wakati umefika wa kuwa na taratibu thabiti za kubana na kuziba mwanya huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisema jambo ambalo kwa hakika hapa limeonyeshwa na Mheshimiwa Rais wetu ambalo limemgusa sana lakini kwa kweli ni kilio cha Watanzania wengi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanafahamu limekuwa likisemewa kwa muda mrefu sana mimi naomba jambo hili lifikie wakati sasa wa kutolewa ufafanuzi na tuwe na msimamo thabiti sisi kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba baada ya mkutano huu kuwe na tamko rasmi kutoka Serikalini, ushauri wangu ni kwamba Bunge lipewe madaraka na liwe na haki ya kuipitia mikataba ambayo Serikali kwa niaba ya Watanzania imekuwa ikiingia na wawekezaji mbalimbali katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa kwenye semina kule Dar es Salaam tulipata ufafanuzi wa kina kwamba kwa sheria zetu za nchi yetu zikiongozwa na Katiba ambayo ndiyo sheria mama kwa sasa hivi haziliwezeshi Bunge kuweza kupitia mikataba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Bunge ndiyo chombo kikuu katika ile mihimili mitatu ya dola, ndiyo lenye mamlaka makubwa ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo Serikali ndiyo mtekelezaji wake. Lakini kuashiria lilivyosimama kwa sasa hivi pamoja na utashi wa kiasa tulio nao lakini hatuna nyenzo, hatuna *instruments* ya kuweza kufikia hili na kulitekeleza hili, Sheria haipo inayoruhusu leo sisi kama Wabunge pamoja na utashi wetu wa kisiasa tulio nao na kilio cha wananchi cha muda mrefu sana na uzoefu umeonyesha na ninaomba katika hili niazime maneno ya Waziri Mkuu alipotukumbusha pale Dar es Salaam siku ya ufunguzi wa semina kwamba historia ni Mwalimu Mzuri Sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshajifunza na tuna uzoefu wa kutosha sasa, mikataba mingi ambayo Serikali imekuwa ikiingia hapo nyuma na wawekezaji mbalimbali ama na washika dau kwa namna moja ama nyingine wa aina mbalimbali mingi imekuwa ina utata na kwa kweli kwa kiwango imepelekea kutufikisha mahali pagumu sana. Sitaki kusema lakini najua Waheshimiwa Wabunge mnafahamu mikataba ya Shirika la Kampuni ya Simu *TTCL*, mkataba wa *IPTL*, tunafahamu kilichofanyika *NBC* wakati inabinafsishwa. Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanafahamu kinachoendelea katika makampuni katika mikataba ambayo imeingia na wawekezaji wakiwemo wawekezaji katika Sekta ya Madini. Hiki ni kilio cha watu na watu hawawezi kunung'unika hivihivi kuna mambo ambayo yameifikisha nchi hii pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najua si wakati wa kulaumiana ninaomba tubadili *approach* ya jambo hili, naomba wakati tunajadili umuhimu wa Bunge kuwa na mamlaka ya kupitia mikataba hii naomba tuweke pembeni nadharia ile ya dhana ya *Separation of Power* ya kusema mgawanyo wa madaraka ambao mihimili hii mitatu ya dola inapaswa iwepo. Naomba *approach* huu ni mkakati wa kitaifa, tuna mkakati wa kitaifa wa kuweza kujenga Tanzania yenye neema lakini pia yenye lengo la kumhakikishia kila Mtanzania maisha bora. Tukishakuwa na mkakati wa pamoja tukaliona hili katika mkakati wa kitaifa badala ya kuliona kwa kujikita katika hili huo mgawanyo wa madaraka basi Katiba tutairekebisha na hasa ibara ya 63(3) tukitumia vile vifungu vya Katiba, mamlaka ambayo Bunge limepewa tukairekebisha Katiba ikaliruhusu Bunge hili kupitia mikataba ama kuridhia wakati ambapo litaona kwamba linahitaji kufanya hivyo tutakuwa tumeimarisha mkakati wetu wa kuziba mianya hii ambayo Mheshimiwa Rais wetu anaiona ni mikubwa mikubwa lakini pia Watanzania wengi wamekuwa wakililia hili jambo lifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba lakini pia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali walione kwa utaifa zaidi badala ya kuliona katika nadharia ya mgawanyo wa madaraka. Katiba irekebishwe ili Bunge hili tukufu liweze kuwa na mamlaka ya kuweza kupitia hiyo mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba pia niongelee sera ya madini. Mimi ni mmojawapo wa wawakilishi wa wananchi ambao wanatokea kwenye maeneo ambayo uchimbaji wa madini unafanyika. Katika hili naomba Sera ya madini tuirekebishe nitamke bayana ili tuweze kuwa na nafasi ya kujua ni jinsi gani wachimbaji wa madini kwenye maeneo ambayo yanazunguka hii migodi wanaweza kufaidika na ile faida ambayo inatokana na shughuli za uchimbaji na hii sera isiishie kwenye madini tu naomba iende zaidi ya hapo kwenye sekta nyingine kwenye sehemu nyingine za maeneo ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa makusudi kwa sababu najua Waheshimiwa walioko hapa hata wananchi ambao hawapo hapa wanafahamu kurudisha faida kwa mfanyabiashara ama mtu yeyote anayejishughulisha na shughuli kubwa ya uzalishaji ama ya kibiashara ambayo inamletea faida kubwa kurudisha sehemu ya pato analolipata au faida anayoipata kwa wananchi wake ile *cooperate social responsibility* ni kitu cha kawaida sana na hata nchi zilizoendelea zinafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali iangalie hili, sera hii ya madini irekebishwe kwani hatuwezi kujua ni mambo yapi ambayo wawekezaji wanaweza kutusaidia kwa kufanya hiyo tutakuwa tumeongeza nguvu katika huu mchakato na mkakati mzima wa kitaifa wa kumhakikishia kila Mtanzania maisha bora. Kwa hiyo naomba Serikali ilichukulie kwa uzito na wakati labda wa majumuisho tuambiwe msimamo wa Serikali ukoje katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana sera hii irekebishwe tujue tunafaidika katika mambo gani sisi ambao tunatoka kwenye maeneo ambayo shughuli kubwa za kiuwekezaji zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho najua nimegongewa kengele kuashiria muda unaelekea kuisha naomba niipongeze sana Serikali kwa hatua ya hivi karibuni vyombo vya habari wiki iliyopita na hata wiki hii kwamba lile jambo ambalo kwa miaka mingi lilikuwa limeshindikana la kuwa na kiwanda cha kusafisha dhahabu sasa linaelekea kupatiwa tiba. Naipongeza sana Serikali kwa kuwapata wawekezaji kutoka Jumhuri ya Czech ambao kwa mujibu wa taarifa nilizozipata kutoka kwenye vyombo vya habari kiwanda kilijengwa Mwanza.

Lakini naomba nitahadharishe jambo moja, tulipokuwa kwenye semina pale Dar es Salaam tuliambiwa wawekezaji waliopo hapa wameshindwa kujenga viwanda vya kusafisha na kukata madini kwa sababu gharama za kujenga viwanda hivyo ni aghali sana na hazileti tija na faida kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niishauri Serikali pengine itufafanulie baadaye kwamba huyu mwekezaji ambaye anasema ana uwezo wa kujenga kiwanda ambacho kitasafisha madini kwa 99% ni mazingira yapi yaliyopelekea mpaka yakamuwezesha yeye kuweza kugharimia na akapata faida wakati hawa wamekuwepo hapa muda mrefu sana na wamesema kwamba kwa mfano nitolee mfano wa Kampuni ya Kahama inasema hata madini yanayochimbwa pale utenganishaji wake ni wa 45% tu maana yake ni kwamba 55% inapelekwa kwenda kusafishwa nje.

Ndiyo maana kuna ile hoja ya mchanga kubebwa kwenda kusafishwa nje, sasa hapa tunaomba tusaidiwe kufafanuliwa ni kitu gani ambacho mwekezaji huyu amepewa ama labda kuna misamaha fulani amepewa ambayo inamwezesha yeye kuwekeza hapa na akapata faida kwa sababu haiingii akilini sawasawa kama hawa wamekuwepo kwa muda mrefu wamekataa wanasema gharama za kujenga kiwanda cha kutenganisha hakiwezi kuwapa faida huyu mwekezaji anawezaje? na 49% ya huyu mwekezaji ni Watanzania wazalendo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ni mambo ambayo tunatakiwa tuyaangalie kitaifa zaidi ili tuweze kujua hasa historia pia inatusaidia kujua kwamba huko nyuma ilikuwaje kulikoni huko nyuma? Na sasa tunakoelekea tujifunze n kutokana na historia ili tuweze kukabiliana na haya mambo lakini kwa faida ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna mengi ya kusema lakini naomba nisema kwamba Sengerema kuna njaa na ninaomba iwemo katika orodha. (*Makofi*)

Naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bahati yetu mbaya ni moja kwamba Wabunge walioingia safari hii ni mafundi wa kuongea wote kwa ujumla kwa hiyo hakuna anayeokoa muda. *(Kicheko)*

Orodha yetu tuliyoibandika pale nje ina wachangiaji 102 ni wale tu walioandikishwa na wako wengine wengi kabisa ambao wanadai kwamba waliandika majina hayakuonekana sasa tunaandika pale kusudi kila mtu aone kabisa ni mtiririko tunaosema wewe uliyezungumza ni wewe kufuatana na tulivyopanga kwa hiyo hatuna namna ya kusema tunamchukua mwingine wa mwisho tukamuweka wa kwanza hapana haiwezekani maana yake tutaanza kugombana hapahapa.

Sasa kesho ni Alhamisi tarehe 9 tulivyoangalia wastani wa kuzungumza kwa siku kwa sababu wote ni mafundi wa kuzungumza tunaweza kuongea watu 20 tu na hapo tumejitahidi sana, 20 tu kwa siku sasa kama mko 102 na ni 20 tu kwa siku tarehe 10 tunategemea kuiachia Serikali ianze kujibu hoja zote kipindi cha mchana kwa hiyo tutakuwa na wengine 10 tu jumla 30 tu kwa hiyo mfahamu kwamba tutakapofika kesho kutwa idadi kubwa ya watu walioomba kuchangia hawatapata nafasi.

Tuna utaratibu wa kuandika mnaweza wengine wote mkaandika maana tumefanya hesabu karibu watu 50 wataachwa kwa hiyo wale wanajiona namba zao ziko mbali sana waanze kuandika tu kwani hatuna namna. Kwa hiyo hilo ndilo tangazo la kwanza naomba kwa hilo tuelewane hatuna namna.

Kuna Mheshimiwa mmoja alitoa mapendekezo kwamba labda tungepunguza zikawa dakika 10 nilipofanya hiyo nikapata tatizo kwamba dakika tulizozihitaji zilikuwa 900, dakika tulizokuwa nazo zilikuwa 465 kwa hiyo maana yake ni wachangiaji 46 tu basi nayo nikaona haiwezekani basi tuendelee na kanuni kama ilivyo kwamba mjue asilimia kubwa mtabakia 50 watabaki.

Kwa hiyo baada ya kusema hayo naomba nitangaze kwamba baada ya kikao hiki baada ya kuahirisha wale Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wabakie hapa kwa kazi ndogo ambayo mliicha mchana. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba kuahirisha kikao mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 9 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*